14 APRILI, 2026

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Nane – Tarehe 14 Aprili, 2026

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tunaendelea na Mkutano wetu wa Tatu, Kikao Nane, leo tarehe 14 Aprili, 2026.

Katibu.

NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Tunaanza na maswali Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Cornel Lucas Magembe, Mbunge wa Chato Kaskazini.

Na. 74

Ujenzi wa Kituo cha Afya Nyamiembe

MHE. CORNEL L. MAGEMBE aliuliza: -

Je, lini Serikali itatoa fedha za ujenzi wa Kituo cha Afya Nyamirembe ambapo ni Makao Makuu ya Tarafa?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF) alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Cornel Lucas Magembe, Mbunge wa Jimbo la Chato Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 hadi mwaka 2025/2026 Serikali imejenga na kuboresha jumla ya vituo vya afya vitano katika Halmashauri ya Wilaya ya Chato kwa gharama ya jumla shilingi bilioni 2.64.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025 na mwaka 2025/2026 Serikali imetoa jumla shilingi milioni 489 kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu katika zahanati ya Kasenga na kuwa kituo cha afya chenye uwezo wa kutoa huduma za dharura na za upasuaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2026/2027 Serikali imetenga jumla shilingi milioni 300 kwa ajili ya ukamilishaji wa vituo vya afya katika Halmashauri ya Wilaya ya Chato kikiwemo Kituo cha Afya Iparamasa kilichotengewa jumla shilingi milioni 108.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya kwenye kata za kimkakati kikiwemo Kituo cha Afya Nyamirembe ili kusogeza huduma za dharura na upasuaji kwa mama wajawazito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Cornel Lucas Magembe.

MHE. CORNEL L. MAGEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, ninapenda kujua Mheshimiwa Naibu Waziri ni lini atapanga safari ya kwenda na mimi jimboni ili akajionee hali halisi ya Kata ya Nyamirembe ambayo ni makao makuu ya tarafa ambayo ina wakazi

zaidi ya 23,000 na vijiji vinne ambao wanahitaji kwa haraka utekelezaji wa ujenzi wa kituo hiki cha afya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa vile tayari Serikali imeshapeleka fedha za kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kasenga, lakini Kasenga ni moja ya kata zilizoko kwenye Tarafa ya Kachwamba, ambapo kuna kata nne ambazo mpaka sasa hawana gari la wagonjwa *(ambulance)*. Je, Serikali ina mpango gani katika kuhakikisha kwamba wananchi hao wanapata *ambulance* ambayo itawasaidia katika kuwaharakisha kuwapeleka katika hospitali nyingine?

MWENYEKITI: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili madogo ya nyongeza ya kaka yangu Mheshimiwa Cornel Lucas Magembe, kule tumezoea kumwita mwalimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Magembe kwa kuendelea kuwapambania Wananchi wa Jimbo la Chato Kaskazini. Nianze kwa kujibu swali la kwanza kwamba lini tutafanya ziara katika kata hii yenye wakazi zaidi ya 23,000 ili kujionea hali halisi na kuboresha miundombinu? Nimwambie tu kaka yangu, kwamba Jimbo la Chato Kaskazini liko katika Mkoa wa Geita, na mimi ninatokea Mkoa wa Geita, Jimbo la Busanda. Kwa hiyo, huyu ni jirani yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutatenga muda mimi na yeye tuweze kwenda kuwaona wananchi hao na kuwaambia nini Serikali inaendelea kufanya kwa ajili ya maendeleo yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari tumeshawasiliana na wenzetu Wizara ya Afya, zile *ambulance* ambazo zimeshafika tuweze kuzitoa na tumalizie taratibu za Kiserikali ili tuweze kuwapatia hasa wahitaji, na hasa zile

kata ambazo hazikupata na zile halmashauri ambazo hazikupata waweze kupata *ambulance* hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Festo Sanga, halafu Mheshimiwa Joseph Tama ajiandae.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nimekuwa nikisimama mara kadhaa hapa kuomba ujenzi wa Kituo cha Afya Matamba, kituo ambacho kinahudumia takribani kata tano. Kituo hiki kina hali mbaya sana, hakipo kabisa kwa maana ni cha mwaka 1970. Je, ni lini watajenga kituo kipya cha afya kama ambavyo wameahidi kwenye hotuba zao mara kadhaa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sanga. Kwanza, tulifanya ziara katika Halmashauri ya Wilaya ya Makete. Ninampongeza tu kwamba, wananchi wa kule ni waungwana sana, walitupokea walitupa na wawadi. Japokuwa kuna miinuko na milima ya hatari, lakini tuliweza kufika tukafanya ziara nzuri tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Sanga, kituo hiki cha afya cha kimkakati tayari pamoja na yale majimbo mengine ambayo bado hayajapata, tumeshapeleka andiko Hazina, na tayari Hazina wameshapitisha andiko letu. Kwa hiyo, fedha zikiingia tutakwenda kukamilisha ujenzi wa kituo hiki cha kimkakati.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Joseph Tama. Ninasisitiza Waheshimiwa Wabunge maswali mafupi ya Kibunge na majibu yanayoeleweka mafupi. Mheshimiwa Joseph Tama.

MHE. JOSEPH E. TAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itatoa fedha za ujenzi wa Kituo cha Afya cha Igwisi katika Jimbo la Kaliua?

MWENYEKITI: Asante sana kwa swali fupi la nyongeza, Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Kaliua kwamba pamoja na yeye tayari tumeshawasilisha andiko kuhusu hili ombi la fedha kutoka Hazina. Kwa hiyo, kituo cha afya cha kimkakati katika Jimbo la Kaliua, kwa *confidence* kabisa nimwambie Mheshimiwa Mbunge awaambie wananchi kwamba tunakwenda kukijenga na kianze kutoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jonas Mbunda Mheshimiwa na Ado Shaibu, maswali mafupi.

MHE. JONAS W. MBUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Serikali ilitoa shilingi milioni 250 kwa ajili ya kujenga kituo cha afya kilichopo Kata ya Myangayanga katika Jimbo la Mbinga Mjini, lakini yalijengwa majengo mawili: jengo la *OPD* pamoja na jengo la maabara. Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya cha Myangayanga?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa Serikali ilitoa fedha za kujenga vituo vya afya hivi, kwa kuanzia na shilingi milioni 250 katika maeneo yote nchini. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, na nimwelekeze Mkurugenzi kwa niaba ya Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kuendelea kutenga fedha ili kukamilisha miundombinu katika hospitali zetu hizi hizi ili kuendelea kutoa huduma katika vituo vyote vya afya.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ado Shaibu.

MHE. ADO S. ADO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Jimbo la Tunduru Kaskazini ni moja kati ya majimbo ambayo hayana kituo cha afya kwa kila tarafa, na kwa kuwa Tarafa ya Nampungu ni tarafa pekee ambayo haina kituo cha afya na haijapata bajeti ya kutosha katika ukamilishaji wa ujenzi wa kituo hicho cha afya, je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya Mpungu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba pia Jimbo la Tunduru Kaskazini lipo katika mpango wa kupata kituo cha afya cha kimkakati; na kwenye yale maombi tuliyowasilisha Hazina kimo kituo hiki cha afya cha Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kukamilisha baadhi ya majengo katika vituo vya afya ambavyo bado havijakamilika ili kuendelea kutoa huduma kwa watu wetu wa Jimbo la Tunduru kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Japhael Masanja Lufungija, Mbunge wa Ulyankulu.

Na. 75

Kuwekeza Bajeti ya *TARURA* – Kaliua

MHE. JAPHAEL M. LUFUNGIJA aliuliza: -

Je, lini Serikali itaongeza bajeti ya *TARURA* Wilaya ya kaliua ili kufungua barabara katika vijiji vipya 22 vilivyopo Jimbo la ulyankulu?

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Japhael Masanja Lufungija, Mbunge wa Jimbo la Ulyankulu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini katika Wilaya ya Kaliua unasimamia mtandao wa barabara wenye jumla kilometa 1,370.41. Kati ya hizo, kilometa 9.23 ni barabara za lami, kilometa 329.73 ni barabara za changarawe na kilometa 1,031.45 ni barabara za udongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2020/2021 bajeti ya matengenezo ya barabara katika Wilaya ya Kaliua ilikuwa shilingi milioni 987. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 na kuendelea bajeti hiyo imeongezeka hadi kufikia shilingi bilioni 4.3, sawa na ongezeko la 335.66%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufungua vijiji vipya 22 vilivyopo Jimbo la Ulyankulu kupitia bajeti ya miaka ya fedha 2021/2022 hadi 2024/2025 Serikali ilitekeleza jukumu la kufungua barabara mpya za vijijini. Vijiji vilivyonufaika na utekelezaji huo ni pamoja na Twigu, Nhw'ande katika barabara ya Twigu – Nhw'ande (kilometa sita); Vijiji vya Taba, Imara, Ibapa, Keza katika barabara ya Taba – Imara – Keza (kilometa nane); na Vijiji vya Usonga, Ikonongo katika barabara ya Usonga – King'wangoko (kilometa 18).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka 2026/2027 Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 785 kwa ajili ya kufungua na kuboresha barabara zinazoelekea katika vijiji vipya. Vijiji vitakavyonufaika na mpango huo ni pamoja na Nyasa, Itumbo katika barabara ya Nyasa – Itumbo (kilometa 6.5), vijiji vya Mwahalaja, Upele

na Miti Mitano katika barabara ya Mwaharaja – Mpandamlowoka (kilometa 38.5).

MWENYEKITI: Mheshimiwa Japhael Masanja Lufungija.

MHE. JAPHAEL M. LUFUNGIJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu ya Serikali. Nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, ninaanza kwa kupongeza kwa juhudi kubwa za namna ambavyo Serikali inaendelea kuongeza mtandao na fedha kwenye barabara zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza. Kwa kuwa barabara ya Chemba – Nhw'ande – Twigu inayounganisha Kata ya Sasu ni barabara ndefu sana ukilinganisha na fedha zilizotengwa. Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba sasa zinajengwa karavati ili barabara iweze kupitika kwa wakati wote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Barabara ya King'wangoko – Usonga imepewa fedha shilingi milioni 416; lakini barabara hiyo inapitika kwa kipindi cha kiangazi tu. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba inajenga daraja pale Mto Igombe? Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuambatana na mimi baada ya Bunge kwenda kutembelea barabara hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu ya maswali hayo mawili.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mheshimiwa Japhael Masanja Lufungija amefuatilia sana ujenzi wa barabara katika Jimbo la Ulyankulu. Nimhakikishie kwamba Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imedhamiria kuhakikisha kuwa barabara za vijijini na mijini zinajengwa na zinapitika vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, barabara hizo ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja, zote mbili nimhakikishie Mheshimiwa

Mbunge kwamba tunaendelea kwanza na tathmini ya mahitaji ya fedha kufuatia uharibifu wa mvua nyingi zilizoonyesha pote nchini, ikiwemo katika Jimbo la Ulyankulu; na tutapeleka fedha kwa awamu kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, kumwelekeza Meneja wa *TARURA* Mkoa wa Tabora na Wilaya ya Kaliua kuhakikisha kwamba wanafanya tathmini na kuwasilisha ongezeko la mahitaji ya fedha kwa ajili ya ukarabati wa barabara hizo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, Mheshimiwa Sara Ally ajiandae.

MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itapeleka fedha ya kujenga barabara ya Kisiwani kwa Fufana iliyopo katika Mtaa wa Nzasa A, Kata ya Kilungule?

MWENYEKITI: Mheshimiwa kama utakuwa na majibu, kwa sababu ni mbali huko, nje na swali la msingi. Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Chaurembo kwamba tunafahamu katika Jimbo la Mbagala katika Manispaa ya Temeke kama ilivyo kote nchini, eneo la Chamazi tunahitaji kujenga barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mipango kadhaa. Moja, mpango wa kawaida wa bajeti ya mwaka huu wa fedha 2025/2026 ambapo tunaendelea na utekelezaji. Tumefanya tathmini ya mahitaji ya fedha za dharura kwa ajili ya barabara zilizoharibiwa na mvua, ambapo tunahitaji takribani shilingi bilioni 120. Serikali iko kwenye taratibu za kupata fedha hizo kwa ajili ya kujenga barabara hizo. Nimhakikishie Mheshimiwa Chaurembo kwamba barabara hizo zitapewa kipaumbele.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sara Ally.

MHE. SARA M. ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini *TARURA* itatenga fedha kwa ajili ya kujenga barabara za kiwango cha zege kwenye maeneo ya milimani kama ilivyo Wilaya ya Mvomero ambapo maeneo mengi yako milimani na barabara zinaharibika kipindi cha mvua?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Sara Msafiri, Mbunge wa Mvomero amefuatilia mara kadhaa Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI kuhusu suala la barabara za Mvomero. Ni kweli, wote ni mashuhuda kwamba Mvomero imekuwa na mafuriko mengi sana na ya mara kwa mara, ikiwemo mwaka 2026. Matokeo yake barabara zetu nyingi za udongo zinazolewa na maji na tunakuwa tunaanza upya mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI tuko kwenye hatua za mwisho za kufanya *design* ya barabara madhubuti na imara zaidi ambazo zitajengwa kwenye maeneo yenye mafuriko, milima na mvua nyingi zaidi ili tuhakikishe kwamba barabara hizo zinadumu na zinahudumia wananchi kwa muda mrefu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumhakikishie Mheshimiwa Sara Msafiri na wananchi wa Mvomero kuwa Serikali sikivu iko kwenye hatua za utekelezaji na tutahakikisha kwamba tunaboresha barabara hizo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Alan Thomas Mvano.

MHE. ALAN T. MVANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. Wilaya ya Kakonko ina mtandao wa barabara wa kilometa 391.24 na uwezo wa *TARURA* ni kufanya matengenezo kilometa 120 tu sawa na 30.6%. Je, ni lini Serikali itaongeza bajeti ya *TARURA* katika Wilaya ya Kakonko?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba bajeti ya *TARURA* kila mwaka, kuanzia mwaka wa fedha 2021/2022 imeendelea kuongezeka. Kwa mfano, kutoka shilingi bilioni 210 mwaka 2021/2022 mpaka mwaka huu wa fedha zaidi ya shilingi bilioni 870, ukiondoa fedha za dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tunatambua kwamba uhitaji wa fedha ni mkubwa zaidi, lakini tutaendelea kutenga fedha kwa awamu kujenga barabara za Kakonko ili wananchi waweze kusafiri na kusafirisha bidhaa zao kwa ufanisi mkubwa zaidi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Selemani Kakoso.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mvua zilizonyesha zimeharibu barabara nyingi kwenye eneo la Wilaya ya Tanganyika, ikiwemo Barabara ya kutoka Kapanga – Bujombe – Kalia, je, ni lini Serikali itakwenda kufanya ukarabati kwa barabara nyingi zilizoharibika kwenye eneo la Wilaya ya Tanganyika?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba katika jimbo la Tanganyika, kama ambavyo ipo katika majimbo takribani yote kote nchini, kumekuwa na uharibifu mkubwa wa barabara zetu za *TARURA*. Serikali imeshafanya tathmini ya mahitaji ya fedha kwa ajili ya ukarabati wa barabara hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo linafanyika sasa, kwanza maeneo mengi bado mvua zinaendelea kunyesha kwa hivyo, siyo rahisi kufanya matengenezo ya uhakika katika kipindi hiki cha mvua. Tunasubiri kwanza hali ya hewa ikae vizuri, mvua zipungue, na baada ya hapo, taratibu za fedha zinaendelea kufanyika ili tuendelee kujenga barabara hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Kakoso kwamba suala hilo liko kwenye *pipeline* na tutakwenda kuhakikisha kwamba tunajenga barabara hizo.

MWENYEKITI: Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Dkt. Selemani Saidi Jafo, Mbunge wa Kisarawe.

Na. 76

Ujenzi wa Shule ya Sekondari Mafizi

MHE. DKT. SELEMANI S. JAFO aliuliza: -

Je, lini Serikali itatenga fedha za ujenzi wa shule ya sekondari eneo la Mafizi ili kupunguza umbali kwa wanafunzi wa Mafizi na Nyani?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Selemani Saidi Jafo, Mbunge wa Jimbo la Kisarawe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kujenga shule za sekondari katika kata ili kuwapunguzia umbali wanafunzi kote nchini, ikiwemo katika Wilaya ya Kisarawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 hadi 2023/2024, Serikali imejenga shule mpya tano za sekondari, ikiwemo shule ya Dkt. Selemani Jafo, Kitanga Kisarawe, Muungano Boga, Visiga na Vitende katika Halmashauri ya Kisarawe kwa gharama ya shilingi bilioni 1.83.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi wanaotoka Mafizi na Nyani wanasoma katika Shule ya Sekondari Gwata Kisarawe, Kata ya Mafizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwaondolea changamoto ya umbali kwa wanafunzi, Serikali katika mwaka wa fedha 2025/2026 imepeleka shilingi milioni 68.81 kwa ajili ya ukamilishaji wa bweni ambapo kwa sasa liko hatua ya umaliziaji.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Selemani Saidi Jafo.

MHE. DKT. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumebakisha mwaka mmoja na miezi minane kuingia katika utekelezaji wa sera yetu mpya ya elimu ambayo itahitaji vijana wa Darasa la Sita na Darasa la Saba itakapofika Januari, 2028 wote waende sekondari. Pale sasa ninataka kujua, je, nini mpango wa Serikali wa haraka kupeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa shule pale Mafizi kwa lengo la kuhakikisha vijana wa Mafizi, Nyani na kutoka shule mpya ya Visimavitatu waweze kupata elimu katika eneo lile?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nini mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba shule takribani 3,000 zinajengwa upya kwa lengo la ku-*accommodate* hawa vijana wa Darasa la Sita na Darasa la Saba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini mpango wa Serikali uliopo sasa kuhakikisha kwamba tunafanya *resource mobilization* kupata fedha kati ya shilingi trilioni mbili mpaka trilioni tatu kwa ajili ya ujenzi wa shule hizo nchi nzima Tanzania kusaidia vijana wa Kitanzania? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Selemani Saidi Jafo, Mbunge wa Jimbo la Kisarawe, Mbunge madhubuti sana na kwa kweli, anawatendea haki wananchi wa Jimbo la Kisarawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Jafo ni nguli sana wa masuala ya TAMISEMI, pia ninafahamu kwamba kwa kweli kupitia Sera ya Elimu ya Mwaka 2014, Toleo la 2023, Darasa la Sita na Darasa la Saba ya mwakani, 2027, watajiunga kwa pamoja Kidato cha Kwanza Januari, 2028.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya madarasa yatakayohitajika ni 23,226, maabara 9,366, na matundu ya vyoo 46,632. Serikali imeshafanya tathmini, tutahitaji kuwaingiza Kidato cha Kwanza wanafunzi 3,021,177. Kwa hiyo, Serikali hii kwanza tunatambua kwamba katika eneo la Mafizi na Nyani tunafanya tathmini ili tuongeze shule nyingine katika maeneo mbalimbali na kusogeza huduma za elimu karibu zaidi na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika tathmini inayoendelea ya kutambua maeneo ya kujenga shule, tutatoa kipaumbele eneo la Mafizi na Nyani pia ili kama linakidhi vigezo hivo, shule iweze kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba Serikali hii ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imejipanga imara na madhubuti kuhakikisha wanafunzi wote 3,000,000 Januari, 2028 watakwenda madarasani bila changamoto yoyote, na tayari tunaendelea ku-*mobilize resources,* na kwa hakika wanafunzi wote watakwenda kwa mujibu wa Sera ya Elimu iliyopo sasa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Boniphace Getere, na Mheshimiwa Nyamizi Mhoja ajiandae.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Wanakijiji wa Kata ya Salama, kijiji cha Kurusanga, wametoa eneo ekari 50, wamefyatua matofali ya *block* yaliyozidi ya Serikali 3,000, wamechanga fedha, na sasa wanazo shilingi milioni 21 benki, wanataka kujenga sekondari. Ni lini Serikali itawaunga mkono kujenga Sekondari ya Kurusanga?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya sehemu muhimu ambayo Serikali inatoa kipaumbele ni kuhamasisha wananchi kuchangia nguvu katika ujenzi wa miundombinu mbalimbali ya huduma za kijamii zikiwemo shule. Kwa hiyo, kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Getere na wananchi katika kijiji hicho kwa kutoa eneo la ekari 50, kufyatua tofali na kuendelea kutoa michango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawahakikishia kwamba katika mpango wa utekelezaji wa sera mpya ya elimu, tayari timu zetu zinaendelea kufanya tathmini na kutambua maeneo ambayo yana sifa za kuongeza shule nyingine ili tuweze kujenga shule hizo za sekondari na wanafunzi wetu Januari, 2028 waingie madarasani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutalifikia eneo hilo na tutaunga mkono juhudi za wananchi kuhakikisha shule hiyo inajengwa ikiwa itakidhi vigezo kwa mujibu wa taratibu za elimu.

MWENYEKITI: Nilimtaja Mheshimiwa Mhoja! Niliyemtaja ninaona jina lake limeshaondoka hapa. Kama hayupo tunaendelea na Mheshimiwa Tinnar Chenge.

MHE. TINNAR A. CHENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Shule ya Sekondari Busangwa iliyopo Kata ya Sakasaka katika Jimbo la Kisesa ina wanafunzi wa kike takribani 250, lakini hakuna mwalimu wa kike hata mmoja. Je, ni lini Serikali itapeleka walimu wa kike? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kama umemwelewa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaomba nipokee hoja ya Mheshimiwa mama yangu, Mheshimiwa Mama Chenge, lakini nitoe tu ufafanuzi ili kuweka rekodi sawa kwamba tunafahamu umuhimu wa walimu wa kike katika

shule zetu zote za wanafunzi wa kiume na wa kike. Tunafahamu pia kuna mahitaji maalum ambayo mara nyingine ni vizuri mwalimu wa kike akiwa katika shule hizo. Kwa hiyo, suala hilo tumelichukua na tutakwenda kulifanyia kazi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nyamizi Mhoja.

MHE. NYAMIZI S. MHOJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Shule ya Msingi ya Sanze Wilaya ya Kisarawe iliyopo Kisarawe, ni jumuishi na imeanza kupokea watoto wenye ulemavu wa bweni kabisa pale. Hata hivyo, shule ile haina walimu ikiwemo hata mkalimani wa lugha ya alama. Sasa, ni lini Serikali itafikiria kuboresha elimu maalum ili hawa wanafunzi waweze kupata haki yao? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba zipo shule maalum ambazo pamoja na wanafunzi wengine, ina wanafunzi wale wenye mahitaji maalum na hususan wenye ulemavu. Serikali imeendelea kila mwaka kuajiri walimu kadiri wanavyotoka katika vyuo vyetu kwa ajili ya kuwapeleka kwenye shule ambazo zina wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba safari ni hatua, tunakwenda kwa hatua na tunaendelea kuboresha pia mafunzo kwenye vyuo vyetu ili walimu wenye mafunzo maalum ya elimu maalum waweze kufika kwenye shule zetu. Kwa hiyo, tutatoa kipaumbele pia katika shule ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Mgore Miraji Kigera, Mbunge wa Musoma Vijijini, aulize swali lake.

Na. 77

Mkakati Juu ya Kiwanda cha *MUTEX*

MHE. MGORE M. KIGERA aliuliza: -

Je, upi mkakati wa Serikali wa kuhakikisha mwekezaji wa Kiwanda cha *MUTEX* anaanza uzalishaji kwa haraka?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgore Miraji Kigera, Mbunge kutoka Musoma Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha *Musoma Textile Mills Tanzania Limited (MUTEX)* kilianzishwa kwa lengo la kuongeza thamani ya pamba iliyozalishwa nchini, kutoa ajira na kuchangia maendeleo ya viwanda katika Ukanda wa Ziwa Victoria na Tanzania kwa ujumla. Hata hivyo, hadi sasa kiwanda hiki hakifanyi kazi, na hivyo kinasimamiwa na Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika juhudi za kufufua kiwanda hiki, Serikali ilipokea maombi ya mwekezaji mwenye nia ya kuwekeza kwenye eneo hili. Hivyo basi, Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mara, walianza mara moja mchakato wa kufanya majadiliano na mwekezaji huyo ambapo pande zote mbili zilifikia makubaliano kuhusu masharti mapya ya uwekezaji. Kufuatia makubaliano hayo, rasimu ya mkataba iliandaliwa na kuwasilishwa kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya mapitio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa mchakato wa kufanyia kazi maboresho yaliyopendekezwa kwenye mkataba unaendelea na mara tu utakapokamilika, mkataba utasainiwa rasmi kati ya Serikali na mwekezaji. Hatua hiyo itafuatiwa na kukabidhiwa kwa kiwanda

pamoja na nyaraka zote za umiliki kwa mwekezaji ili aweze kuanza utekelezaji wa uwekezaji na kurejesha uzalishaji wa kiwanda hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mgore Miraji Kigera. Walio karibu wazime *mic* zao kwanza.

MHE. MGORE M. KIGERA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Je, Serikali haioni wakati sahihi umefika kuhakikisha wanakamilisha makubaliano na kusaini mkataba na mwekezaji huyo ili kuweza kutekeleza ahadi yake kwa wananchi wa Jimbo la Musoma Mjini, kukuza ajira na uchumi wa Musoma Mjini kupitia kiwanda hiki cha *MUTEX*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Ni lini Serikali itawalipa waliokuwa wafanyakazi wa kiwanda hicho cha *MUTEX* kwani tangu mwaka 1994, wafanyakazi hao wamekuwa wakiidai Serikali fedha zao? Ninashukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninachukua nafasi hii kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Mgore Miraji Kigera, Mbunge wa Jimbo la Musoma Mjini, kwa kuendelea kufuatilia kwa ukaribu sana kuhusu hiki Kiwanda cha *MUTEX* ambacho kimsingi, kama kitafufuliwa, kitakuwa na tija sana kwa wananchi wa Musoma Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme, Mheshimiwa Mbunge amekuwa akitusumbua sana na amefuatilia kwa karibu sana kuhusu hiki kiwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo, ninaomba kujibu maswali mawili yaliyoulizwa na Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia na dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba tunavutia wawekezaji, na sisi kama Serikali tumejipanga, maeneo yote yale ambayo kimsingi yapo *idle*, hayafanyi kazi, tunatafuta wawekezaji ili tuweze kuhakikisha tunawekeza. Hii ni sehemu ya utekelezaji wa Dira yetu ya 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia hilo, na sisi tumeona kuna haja sasa ya ku-*fast track process* ya kuhakikisha kwamba huyu mwekezaji anasaini mkataba kwa haraka. Pia tutamsimamia, tutampa *performance contract,* ili ndani ya muda mfupi tuone uwekezaji unaanza katika Jimbo la Musoma Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vigezo vikubwa ambavyo tunaviweka kwa sasa hivi, kwanza tunataka mwekezaji atakaposaini mkataba, atoe *commitment,* ni lini ataanza kuwekeza katika eneo la Musoma Mjini? Pili, ni kiasi gani cha ajira atakuja kuzalisha? Tatu, tunataka achangie katika mnyororo wa thamani, hususan katika Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Ni kweli kulikuwa kuna wafanyakazi ambao walikuwa wanafanya kazi katika kiwanda cha *MUTEX*, takribani 935. Kati ya hao, wafanyakazi 856 walishalipwa mafao yao na wafanyakazi 79 walikuwa bado hawajalipwa mafao yao. Hawa 79 hawakujitokeza wakati wa uhakiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua nafasi hii sasa kuwataka wale wote 79 ambao hawakujitokeza, wakati tunafanya uhakiki, wapeleke nyaraka zao kwenye ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Mara, wahakikiwe na baada ya kuhakikiwa Serikali itakuwa tayari kuwalipa. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Christina Mndeme, Mheshimiwa Paschal Chinyele ajiandae.

MHE. CHRISTINA S. MNDEME: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa, Serikali imekuwa ikifanya kazi nzuri ya kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji nchini, na kwa kuwa kiwanda cha nyuzi cha Tabora, *(TABOTEX)* kimesimama miaka mingi sana bila kufanya kazi, je,

Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba kiwanda hiki cha nyuzi Tabora kinafufuliwa na kuanza kufanya kazi ili kiweze kutoa ajira kwa Wanatabora na Watanzania kwa ujumla na kukuza uchumi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninachukua nafasi hii kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kutoka Mkoa wa Tabora. Ninajua michango yake mingi nimekuwa nikiifuatilia, amekuwa akichangia sana kwenye suala la uwekezaji, na jinsi ya kuwezesha kinamama katika suala la uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hiki kiwanda cha nyuzi cha Tabora ambacho kimesimama kama tutakifufua kitakuwa na tija sana kwa uchumi wa Taifa. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi kama Serikali tumeweka mkakati wa kutathmini viwanda vyote ambavyo vimesimama na baada ya tathmini hiyo tutaandaa mpango mkakati wa kuvifufua ikiwa ni pamoja na kuvutia wawekezaji. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Paschal Chinyele.

MHE. PASCHAL I. CHINYELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, ni lini Serikali itatekeleza mpango wa ujenzi wa viwanda katika kongani za viwanda katika kata za Nala pamoja na Mpunguzi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua nafasi hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Chinyele, Mbunge wa Dodoma Mjini, kwa kuwatetea wananchi wa Dodoma, hususan wananchi wa Nala na wananchi wa Mpunguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mpango wetu wa miaka minne, tume-*commit* kuanzisha miradi saba ya kielelezo *(National*

Flagship Programs). Katika ile miradi saba ya kielelezo, tunakuja kuanzisha kongani ya viwanda eneo la Nala ambayo kimsingi tunaweka pale viwanda vya kuchenjua dhahabu kwenye madini ambayo ni *rare* na *critical*, kwa mfano *lithium*, *cobalt*, *nickel* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa eneo la Mpunguzi tumelitenga kama eneo la mkakati kwa sababu Mpunguzi wanazalisha sana zabibu. Kwa hiyo, ninamwondoa mashaka Mheshimiwa Chinyele, Mbunge wa Dodoma Mjini, kwamba hili lipo kwenye mpango wetu wa miaka mitano. Pia, tumeliingiza na kwenye mpango wa mwaka mmoja, tumelitengea bajeti. Ninashukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunakwenda Wizara ya Nishati kwa dharura, baadaye tutarudi Wizara ya Mambo ya Ndani. Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mbunge wa Bahi, aulize swali lake. Kwa niaba yake Mheshimiwa Ester Bulaya.

Na. 87

Kusafisha Mafuta Ghafi Kutoka Bomba la Mafuta Toka Uganda – *EACOP*

MHE. ESTER A. BULAYA K.n.y. MHE. KENNETH E. NOLLO aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza kusafisha mafuta ghafi yanayotoka Uganda kupitia Bomba la Mafuta *EACOP*?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali Na. 87.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, ninaomba kujibu swali namba 87 la Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mbunge wa Bahi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushiriki wa Tanzania kwenye mradi wa bomba la *EACOP* upo kwenye biashara ya kusafirisha mafuta ghafi tu, yaani *transit nation* kutoka Kabaale – Hoima hadi Chongoleani – Tanga na baadaye kupelekwa kwenye masoko ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikataba ya mauzo ya mafuta hayo imeshaingiwa tayari kati ya wabia wa mkondo wa juu nchini Uganda, yaani *up streamers* ambao ni Serikali ya Uganda na makampuni ya Kimataifa ya *Total Energies* kutoka Ufaransa na *CNOOC* kutoka China kwa kuzingatia vigezo vya usanifu wa kitaalamu na uwezo wa uzalishaji wa visima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba ifahamike kwamba kwenye biashara hii tayari mikataba ya mauzo ya mafuta haya imeshaingiwa kati ya wabia wa mkondo wa juu na wanunuzi wa masoko ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ester Bulaya.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Mosi, je, katika mikataba iliyoingia Wizara ya Nishati, mmezingatia vipi maslahi ya nchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kupitia mradi huo, Tanzania tutanufaika nini? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti ninakushukuru. Kwanza, ninampongeza dada yangu, Mheshimiwa Ester Bulaya kwa kufuatilia kwa karibu juu ya faida za Mradi huu wa Bomba la *EACOP* kwetu sisi Tanzania. Yako manufaa mengi ambayo Watanzania wameshayapata mpaka sasa hivi. Hivi tunavyozungumza, kipindi cha ujenzi wa bomba hili la mafuta, Watanzania zaidi ya 10,000 wamenufaika kwa ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya Mkoa wa Tanga ambako kimsingi ndiyo bomba hili linapoishia kwa ajili ya kutoa mafuta kupeleka nje, wananchi wale wamejengewa miradi ya maji, wamejengewa miradi ya barabara, wamechimbiwa visima na kama haitoshi, wamefanyiwa mafunzo mbalimbali kwa ajili ya upandaji wa miti na utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiachana na hilo, Tanzania itanufaika na uwepo wa bomba hili kwa sababu kuna asilimia ambayo nchi yetu itanufaika kama sehemu ya mradi wa bomba la mafuta. Ukiachana na hilo, sisi Watanzania tutapata faida ya kuuziwa sehemu ya mafuta hayo ghafi ambayo yakiwa yameshasafishwa tutayapata kwa ajili ya matumizi ya ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako manufaa makubwa ambayo tunamshukuru Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kukubaliana na Mheshimiwa Rais wa Uganda, waliamua kufanya mradi huu wa kimapinduzi ambao unaenda kutatua changamoto ya mafuta na ya kiuchumi katika nchi yetu.

MWENYEKITI: Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea sasa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Ali Vuai Khamisi, sasa aulize swali lake.

Na. 78

Ujenzi wa Kituo cha Polisi Matemwe – Mkwajuni

MHE. ALI VUAI KHAMIS aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga kituo cha Polisi katika Kijiji cha Matemwe Jimbo la Mkwajuni Unguja kutokana na uwekezaji mkubwa uliopo katika eneo hilo?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kumjibu swali Mheshimiwa Ali Vuai Khamis, Mbunge wa Mkwajuni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la Matemwe Jimbo la Mkwajuni, hakuna sehemu iliyotengwa rasmi kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha Polisi. Napenda kutumia fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu, kumshauri Mheshimiwa Mbunge pamoja na Kamisheni ya Ardhi Zanzibar kupitia Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi ili kutenga eneo kwa ajili Kituo cha Polisi Matemwe, ili Serikali iweze kutenga fedha kutoka kwenye bajeti yake kwa ajili ya kujenga kituo hicho cha Polisi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ali Vuai Khamis.

MHE. ALI VUAI KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninapokea ushauri, pia nina maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, Serikali ina mpango gani wa kuwapeleka askari wa doria katika eneo hilo ambalo liko mbali na kituo cha Polisi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, je, yuko tayari kutembelea Kijiji hicho kwenda kuona matatizo halisi ya umuhimu wa ujenzi wa kituo cha Polisi?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Khamis kwa kufuatilia kwa karibu hali ya ulinzi na usalama katika Ukanda wa Mkwajuni hasa katika eneo la Matemwe, eneo ambalo ni ukanda wa utalii na lina ongezeko kubwa la idadi ya watu kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ninaomba kujibu hoja zake mbili. La kwanza, tuna mpango gani wa doria, kwa ukanda wote wa kuanzia Matemwe, Pwani Mchangani, Kiwengwa hadi Nungwi. Kwa sasa Jeshi letu la Polisi linaendelea na doria kwa sababu eneo lote hilo ni la kimkakati kwa ajili ya uwekezaji wa utalii, na kila siku Jeshi la Polisi kupitia Kituo Kikuu kilichopo Mkokotoni wanaendelea kufanya doria

na Kituo Kidogo kilichopo Kiwengwa katika ukanda wote wa Pwani ambao amezungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa pili wa ombi lake la kutembelea hilo na kuona umuhimu wa kujenga kituo katika eneo hilo, napenda kukubaliana naye kimsingi kwamba eneo la ukanda wa Matemwe ni eneo la utalii, na kwa sababu ni eneo la utalii, kasi kubwa ya uwekezaji pamoja na ujio wa watalii na wageni mbalimbali kutembelea maeneo hayo, kunaakisi hoja aliyoileta ya kuweza kujengwa kituo katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ninaomba nimjibu tu Mheshimiwa kwamba niko tayari kutembelea eneo hilo. Pili, tunaona umuhimu wa kujenga kituo cha Polisi katika eneo hilo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwinyi Ramadhan.

MHE. MWINYI JAMAL RAMADHAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa heshima hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Ninaomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri, je, ni sababu zipi zinafanya kujengwa kwa kituo cha Polisi? Ni wingi wa watu, idadi ya uhalifu, kilometa, nyumba au ni nini?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nimemwelewa vizuri alichotaka hasa ni elimu ya kufahamu kwamba tunapokwenda kufanya maamuzi ya kujenga vituo vya Polisi, ni vigezo gani vinavyotusababisha kufanya maamuzi hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hivyo ndivyo, nataka kumwambia tu Mheshimiwa Mwinyi Jamal Ramadhan kwamba kwenye vyombo vya ulinzi na usalama kuna kitu kinaitwa *security audit* kwa maana ya ukaguzi wa kiusalama. Eneo ambalo linaonekana lina matishio zaidi ya kiusalama, ndilo eneo ambalo tunalipendekeza kuweza kuliwekea miundombinu ya kiulinzi vikiwemo vituo vya Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wingi wa watu au idadi ya watu ni moja ya sababu, kasi ya ukuaji wa uchumi inaweza ikawa moja ya sababu, uhamiaji unaweza ukawa pia ni sehemu ya sababu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Asha Salum.

MHE. ASHA S. MOTTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza. Je, Serikali haioni haja ya kujenga nyumba za ghorofa kwa wafanyakazi wa Kituo cha Polisi Fuoni pamoja na kununua gari la doria?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Serikali inaona umuhimu wa kujenga nyumba za Polisi nchi nzima. Katika eneo la Fuoni hivi sasa zipo nyumba za Polisi, na baadhi yake ni za ghorofa, isipokuwa tu ninajua Mheshimiwa Asha amekuwa karibu na wananchi wake katika eneo la Fuoni na anafuatilia mwenendo wa hali ya usalama kwenye eneo lile na hasa kufuatilia ukamilishaji wa kituo cha Polisi pamoja na ujenzi wa nyumba za makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati, eneo hilo tumeshatembelea mimi na Mheshimiwa Asha, tumeshaliona na kubainisha baadhi ya maeneo yenye uhitaji wa kujengwa hizo nyumba na tayari tumetoa maelekezo kwa wenzetu wa Jeshi la Polisi kuweka mpango wa kujenga nyumba hizo kama ambavyo Mheshimiwa amependekeza.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Baraka Mwamengo.

MHE. BARAKA A. U. MWAMENGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona na kunipa nafasi hii. Ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi cha Kasumulu kilichopo *border* ya Kasumulu ndani ya Jimbo la Kyela kwa kuwa kiliathirika na vurugu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, tumehamia Kyela sasa. Majibu kama unayo.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge wa Kyela na nimpongeza vilevile kwa kuona umuhimu, na ninadhani kwa sababu ya ufafanuzi wangu wa hoja ya msingi ya kwa nini tunajenga vituo vya Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi kwenye swali la msingi tulilojibu la Jeshi la Polisi kwa mara ya kwanza Bungeni, tulikuja na mpango wa dharura wa maeneo ambayo yana uhitaji wa kujenga vituo vya Polisi na tuliainisha wastani wa maeneo 698 nchi nzima. Hayo ndiyo maeneo ya dharura kujenga vituo vya Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo hayo 698 ambazo ni karibu kata zaidi ya 600 zilikuwa hazina kabisa vituo vya Polisi na kata 77 zilikuwa zimeanza ujenzi kwa maboma, lakini hawajakamilisha. Nataka kumwambia tu Mheshimiwa kwamba tunaona umuhimu wa kujenga kituo cha Polisi eneo hilo, lakini lini? Mpango ule tumeugawa katika awamu tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya kwanza tutakuwa na vituo 196, awamu ya pili tutakuwa na vituo 212 na awamu ya tatu tutakuwa na vituo 211. Kwa hiyo, kukamilika kwa Mpango huu, basi na eneo lake litakuwa tayari limeingia kwenye ujenzi.

MWENYEKITI: Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Emmanuel John Khambay, Mbunge wa Babati Mjini.

Na. 79

Maboresho ya Makazi ya Askari Magereza na Kununua Magari Mapya Gereza la Babati Mjini

MHE. EMMANUEL J. KHAMBAY aliuliza: -

Je, lini Serikali itafanya maboresho ya makazi ya askari pamoja na kununua magari mapya Gereza la Babati Mjini?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Emmanuel John Khambay, Mbunge wa Babati Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Gereza la Babati ni miongoni mwa Magereza yaliyojengwa miaka mingi tangu mwaka 1974 hali iliyosababisha uchakavu wa miundombinu ya gereza pamoja na majengo ya makazi ya Askari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Jeshi la Magereza limeanza kutekeleza mpango mkakati wa muda mfupi na muda mrefu ambapo kwa Gereza Babati ziko nyumba tatu zinaendelea na ujenzi kwa kutumia mapato ya vyanzo vya ndani vya ubunifu. Aidha, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali imetenga shilingi 5,380,000,000/= kwa ajili ya ununuzi wa magari 31 kwa shughuli za Utawala na kusafirisha Mahabusu. Pindi magari hayo yatakapofika, Gereza la Babati litapatiwa gari moja mpya kwa matumizi ya kituo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Emmanuel John Khambay.

MHE. EMMANUEL J. KHAMBAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali, nina swali moja la nyongeza. Kama ambavyo amekiri mwenyewe kwamba Gereza la Babati ni miongoni mwa magereza yaliyojengwa kwa miaka ya zamani, je, ni nini mpango wa Serikali wa kujenga gereza lingine jipya ambalo pia litakuwa ni gereza la kisasa linaloendana na wakati?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Emmanuel kwa swali lake la nyongeza ambalo ni la muhimu sana. Kwanza tukiri ni kweli tuna uhitaji mkubwa wa magereza nchini, kwani katika hali ya sasa nchi nzima tuna idadi ya magereza 129. Kati ya magereza hayo, magereza 10 yana hadhi ya magereza ya kanda, magereza 76 yana

hadhi ya magereza ya mikoa na wilaya na magereza 43 ni magereza ya wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali hiyo, tuna upungufu wa takribani wilaya 50 ambazo hazina magereza, lakini kazi inayoendelea sasa ya ujenzi wa magereza katika maeneo mbalimbali ambayo kwa kweli kwa baadhi ya maeneo imepiga hatua nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Wilaya ya Karatu gereza limekamilika, Wilaya ya Kilosa limeanza ujenzi, Wilaya ya Gairo linaendelea, Wilaya ya Kingurungundwa kule Mchinga nalo linaendelea. Ninaamini kwamba na maeneo mengine pia tutaendelea na hatua kama ambavyo nimetaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Serikali kwenye ujenzi wa magereza haya ni kuendelea kuweka fedha kwenye bajeti, kwani tayari tumeshafanya tathmini ya uhitaji wa magereza hayo kwamba kila gereza moja linahitaji wastani wa shilingi bilioni nane kulijenga. Hivyo, kwa magereza 50 tunahitaji wastani wa shilingi bilioni 40 ili tuweze kujenga magereza hayo. Sambamba na hilo, tunafahamu pia ipo changamoto kubwa ya makazi ya Askari Magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jambo hilo, pia Serikali imeandaa mpango wa muda mrefu ambao utajenga wastani wa nyumba 6,368 za magereza zitakazoweza kukaliwa na wastani wa kata 21,187. Bajeti ya fedha hizo zinahitajika zaidi ya shilingi trilioni 2.88 kwa ajili ya kukamilisha mradi huo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, ninakushukuru sana kwa majibu hayo ya jumla. Ninafikiri yametosheleza kuhusiana na suala la magereza nchi nzima.

Kwa hiyo, tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, Mbunge wa Magu aulize swali lake.

Na. 80

Ujenzi wa Mradi wa Maji Lugeye Kigangama

MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA aliuliza: -

Je, lini Serikali itatoa fedha za kumalizia Mradi wa Maji Lugeye Kigangama uliosimama kwa miaka miwili sasa?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Boniventura Kiswaga, Mbunge wa Jimbo la Magu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele cha Serikali ni kuhakikisha miradi yote inayoendelea na utekelezaji, inakamilika na kuanza kutoa huduma iliyokusudiwa kwa wananchi ukiwemo mradi wa Lugeye – Kigangama uliopo Wilaya ya Magu Mkoani Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huo unagharimu zaidi ya shilingi bilioni saba na umefikia wastani wa 65% za utekelezaji ambapo unahusisha ujenzi wa dakio *(intake)* yenye uwezo wa kuzalisha maji lita milioni 3.7 kwa siku kutoka chanzo cha ziwa Victoria. Ujenzi wa mtambo wa kutibu maji *(treatment plant)*, ujenzi wa tanki lenye ujazo wa lita 1,000,000, ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 52 sanjari na ujenzi wa vituo 10 vya kuchotea maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kupeleka fedha za utekelezaji wa mradi huo kadiri zinavyopatikana ili kuhakikisha unakamilika ndani ya mwaka wa fedha 2026/2027 na kuanza kutoa huduma iliyokusudiwa kwa zaidi ya wananchi 47,076 waishio katika vijiji saba vya Kitongosima, Lugeye, Kigangama, Bundilya, Nyanguge, Bugumangala na Muda.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga.

MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa mradi huu umechukua muda mrefu na mkandarasi ameshafanya kazi zaidi ya shilingi bilioni 4.5 na amelipwa shilingi bilioni 1.5, je, nini mkakati wa Serikali wa kupeleka fedha ili huyo mkandarasi arudi kazini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa kuna miradi ambayo imefikia 98%, Mheshimiwa Naibu Waziri anaifahamu, Mradi wa Iseni, Nyang'hanga, Mradi wa Mwarina – Mwamabanza – Salong'we, lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kumalizia hizo asilimia ambazo zimebaki ili wananchi waweze kupata huduma?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Boniventura Kiswaga, Mbunge mahiri kutoka Mkoa wa Magu katika Jimbo la Magu, kwa kazi nzuri ambayo anaendelea kuifanya ya kuwatetea hasa katika kumtua mama ndoo kichwani ambayo ni falsafa ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikiri kwamba Mheshimiwa Mbunge ni mfuatiliaji mzuri sana na kwa mantiki hiyo, hivi sasa ninayo maelekezo ya Mheshimiwa Waziri wa Maji Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso kuhakikisha mradi huu na mkandarasi huyu ndani ya malipo ya mwezi huu tuhakikishe kwamba analipwa. Ndiyo mkakati wa kuhakikisha kwamba tutaendelea kumlipa mpaka pale ambapo fedha zote zitakuwa zimeshalipwa ili mradi uweze kukamilika. Hivi sasa mradi uko 65% na tunaamini kwamba akishalipwa atarudi *site*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, mpaka sasa mkandarasi tumeshamwita hapa Dodoma, leo tutakuwa na mazungumzo naye ili tuhakikishe tutakapolipa hizi fedha, arudi *site* moja kwa moja ili tukaone sasa matunda ya kazi kubwa inayofanywa na Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo miradi mingine ndani ya Jimbo la Magu ambapo ni matokeo ya kazi nzuri sana ya Mheshimiwa Mbunge. Tunayo miradi takribani sita, ukiwemo wa Lugeye. Miradi hii kwa jumla yake kuna uwekezaji mkubwa sana wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya shilingi 18,000,000,000 zimewekezwa pale, na pia miradi ya Nyang'hanga, Iseni, Sagani, Misungwi, Mahaha, Nsola, Bubinza yote hiyo iko katika hatua mbalimbali. Mmoja upo 90%, mwingine 98%, mwingine uko 65%, mwingine uko 50%. Tunaamini kwamba tukiendelea kupeleka fedha, miradi hii itatoa matokeo kwa haraka sana. Nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Adonis Alfred, Mheshimiwa Mecktridis Mdaku, ajiandae.

MHE. ADONIS A. BITEGEKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kuniona na kunipa nafasi. Jimbo la Muleba Kaskazini, Wilaya ya Muleba ina miradi miwili ya maji, Mradi wa Makongora na Mradi wa Iroba ambayo kwa muda mrefu inasubiri Serikali kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji. Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo ili kusaidia wananchi takribani 9,000 kupata huduma ya maji salama?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera yetu ya Maji, kwanza kabisa ni kuhakikisha kwamba maji yawe safi, yawe salama na yawe ya kutosheleza. Ujenzi wa chujio ni sehemu ya sera kwa sababu ni lazima chujio hilo liweze kutumika katika kuhakikisha kwamba maji yanakuwa safi, na pia yanatibiwa vizuri ili yawafikie wananchi yakiwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima chujio hilo liweze kutumika katika kuhakikisha kwamba maji yanakuwa safi na yanatibiwa vizuri ili yawafikie wananchi yakiwa salama. Nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge na kwa kazi kubwa. Ninafahamu ana miezi michache tangu ameingia, lakini amekuwa mfuatiliaji mzuri sana wa miradi hii ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wizara ya Maji tunaahidi kuendelea kumpa ushirikiano Mheshimiwa Mbunge ili kuhakikisha kwamba fedha zinapelekwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba chujio hili linajengwa ili likamilike na kutoa huduma iliyokusudiwa kwa wananchi. Ninakushukuru sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mecktridis, ajiandae Mheshimiwa Moses Bujaga. Walio karibu wazime *mic* zao. Jaribu kuzima.

MHE. MECKTRIDIS F. MDAKU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Jimbo la Malinyi lina Miradi ya Maji katika Kijiji cha Misegese – Ihowanja na Mtimbira na miradi hii imekaa muda mrefu zaidi ya miaka mitatu sasa bila kukamilika. Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa fedha ili kukamilisha miradi hii? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, kama una majibu ya Malinyi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge wa Malinyi, ni Mbunge mahiri, na pia ni Mjumbe katika Kamati yetu ya Maji na Mazingira, tunaendelea kutambua mchango wake mkubwa sana katika kuishauri Serikali na kuisimamia. Katika kuwatetea wananchi wake, sisi tutaendelea kumpa ushirikiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo madai ya wakandarasi ndani ya Jimbo lake, na tayari yameshaletwa na yameshafika kwenye Ofisi ya Katibu Mkuu, wanayafanyia kazi. Tunaamini kabisa kwamba ndani ya kipindi cha miezi miwili mitatu hii, tutapeleka fedha ili wakandarasi hawa walipwe ili miradi hii ambayo imekaa kwa muda mrefu iweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhamira ya Serikali, siyo hiyo miradi pekee, miradi yote inayoendelea kutekelezwa nchini tunayo maelekezo mahsusi ya Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba tunakamilisha kwanza hii miradi ambayo imeishaanza badala ya kuanza miradi mipya ili kuhakikisha kwamba tunaanza kupata matokeo kabla ya kuanzisha miradi mingine mipya. Ninakushukuru sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Moses Bujaga.

MHE. MOSES C. BUJAGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria kuja Mji Mdogo wa Malya umesimama. Swali langu ni kutaka kujua, ni lini mkandarasi atalipwa fedha ili arudi kazini na kukamilisha mradi huu? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Moses Charles Bujaga, Mbunge wa Sumve, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa mradi ule unaopita Hungumalwa – Malya kwenda kule Sumve, na pia mradi huu unaenda mpaka kwa Mheshimiwa Mashimba Ndaki. Mheshimiwa Mbunge tulishakaa pamoja na mkandarasi kwa pamoja tukakubaliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninaomba sasa nimhakikishie kwamba ule mpango wa kuhakikisha kwamba analipwa, tumeweka kipaumbele katika kipindi hiki cha miezi miwili ili mkandarasi aweze kulipwa na arudi *site*, kwa sababu tunajua kuna matanki ambayo tayari ameshayajenga, lakini kuna kilometa kadhaa za kulaza mabomba ili aweze kumalizia na kuhakikisha kwamba wananchi wa maeneo hayo wanaweza kunufaika na huduma ya majisafi na salama. Ninakushukuru sana.

MWENYEKITI: Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Omary Marcus Msigwa, Mbunge wa Madaba. Mheshimiwa Omary Marcus Msigwa.

Na. 81

Hitaji la Maji Safi na Salama Madaba

MHE. OMARY M. MSIGWA aliuliza: -

Je, lini Serikali italeta fedha katika Jimbo la Madaba ili kutatua changamoto ya maji katika Vijiji vya Gumbiro, Ngadinda na Lilondo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Omary Marcus Msigwa, Mbunge wa Jimbo la Madaba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi ya maji katika vijiji vya Gumbiro, Ngadinda na Lilondo vilivyopo Halmashauri ya Madaba Wilaya ya Songea Mkoani Ruvuma. Miradi hiyo kwa pamoja inagharimu jumla ya shilingi bilioni 2.451 ambapo inahusisha ujenzi wa vyanzo vya maji vitatu; ujenzi wa matanki matatu yenye jumla ya ujazo wa lita 325,000, ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 62.9, sanjari na ujenzi wa vituo 28 vya kuchotea maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hiyo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji ambapo inatarajiwa kukamilika ndani ya mwaka wa fedha 2025/2026 na kunufaisha zaidi wananchi 12,570 waishio katika Vijiji vya Gumbiro, Ngadinda na Lilondo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, hadi kufikia Mwezi Machi, 2026, Serikali imelipa jumla ya shilingi bilioni 1.536 katika utekelezaji wa miradi hiyo na itaendelea kupeleka fedha kadiri zinavyopatikana ili iweze kukamilika na kuanza kutoa huduma iliyokusudiwa kwa wananchi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Omary Msigwa.

MHE. OMARY M. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina swali moja la nyongeza. Mheshimiwa Waziri ninatamani kujua ni lini utatembelea Mradi huo wa Maji wa Mtyangimbole, Ngadinda na Gumbiro ambapo miradi hiyo imekamilika na maji yapo kwenye matanki isipokuwa hayajafika kwa wananchi na maji yanamwagika pale? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante. Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa ushirikiano mzuri ambao anaendelea kuutoa na ninamshukuru sana kwa kutupa taarifa nzuri za maendeleo ya miradi ndani ya Jimbo lake. Miradi hii imefikia hatua nzuri kabisa mpaka sasa Mradi wa Gumbiro upo 90%. Pia, Mradi wa Ngadinda upo 67%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, Serikali tumejipanga, na mpaka sasa hatuna changamoto ya kifedha ndani ya miradi hii, na ndiyo maana upo katika hatua nzuri kabisa ya utekelezaji. Ninamtoa hofu Serikali ya Awamu ya Sita itaendelea kutekeleza hii miradi na kupeleka fedha ili iweze kukamilika kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameendelea kuomba. Ninakushukuru sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo.

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Wilaya ya Muleba ni kati ya wilaya kongwe na yenye matatizo makubwa sana ya maji kutokana na jiografia yake. Tuna mradi wa kutoa Maji Ziwa Victoria ambao usanifu umekamilika na ninashukuru Mheshimiwa Rais aliyouongelea wakati wa kampeni; je, ni lini utekelezaji au ujenzi wa mradi huu kwa ajili ya wakazi wa Wilaya ya Muleba utaanza? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa majibu, kama unaelewa kwenye eneo hilo.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Muleba Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumpongeza sana kwa kazi nzuri sana kwa sababu katika utekelezaji wa miradi ya maji, cha

kwanza tunafanya *need assessment* na Mheshimiwa Mbunge alitoa mchango mkubwa sana katika kubainisha mahitaji ya mradi ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo tulifanya upembuzi yakinifu na baada ya hapo, tukafanya usanifu wa kina. Kinachofuatia ni Serikali kutafuta fedha, na sasa tuko katika michakato mbalimbali ya kuhakikisha kwamba fedha inapatikana ili iweze kwenda kutekeleza mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu Serikali hii ambayo imejipambanua kuhakikisha kwamba inamtua mama ndoo kichwani, Wanamuleba wako ndani ya mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba watapata huduma ya majisafi na salama kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameendelea kufuatilia kwa niaba yao. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chifu Thomas.

MHE. THOMAS M. KITIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Ikungi Mashariki, kuna visima vingi vilichimbwa, lakini maji hayajaweza kusambazwa katika maeneo mbalimbali. Mfano mzuri ni Kijiji cha Misule, Kata ya Misughaa. Je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kuhakikisha kwamba wananchi wale wa Kata ya Misughaa, Kijiji cha Misule wanaweza kusambaziwa maji na wanaweza kupata hayo maji ili waweze kuwa na imani ya Serikali yao kwa maana ya kumtua mama ndoo kichwani?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa maeneo ya Misughaa, kwanza kabisa Serikali itachimba visima na baada ya kuchimba visima tunafanya *pump test* na baadaye tunajiridhisha na *que* ya maji. Tukishajiridhisha na *que* ya maji, maana yake sasa ndiyo tunafanya usanifu wa kutengeneza

mtandao unaoendana na maji ambayo yanazalishwa pale. Kwa hiyo, tukishajiridhisha, baadaye sasa tunayafikisha kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, bajeti ya kwanza ilikuwa kuchimba visima, bajeti ya pili ni kusambaza baada ya kujiridhisha na uwingi wa maji yaliyopatikana katika visima. Ninamtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, kwa vile tumekamilisha uchimbaji wa visima na *pump testing* imeishafanyika. Sasa tuko kwenye mchakato wa kuingiza katika bajeti ya kuhakikisha kwamba sasa tunaenda kujenga mtandao wa maji ili maji yawafikie watumiaji na wananchi wa Misughaa. Ninakushukuru sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masache Kasaka.

MHE. MASACHE N. KASAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Mradi wa Maji wa Mazimbu uliopo Kata ya Matwiga ambao utekelezaji umekwenda 65% pamoja na mradi wa Maji wa Kambikatoto ambao utekelezaji wake upo zaidi ya 90% umesimama kwa sasa hivi na wakandarasi wameshaondoka *site,* je, ni lini sasa Serikali itatoa fedha ili miradi hii ya maji iweze kutekelezwa na wananchi waweze kunufaika kama lengo lilivyokusudiwa? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi unapofikia 90%, maana yake umekaribia kutoa huduma ya maji kwa wananchi. Tunayo maelekezo ya Mheshimiwa Waziri, na mimi nimepewa maelekezo ya kusimamia miradi yote ambayo iko ukingoni kutoa huduma kwa wananchi, ni bora ikakamilika ili wananchi waweze kupata matokeo katika miradi hiyo huku tukiwa tunaendelea na miradi mingine ambayo iko katika hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamtoa hofu Mjumbe wetu wa Kamati yetu ya Maji na Mazingira kwa kazi kubwa anayoifanya kwenye Jimbo la Lupa la kuwasemea wananchi ikiwemo hata ule Mradi wa Miji 28 ambao upo katika hatua mbalimbali za mazungumzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuhakikishia Serikali ya Awamu ya Sita imejipanga kwenda kuhakikisha kwamba miradi ya aina hiyo inakamilika na kutoa matokeo kwa wananchi wakiwemo wananchi wa Lupa. Ninakushukuru sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa majibu hayo kwa Waheshimiwa Wabunge. Sasa tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Othman Maulid Suleiman, Mbunge wa Mahonda, aulize swali lake.

Na. 82

Kuongeza Viwanda Nchini

MHE. OTHMAN MAULID SULEIMAN aliuliza:-

Je, ipi mikakati ya Serikali ya kuongeza viwanda nchini ili kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara ninaomba nijibu swali namba 82 kutoka kwa Mheshimiwa Othman Maulid Suleiman, Mbunge wa Mahonda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya CCM pamoja na Dira ya Maendeleo ya 2020 - 2050 inatoa kipaumbele kwenye uwekezaji na uzalishaji wa ndani, ongezeko la thamani la bidhaa zetu za ndani na mkakati wa Serikali unalenga katika kukuza uchumi wa viwanda, kuanzisha viwanda vipya na kufufua viwanda ambavyo vimesimamisha uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika muktadha huo, hadi kufikia mwezi Desemba, 2025, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi, imefanikiwa kuanzisha kongani 36 katika mikoa 16 nchini. Kati ya hizo, kongani sita zipo katika hatua ya ujenzi na baadhi ya viwanda ndani

ya kongani hizo, tayari vimeanza uzalishaji. Mathalani, Kongani ya Kwala iliyopo Mkoa wa Pwani na Kongani ya Kilimanjaro iliyopo Kigamboni ambapo kila moja ina viwanda vinne ambavyo vinaendelea na uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali imeanza kutekeleza Mpango Maalum wa Miaka sita (2025/2026 – 2030) wa kuendeleza viwanda vya ndani ambapo kupitia mpango huo, kongani zipatazo 52 (kongani mbili kwa kila mkoa) zitajengwa. Ujenzi wa kongani hizi zenye viwanda ndani yake utasaidia kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Othman Maulid Suleiman. Waheshimiwa mliowasha *mic* ninaomba mzime.

MHE. OTHMAN MAULID SULEIMAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nilikuwa ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhamasisha wananchi kuweza kuzipenda na kuzinunua bidhaa zinazozalishwa Tanzania, nikiwa na maana ya kununua bidhaa za Tanzania kwanza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, je, Serikali haioni haja ya kuanzisha programu hii ya kizalendo kwa umma ili ipate mwamko wa kuzipenda bidhaa zetu na kuzinunua? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niungane na Mheshimiwa Mbunge kwamba jukumu la kukuza, kuendeleza na kuhamasisha bidhaa zetu za ndani ni jukumu letu Watanzania wote. Wizara ya Viwanda na Biashara chini ya maelekezo ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia Taasisi ya *TanTrade* tunaendelea kufanya mradi mkubwa wa *branding* wa bidhaa ambazo zinatengenezwa Tanzania maarufu kama *Made in Tanzania Brand*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, pamoja na hayo kupitia miradi mbalimbali ya uendelezaji wa viwanda, tunaendelea kutoa hamasa kwa Watanzania na mwamko sasa hivi umeendelea kuwa mkubwa hasa kwa viongozi wa Serikali na taasisi binafsi ambao tunaendelea kuona wakivaa ama wakitumia bidhaa za Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, ninaomba kutoa rai kwa sisi Wabunge kuendeleza hamasa yaku-*promote* bidhaa zetu za ndani kwa kuzitumia na kuonesha Watanzania kwamba bidhaa zetu zina ubora, zinakidhi viwango na tunazipenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nuru Issa, jiandae Mheshimiwa Imamu Vuai. Mheshimiwa Imamu Vuai au Mheshimiwa Nuru Issa hajaweza kuwasha? Mheshimiwa Imamu Vuai.

MHE. IMAMU MTUMWA VUAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi. Ni lini Serikali itakuja na mkakati madhubuti wa kulinda viwanda vya ndani dhidi ya ushindani wa bidhaa za bei nafuu kutoka nje?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nishukuru kwa swali zuri la Mheshimiwa Mbunge kuhusiana na suala la kulinda viwanda vyetu vya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, tumeendelea kutengeneza sheria, lakini pia tumeendelea kutengeneza kanuni na kuboresha kanuni mbalimbali, lengo ni kulinda bidhaa za ndani, na pia kuchochea uwekezaji na kuendeleza uzalishaji wa bidhaa zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili, tunaweza kuona wiki iliyopita Waziri wa Viwanda na Biashara aliongoza zoezi la kukamata mali ambazo zimezalishwa kinyume na sheria ama zimeingizwa kinyume

cha sheria ambazo zimeingizwa sokoni chini ya viwango ama kinyume cha taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la kufanya hivi, ni kulinda viwanda vyetu vya ndani, kuongeza imani ya walaji, lakini pia kulinda mitaji ya Watanzania. Tutaendelea kufanya hivyo ili kuwavutia wawekezaji wapya, lakini pia kulinda wawekezaji na wazalishaji wa bidhaa za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Stella Ikupa.

MHE. STELLA I. ALEX: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Je, ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba viwanda vyetu vinazalisha bidhaa ambazo ni shindani, yaani bidhaa ambazo ni sawasawa na zile za nje au zaidi ya zile bidhaa za nje? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada za kuanzisha viwanda vipya na kufufua viwanda ambavyo vinaendelea na uzalishaji katika maeneo mbalimbali, tumeendelea kuvutia wawekezaji, na pia kuhamasisha teknolojia mpya na matumizi ya teknolojia mpya kwa uzalishaji wa bidhaa za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili, Wizara ya Elimu na Teknolojia, tumeona imeendesha programu mbalimbali za kuongeza ujuzi wa vijana wetu katika vyuo vyetu vya *VETA* ili kutumia ujuzi mpya, teknolojia mpya, kupunguza gharama ya uzalishaji, kuwa na bei shindani katika soko, lakini kuwa na viwango ambavyo bidhaa zetu zinaweza zikashindana katika soko, siyo tu kikanda, lakini Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na wadau wengine wakiwemo Wizara ya Elimu, tunaendelea kuboresha ujuzi wa vijana wetu ili wazalishe bidhaa zenye ushindani katika soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Asia Halamga.

MHE. ASIA A. HALAMGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kata ya Mogitu iliyopo Wilaya ya Hanang ina malighafi ya kutosha ya kutengeneza simenti inayoweza kudumu kwa zaidi ya miaka 100. Je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kuambatana na mimi ili kwenda kuona rasilimali hii muhimu kwa nchi yetu? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaomba kupitia Bunge lako kumwahidi Mheshimiwa Mbunge Asia Halamga kwamba, nipo tayari kuambatana naye katika jimbo lake. Pili, kumhakikishia kwamba, Serikali inaendelea na tathmini ya viwanda vya kimkakati kwa kuangalia malighafi ambazo zinaweza kutumika katika uzalishaji wa bidhaa mbalimbali na kuongeza thamani ya bidhaa zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo, Mkoa wa Manyara, hususan Jimbo la Hanang, ni miongoni mwa maeneo ya kimkakati ambayo tunaendelea kuangalia uwepo wa malighafi, hasa za chumvi na simenti, ili kuangalia namna gani tunaweza kuvutia wawekezaji kuwekeza katika bidhaa hizo. Lengo ni kuongeza uzalishaji wa bidhaa na kujihakikishia soko katika Ukanda wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYETIKI: Mheshimiwa Hawa Mwaifunga.

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kuniona. Kwa kuwa, tathmini na eneo la ujenzi wa kiwanda cha mbolea katika Mkoa wa Tabora tayari limepatikana na mwekezaji yupo, ni lini Serikali itaanza mchakato kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha mbolea katika Mkoa wa Tabora? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Jibu, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunafahamu kwamba kilimo ndiyo uti wa mgongo na kimeajiri wengi. Ilani ya Chama cha Mapinduzi pamoja na Dira ya Maendeleo ya 2020 – 2050 inazungumzia ni jinsi gani tunaenda kutumia kilimo kama mhimili wa kutupeleka kwenye uchumi wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika muktadha huo, Mheshimiwa Mbunge ataungana nami kujua changamoto ambayo inatukabili kwenye sekta ya kilimo, hasa kutokana na vita inayoendelea kule *Ukraine* na pia, kule Mashariki ya Kati ambao ndiyo wazalishaji wakubwa wa mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto hii inatupeleka kuona kwamba, sisi kama Serikali, tunatafuta majawabu ya uhakika kuona sekta ya kilimo haiyumbi ili kuhakikisha tunaenda kuanzisha viwanda vya mbolea na kuviimarisha vile vilivyopo, ili kutoa majibu ya uhakika katika suala zima la usambazaji wa mbolea na kuimarisha sekta ya kilimo katika nchi yetu, ambayo ndiyo uti wa mgongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo mengi ya Waheshimiwa Wabunge kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara. Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii. Mheshimiwa Salumu Khamis Salim, Mbunge wa Meatu.

Na. 83

Tembo Kuvamia Vijiji, Meatu

MHE. SALUM K. SALIM aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka na wa kudumu wa kuzuia tembo kuvamia Vijiji vya Meatu?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Salum Khamis Salum, Mbunge wa Meatu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za haraka katika kukabiliana na changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu, hususan tembo, kwenye maeneo mbalimbali nchini, vikiwemo Vijiji vya Wilaya ya Meatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hizo ni pamoja na kujenga vituo vinne vya askari wa kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu na kuwawezesha rasilimali watu pamoja na vitendea kazi muhimu. Kupitia vituo hivyo, kati ya mwezi Julai, 2025 hadi Machi, 2026 doria imefanyika na kuwezesha kudhibiti matukio 352 katika Wilaya ya Meatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendelea kuimarisha matumizi ya teknolojia na mbinu mpya, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa uhifadhi katika mwaka wa fedha ujao, inatarajia kujenga uzio wa umeme wenye urefu wa kilometa 104 kwenye mpaka wa hifadhi ya Pori la Akiba Maswa kwa upande wa Magharibi unaopakana na makazi ya wananchi katika Wilaya za Meatu, Itilima na Bariadi. Uzio huo utawezesha kudhibiti tembo kutoka nje ya hifadhi. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Salum Khamis Salum, swali la nyongeza.

MHE. SALUM KHAMIS SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu ya Naibu Waziri, lakini kwa sababu suala la tembo katika Wilaya ya Meatu na Jimbo la Meatu limekuwa ni la siku nyingi na mkakati wake ni huu huu kila siku, na majibu ni hayo hayo, je, Mheshimiwa Naibu Waziri haoni kwamba, kuna sababu ya kuwa na azma kubwa ya kuwaondoa tembo ambao wanaishi maeneo ya watu kwa sasa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili. Hawa tembo sasa hivi tunavyoongea, wanaharibu mazao ya watu na wanawaumiza watu walioko kwenye mashamba yao. Je, ni kwa nini sasa Wizara isichukue hatua za mwanzo kuwaondoa wale tembo wote ambao wako ndani ya mashamba ya watu? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaomba kumpongeza sana Mheshimiwa Salum kwa kuwa na yeye sasa ni sehemu ya hifadhi na anashirikiana na taasisi zetu katika kuhami jamii yetu dhidi ya wanyama hawa wakali na waharibifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijibu maswali yake yote mawili kwa pamoja. Ninaomba kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri nitoe maelekezo kwa Kamishna Mkuu *TAWA* na *TANAPA* kwa kushirikiana na halmashahuri zetu kote nchini waende kuwaondoa wanyama hao ambao wapo katika makazi ya watu na katika mashamba yao. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Kwa vile umejibu kwa ujumla, basi ninakushukuru sana kwa majibu hayo.

Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Selina Henry Kingalame, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 84

Umuhimu wa Elimu kwa Vitendo *(Internship)*

MHE. SELINA H. KINGALAME aliuliza: -

Je, Serikali haioni haja ya kuanzisha Mfumo wa Elimu ya Vitendo *(Internship)* kwa kada nyingine za elimu, kama ilivyo Elimu ya Utabibu?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo, Mhehsimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, ninaomba nijibu swali la Mheshimiwa Selina Henry Kingalame, Mbunge wa Viti Maalumu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa mafunzo kwa vitendo *(internship)* katika kuimarisha ubora wa wahitimu. Kwa sasa Serikali kupitia vyuo vya kati na vya elimu ya juu, imeweka utaratibu wa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi, ambapo uendeshaji wake hutofautiana kulingana na kada na mahitaji ya taaluma husika kwa kutumia mfumo wa *field practical* na *industrial trainings*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Serikali inaendelea kuboresha miongozo ya mafunzo kwa vitendo, ili kuongeza tija na kuhakikisha yanaendana na mahitaji ya soko la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, katika kada ya ualimu, Serikali imeandaa Kiunzi cha Kitaifa cha Mafunzo ya Ualimu kwa Vitendo *(National Teachers' Internship Framework)* cha Mwaka 2026 ambacho kitatekelezwa kwa mtindo unaofanana na kada ya utabibu na kinatarajiwa kuanza katika mwaka wa masomo 2026/2027. Hivyo, Serikali itaendelea kuboresha mfumo wa utoaji mafunzo kwa vitendo kadiri itakavyoonekana inafaa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Selina Henry Kingalame.

MHE. SELINA H. KINGALAME: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Swali langu la kwanza, nini kauli ya Serikali kuhakikisha hizi *internships* zinaanza kutolewa kwa haraka kwa kada zote za kitaaluma, ili kuondoa ombwe la wahitimu wengi kukosa fursa za ajira kwa kigezo cha uzoefu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Kwa kuwa, changamoto ya uzoefu imekuwa kilio cha muda mrefu, je, Serikali

haioni haja sasa hizi *internships* ziwe ndiyo uzoefu hitajika kwa wahitimu wanapoomba ajira, na siyo miaka miwili, mitatu na kuendelea? Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu katika swali la msingi, Serikali inatambua umuhimu wa kuanzisha na kuimarisha Mfumo wa Mafunzo kwa Vitendo katika kada mbalimbali ili kuwawezesha vijana kupata uzoefu unaohitajika. Serikali itaendelea kufanya tathmini kuhusu upanuzi wa utoaji wa mafunzo kwa vitendo katika kada nyingi tofauti zaidi ili kuhakikisha utekelezaji wake unakuwa endelevu na wenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili, Serikali inatambua kuwa, kigezo cha uzoefu kwa wahitimu katika baadhi ya nafasi ni kikwazo. Ndiyo maana tumeendelea kufanya tathmini juu ya upanuzi wa mafunzo haya kwa vitendo ili kuona kwamba mafunzo haya yanakuwa sehemu ya kuwatayarisha wahitimu kuingia katika soko la ajira. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hii ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge lako na kutoa maelezo, ninaomba na mimi nitumie nafasi hii kumshukuru sana Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuniona na kunipa heshima hii ya kuwa Waziri ninayesimamia eneo la utawala bora na utumishi wa Umma ndani ya ofisi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno hayo, ninaomba kwanza kumpongeza Naibu Waziri kwa maelezo mazuri aliyoyatoa, ambayo ni ya ukweli pasi na shaka kwamba, ndiyo utaratibu Serikali imeweka, lakini liko jambo moja la kuongeza katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2024, kwa maana ya mwaka wa kifedha 2024/2025, Serikali ilikamilisha mwongozo wa kujitolea. Mwongozo ambao unatakiwa sasa uende kwa wadau ukajadiliwe ili uweze kuwa na *input* ambazo kila mmoja atakuwa nazo, lakini kila kada ambayo imezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge katika maswali yao, nayo itakuwa imeangaliwa ili kuweza kujibu masuala na matakwa wanayotaka wananchi wa Tanzania juu ya mfumo mzima wa kujitolea ili kufanya elimu ya vitendo iweze kuwa na ubora unaotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, kitabu hicho au mwongozo huo tutaupitisha katika vikao vinavyohusika kupitia Kamati za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, utaletwa katika Bunge lako ili baada ya Bunge kuidhinisha, basi mfumo huo sasa utangazwe rasmi uweze kwenda kuwa mfano katika elimu ya kujitolea na vitendo itakayokwenda kuzaa matunda mazuri kwa kesho ya Tanzania. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Ninakushukuru sana kwa maelezo hayo ya ziada kuhusiana na elimu kwa njia ya vitendo. Basi ninawashukuru kwa majibu hayo ya Mheshimiwa Mbunge.

Tunaendelea sasa na Wizara ya Uchukuzi. Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 85

Wanawake Kushiriki kwenye Miradi ya Uchukuzi

MHE. JANETH E. MAHAWANGA aliuliza: -

Je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha wanawake wanashiriki katika miradi mikubwa ya uchukuzi, ikiwemo Mradi wa *SGR*?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeweka sera, sheria na miongozo mbalimbali inayolenga kuhimiza na kuhakikisha usawa wa kijinsia katika ajira. Katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati, ikiwemo ujenzi wa *SGR*, wakandarasi na washauri wanawajibika kuzingatia masharti ya mikataba, pamoja na sera za Kitaifa ambazo zinataka utoaji wa fursa sawa za ajira kwa wanawake na wanaume katika kada mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa masharti ya mikataba ya ujenzi inayotumika katika Ujenzi wa *SGR*, mkandarasi na mshauri, wanatakiwa kufuata sheria zote za nchi, zikiwemo zile zinazohusu ajira, kazi na usawa wa kijinsia. Hivyo, Serikali imeendelea kusisitiza utekelezaji wa matakwa haya ili kuhakikisha wanawake wanashiriki kikamilifu katika miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia, inaendelea kufanya ufuatiliaji na tathmini ya mara kwa mara ya utekelezaji wa sera na miongozo hiyo kwa lengo la kuhakikisha kuwa, malengo ya usawa wa kijinsia yanafikiwa na wanawake wanapata fursa stahiki za kushiriki katika miradi mikubwa ya kimaendeleo nchini.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga.

MHE. JANETH E. MAHAWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, ni kwa namna gani Serikali imeandaa programu maalumu au mafunzo ya uwezeshaji ili kuhakikisha wanawake wanashiriki kikamilifu katika miradi hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; je, Serikali imeweka mikakati gani kuhakikisha wanawake hawabaki nyuma katika fursa za zabuni na uwezeshwaji kiuchumi katika miradi mikubwa ya Serikali? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Janeth, kama ambavyo ameongezea. La kwanza, ametaka kufahamu programu na mafunzo mbalimbali, ambazo kimsingi Serikali hii inafanya katika kuimarisha wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kwanza kabisa, kama nilivyosema kwenye swali la msingi, msingi namba moja ni uwepo wa sheria na miongozo mbalimbali. Kwa hiyo, cha kwanza Serikali inahakikisha kwamba, sheria, miongozo na kanuni mbalimbali ambazo zinawapa fursa wanawake zinapewa msukumo wa kipekee, lakini pia ziko programu mbalimbali kama vile mafunzo ambayo kwa mfano wenzetu wa *TanTrade* wanayo, wenzetu wa Bodi ya Wakandarasi wanayo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo ya elimu kwa vitendo *(internship)* hapa yameongelewa mara kadhaa. Yote hiyo ni kuwajengea uwezo wanawake kuhakikisha kwamba, wanapata uwezo wa kushiriki katika ujenzi wa uchumi wa nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tumeweka mafunzo muhimu ya kiufundi, kama vile kupitia vyuo vyetu vya *VETA,* ambapo tunawajengea uwezo wanawake, wakimaliza, wakipata ufundi huo, waweze kwenda kwenye shughuli za uzalishaji mali na hivyo kuweza kushiriki kikamilifu kuwa na nguvu ya kifedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipaumbele mbalimbali katika utoaji wa ajira, yote haya pamoja na mengine, imekuwa ni mambo muhimu ambayo tunayafanya, kama sekta, ikiwa ni pamoja na kutoa elimu mbalimbali katika masuala ya fidia, kwamba, fedha mtakazopata zitumikaje, ili isije ikatokea mtu amepata *compensation* halafu tena zile fedha amezitumia vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kama tulivyozungumza, mikakati mbalimbali inatolewa kuhakikisha kwamba, wanapata nafasi kama vile kwenye zabuni na kadhalika. Hii ni pamoja na fursa za kielimu. Hapa kwenye elimu, nchi yetu imetoa nafasi kubwa kwa mwanamke kuhakikisha kwamba, kila mtoto wa kike anayetaka kusoma shule au anayetaka kwenda shule kuanzia elimu ya awali mpaka chuo kikuu, anashiriki kikamilifu bila ubaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia inatoa fursa maalum kama vile ambavyo Mheshimiwa Rais kwa ubunifu wake amekujanavyo, kama vile *Samia Scholarship Award,* ambayo kimsingi inawasaidia watoto wa kike waliofanya vizuri kwenye masomo mbalimbali, kama vile sayansi, waweze kupata msukumo wa kipekee na kuwajengea uwezo waweze kufikia ndoto zao ambazo kimsingi wanazihitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *financial institution* zetu (taasisi za kifedha) zimekuwa ni maeneo mengine inapotokea mwanamke ana bidii katika shughuli za uzalishaji mali, wanatoa msukumo wa kipekee katika kumpa mikopo, ili kuhakikisha kwamba, wanawake kwenye nchi yetu wanafanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye Sheria zetu za Manunuzi, imetoa fursa na upendeleo maalumu, kwamba 30% ya kandarasi zetu au *tender* zetu, basi msukumo utolewe kwa wananchi, kwa wanawake, na pia, upande wa udhibiti vitendo vya kikatili ni moja kati ya mikakati ambayo Serikali inafanya, ili kumfanya mwanamke asijisikie mnyonge kwenye jamii, ashiriki kwenye uzalishaji kama kiumbe mwingine kwenye jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kabla sijahitimisha ikiwa ni pamoja na kwenye uongozi, tayari unaweza kuona jinsi ambavyo wanawake wanashirikishwa katika masuala ya uongozi. Pamoja na kuwapa nafasi ya kushiriki kama watu wengine, bado wanapewa dawati la pekee kama vile kwenye Viti Maalumu ama katika uteuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo ni kwamba, washiriki katika maamuzi wanapotunga sera au kanuni au sheria na wao waweze

kuwa sehemu ya kuwasemea wanawake wenzao nchi nzima. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hawa Chakoma.

MHE. HAWA M. CHAKOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Mheshimiwa Naibu Waziri kwenye ufafanuzi wake au katika majibu ya swali la nyongea tayari ameshajibu nililotaka kuuliza. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Edifonsi Kanoni.

MHE. EDIFONSI J. KANONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza. Wilaya ya Kalambo ina bandari ambayo ni muhimu sana katika uchumi wa nchi, uchumi wa Wilaya ya Kalambo na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii bandari Serikali imewekeza shilingi 7,200,000,000 lakini kutokana na mabadiliko ya tabianchi, imezama toka mwaka 2023. Nini mpango wa Serikali kuboresha bandari hii ili ianze kufanya kazi iwanufaishe wananchi wa eneo lile pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa, hilo swali halifanani kabisa na swali la msingi, labda kama Mheshimiwa Waziri ana majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaweza kufafanua kidogo. Kwanza ninamshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kuweza kutambua kazi ambayo Serikali imefanya kwenye upande wa Bandari yetu ya Kalambo, Mkoani Rukwa, ambapo ni moja ya bandari ambazo zilirasimishwa, lakini pamoja na kurasimishwa Serikali iliona umuhimu ikaiendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa, pamoja na dhamira njema ya Serikali kuiendeleza tulipata changamoto kubwa ya maji. Kwa hiyo, maji yalijaa na yale maji hayakujaa kwenye Bandari ya Kalambo peke yake, ni karibu maziwa makuu yote. Tayari Serikali

inaandaa mkakati, tumetafuta mkandarasi au mshauri mwelekezi, ambaye anatusaidia kutuambia nini tukifanye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ni katika kutatua changamoto ya maji yaliyojaa kwa sasa hivi. Mbili, *in long run,* ni tufanye nini, ili tatizo kama hili likijitokeza, basi lisiweze kuathiri bandari zetu na hivyo, wananchi wa Kalambo na maeneo mengine wanufaike na bandari ambazo zipo kwenye maeneo yao.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, kwa hili, nilitegemea wanawake wengi wangeuliza ushiriki wa wanawake kwenye miradi mikubwa, lakini kwa vile hakuna wanawake wengi, basi ninakushukuru kwa majibu yako.

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, Mbunge wa Ushetu, aulize swali lake.

Na. 86

Kupunguza Tozo kwa Zao la Tumbaku

MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI aliuliza: -

Je, upi mpango wa kupunguza tozo kwa wakulima wa tumbaku, kwani kwa kila mfuko wa mbolea, benki hukata USD 0.5 na Benki Kuu USD 5.80?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, Mbunge wa Jimbo la Ushetu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuboresha kilimo cha zao la tumbaku ili kuongeza

uzalishaji na tija kwa mkulima kwa kuimarisha mapato ya mkulima na kupunguza gharama za uzalishaji wa zao hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa, Serikali ipo kwenye hatua ya kupitia gharama za uzalishaji za mkulima ili kuainisha maeneo ambayo yanahitaji kufanyiwa maboresho ikiwemo riba za kibenki ambayo ni dola za Kimarekani 0.5 kwa mfuko wa mbolea ikiwa ni ada ya hati ya dhamana ya benki iliyotoa mkopo pamoja na dola za Kimarekani 5.8 inayojumuisha riba ya mkopo, dhamana ya Benki Kuu, bima ya mkopo na kodi ya ongezeko la thamani. Aidha, jitihada hizo zitaenda sambamba na kushirikisha Benki zinazotoa mikopo hiyo kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Bodi ya Tumbaku na Tume ya Maendeleo ya Ushirika, zitaendelea na jitihada za kuboresha mazingira ya uzalishaji kwa wakulima wa zao la tumbaku ikiwemo kuboresha tija na kuainisha tozo ambazo zinahitaji kufanyiwa maboresho ili kuweza kupunguza gharama za uzalishaji kwa wakulima wa zao hilo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani.

MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa nini sasa Serikali isikae na wadau wote wa sekta ndogo ya tumbaku pamoja na taasisi zote za fedha ili kubaini haraka changamoto ambazo zinaonekana kuongeza gharama za uzalishaji kwa mkulima ili kupunguza gharama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Kwa kuwa bei ya pembejeo ilipangwa kabla bei ya tumbaku haijatoka na walitumia *grant list* ya mwaka 2025 ambayo ilikuwa dola 2.1, lakini pia sasa bei ya tumbaku imeshuka na kuwa dola 1.5, Serikali haioni sasa kwamba wakulima hawa wanaenda kupata hasara na kusababisha kuuvuruga ushirika?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Cherehani, Mbunge wa Ushetu na

mdau mkubwa wa zao la tumbaku. Moja, amekuwa mtetezi mkubwa wa zao hili, lakini amekuwa akilisemea. Jambo moja ambalo nikuthibitishie ni kwamba Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na bahati nzuri hata Waziri wangu yupo hapa ananisikia, moja ya maelekezo ambayo Rais alitupatia ni kuwa wadau wanahitaji kukaa kikao na sisi ili kufanya mapitio na kuangalia namna bora ambayo tunaweza tukafanya maboresho tunaweza tukafanya kikao hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwondoe tu shaka kwamba Serikali ipo tayari muda wowote kukaa na wadau, mabenki na sekta binafsi ili kuhakikisha kwamba tunafanya maboresho sahihi ambayo yanaweza kumsaidia mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bei ya tumbaku, moja wewe mwenyewe unafahamu kwamba bei ya tumbaku huwa inapangwa kwa kuangalia gharama za uzalishaji, hiyo ndiyo tunasema *baseline*. Ndiyo mahali ambapo huwa tunaanzia, halafu tukishaangalia zile gharama ndiyo tunatengeneza bei ambayo inaweza kumsaidia mkulima kupata faida. Kwa hiyo, bei ya mwaka huu baada ya kuzingatia vigezo vyote ndiyo ikaangukia katika dola 1.95.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mapendekezo ya Mheshimiwa Mbunge aliyoyasema, bado Serikali tunaweza tukaangalia na kuona namna bora ambayo tunaweza tukampatia faida zaidi mkulima hapa nchini, ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge, na muda wetu wa maswali umekwisha.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa maswali umefikia ukingoni na hapa tuna matangazo.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza tunayo matangazo ya wageni waliopo Bungeni asubuhi hii ambao ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge.

Tunao wageni sita wa Mheshimiwa Maryprisca Winfried Mahundi, Mbunge na Naibu Waziri wetu wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, ambao hawa ni Mapadre wa Shirika la *Camel* kutoka Uyole Mkoani Mbeya, karibuni sana Mapadre wetu. *(Makofi)*

Kuna wageni wanne wa Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, Mbunge, ambao ni familia yake kutoka mkoani Tanga, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, ambao ni Wachungaji kutoka Bunda Mkoani Mara, karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 12 wa Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge, ambao ni wanamaombi na wanakwaya 23 kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tuna wageni ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Tunao wageni watano kutoka *Youth Orphans and Women Organization* kutoka Mkoani Tabora, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye Ndugu Wilhelmina Soma kutoka Tanzania *Atomic Energy Commission* Mkoani Kilimanjaro, karibu sana, nimemwona yule pale. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wananchi sita kutoka Mkoa wa Pwani, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wanafunzi 65 na walimu sita kutoka shule ya Shalom Jijini Arusha, karibuni sana wanafunzi wetu kwa ajili ya mafunzo katika Bunge letu. *(Makofi)*

Katibu.

NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

(Majadiliano Yanaendelea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano yetu, tutaanza na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, atafuatiwa na Mheshimiwa Baraka Ambindwile Ulimboka, Mheshimiwa Silvery Luboja Salvatory na Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, wajiandae.

MHE. DEODATUS P. MWANYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye hoja iliyopo mbele yetu inayohusiana na hotuba ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema ili kuweza kusimama hapa leo na kuweza kutoa mchango wangu angalau kwa kifupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Waziri wetu Mkuu kwa kuwasilisha bajeti nzuri sana, bajeti ambayo inatoa mwelekeo wa utendaji wa Serikali. Siyo utendaji tu, lakini na makadirio ya matumizi na mapato kwa kipindi cha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watu wa Njombe, tumekuwa ni wanufaika wakubwa wa miradi mbalimbali ambayo tumeipata katika kipindi hiki cha bajeti iliyopita, lakini katika kipindi cha miaka mitano ya Serikali ya Awamu ya Sita. Tuna kila sababu ya kumshukuru sana Rais kwa mambo mengi makubwa ambayo ametufanyia wananchi wa Njombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo ambayo yamefanyika katika maombi ya kawaida ya kibajeti, lakini kuna mambo

yamefanyika kwa sababu tumemwomba Rais moja kwa moja alipotutembelea Njombe, na tuna mifano mingi ya mambo hayo na ndiyo maana tuna kila sababu ya kusema ahsante kwa mambo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa hatuna Chuo Kikuu Njombe, na tumekuwa na kiu ya muda mrefu sana ya kuwa na Chuo Kikuu, lakini Mheshimiwa Rais alitoa kibali cha haraka, leo tunavyoongelea Chuo Kikuu cha *UDOM*, *campus* ya Njombe inajengwa kwa *speed* kubwa sana, na mwaka huu *intake* ya kwanza inaingia pale Njombe kwa ajili ya kujifunza masuala ya ujasiriamali yanayoendana na rasilimali zilizopo Njombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa hatuna uwanja wa ndege wa kisasa, tumemsikia Naibu Waziri, akijibu maswali hapa, akionesha namna gani Wananjombe tuliomba jambo hili na Serikali imelisikiliza na imeamua kulitekeleza, na sasa mchakato upo katika hatua nzuri ya kufanya tathmini ya eneo na kulipa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero yetu kubwa kuliko zote Njombe, na nilisema, ilikuwa ni maji. Tumepata miradi mingi ya maji karibu mitano, uwekezaji wa shilingi bilioni 60 ndani ya Mji wa Njombe. Miradi ipo katika hatua mbalimbali na inaendelea vizuri, na kero ya maji muda siyo mrefu itakuwa historia kwa wananchi wa Njombe. Kwa hiyo, tuna kila sababu ya kuwa na shukrani kwa yanayofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo yote, bado tuna changamoto ambazo tunaendelea kuzipitia, na wananchi wa Njombe wangependa kuzisikia Mbunge wao waliyemchagua akiziongelea katika ukumbi huu wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Njombe ni Mkoa wa kiuchumi na wengi wanalifahamu hilo, na waliotembelea Njombe wanafahamu hilo. Njombe ni Mkoa ambao una baraka, Njombe inao mchango mkubwa kwenye uchumi wa Tanzania, Njombe ina *potential* kubwa sana ya kuchangia mara dufu, mimi nasema siyo maradufu labda mara mia ya kile inachochangia leo; lakini inachangamoto za msingi

ambazo zikitatuliwa, tuna uhakika Njombe tunayoiongelea itakuwa ni Njombe tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo barabara yetu ya Itoni – Lusitu yenye urefu wa kilometa 51. Barabara hii tunaendelea kumshukuru Rais, kwa sababu alipokuja katika barabara 14 za kwanza alizosaini ili ziingie kwenye mchakato wa manunuzi, barabara ya Itoni – Lusitu ilikuwemo shilingi bilioni 95, ukiongeza na *VAT* kama shilingi bilioni 110. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa furaha mkandarasi amepewa *site,* ameijenga kwa kipindi cha mwaka mmoja, kutengeneza tuta na kazi inaendelea, lakini kwa masikitiko, kwa kipindi cha miaka miwili barabara hii imesimama, lakini usimamaji wa barabara hii umekuja na maumivu makubwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Njombe kwa sababu barabara hiyo inayojengwa ndiyo wanayotumia kupitisha mazao mbalimbali, mazao ya Njombe ya kilimo ni viazi, mazao ya misitu ambayo yanahitaji usafiri. Kwa hiyo, wamepitia vipindi viwili vya mvua ambavyo havikuwa vizuri kwao, ambavyo vimewarudisha nyuma na vingine vimewatia umaskini. Tunaiomba sana Serikali ilitilie maanani suala la barabara ya Itoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ndiyo inayokwenda kwenye migodi ya Liganga na Mchuchuma. Huwezi kuongea Liganga na Mchuchuma bila kuongelea barabara ya Itoni – Lusitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali, tunafahamu mkandarasi haidai Serikali kwa maana ya kwamba kazi iliyofanyika amelipwa, baada ya sisi kuweka nguvu kubwa, lakini tunachosema, tunaomba itakapoanza ujenzi baada ya hizi mvua kwisha, tunaomba barabara hii isisimame tena, kwa sababu ni barabara kubwa ya kipaumbele, ni barabara ya kiuchumi, na ni barabara inayofungua Liganga na Mchuchuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niliseme hilo kwa udogo wake. Tuna barabara ya Makambaku – Songea ambayo tunahitaji

iweze kukamilishwa. Barabara hii ina miaka 40, Kamati ya Miundombinu imeitembelea, ni barabara kubwa ya Uchumi. Kama ingekuwa ni katika mwili wa binadamu, ni mshipa mkubwa wa damu. Tunaomba sana Serikali ifanye utaratibu wa kutafuta fedha. Tunafahamu inaendelea na mchakato ili tupate barabara hii iweze kuanza kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la barabara za vijijini kwangu ndiyo eneo kubwa na la muhimu sana. Tuna mtandao mkubwa sana wa barabara Njombe, karibu kilometa 1,000 za Barabara, ambapo ni kilometa kama 40 tu za lami. Mazao yote ya viazi, parachichi, mazao ya mbao, mazao ya chai yote yanatoka katika maeneo ya vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Njombe ni Jimbo la Mjini na Vijijini. Mazao yote yanatoka vijijini ambapo kuna uhitaji mkubwa sana wa barabara. Sasa mimi nasema kuna *vicious cycle*, kwa sababu Mwenyezi Mungu ametubariki na mvua nyingi na mazao mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao hayo yanahitaji magari makubwa yaweze kuyachukua. Magari hayo yanahitaji kuingia vijijini. Magari ya tani 10, tumeshasahau tunaongelea *semitrailer* tani 32, tani 40 ndiyo yanayokwenda vijijini kuchukua mizigo. Kuwalisha Watanzania sio Wananjombe peke yao, ni Watanzania wa Mikoa karibu yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitoa hoja hapa na Wabunge wengi walichangia. Katika mgawanyo wa fedha ya *TARURA*, kwanza tunaishukuru Serikali kwa kuongeza bajeti kufikia *1.2 trillion,* lakini tulidhani kwamba ingekuwa ni busara, yale Majimbo ambayo yana mijini na vijijini yangeangaliwa kwa namna ya pekee ili angalau yaongezewe fedha ili ziweze kukidhi kusaidia kutengeneza hizo barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana mwaka 2021/2022 nilijenga hoja kubwa sana hapa ya barabara, tukapata fedha za kutosha, shilingi bilioni 3.8 kwa ajili ya ujenzi wa barabara za mji wa Njombe, lakini uhakika ni kwamba shilingi bilioni 1.5 ilikwenda kwenye barabara za mjini na iliyobaki ilikwenda barabara za vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli barabara za vijijini ambazo tulizijenga kwa zile fedha, leo hii ukienda hutaamini kama hizo barabara ni zile tulizotumia fedha nyingi. Kwa hiyo, ninakubaliana na hoja ya Waheshimiwa Wabunge hapa, ni bora twende pole pole kujenga barabara za vijijini kuliko kwenda kupoteza fedha kwa kujenga barabara ambazo zinaondolewa na mvua kila mwaka unapokuja. Ni hasara kwa nchi yetu na kwa Serikali. *(Mkaofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, Waziri Mkuu, hapa aliongelea kuhusu lumbesa, ninamshukuru sana. Ni kero kubwa sana kwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na mikoa mingine kama Kilimanjaro na Kagera. Maeneo ya mahindi, vitunguu na viazi, wananchi wamekuwa wakinyonywa kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru Waziri Mkuu, kwa kulisema. Ninaomba nitoe ombi, jambo hili ili lifanikiwe, linahitaji lisimamiwe kwa ukaribu, Halmashauri zote. Wananchi wa Njombe wakiamua kutekeleza suala la lumbesa; kutokuwa na lumbesa, kufunga mizigo kwa kilogramu 100; wananchi wa Chunya wasipofanya, wananchi wa Njombe ndio watakaopata hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, linatakiwa lisimamiwe kwa ukamilifu, lifuatiliwe, kuwe na *monitoring* na wenzetu wa TAMISEMI wahakikishe kuwe na *measures* kwa Maofisa wa Halmashauri ambao hawatasimamia agizo la Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika.

Waheshimiwa Wabunge, kwa vile wachangiaji bado ni wengi sana, ninaomba tujali muda, kengele ya pili ikilia, basi tuweze kumaliza. Jitahidini kufupisha au kuweka mambo ya msingi ambayo unaona ni lazima uyazungumze.

Tunaendelea na Mheshimiwa Baraka Ulimboka, Mheshimiwa Silvery Salvatory, Mheshimiwa Zuena ajiandae.

MHE. BARAKA A. U. MWAMENGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia Ofisi hii ya Waziri Mkuu. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, aliyetufikisha siku ya leo tukiwa wazima, wenye afya njema na leo tupo Bungeni hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kuipongeza Serikali ya Awamu ya Sita kupitia kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais na jemedari wetu kwa jinsi ambavyo ameendelea kuisimamia Serikali na malengo mazima ambayo yanatufanya tunaendelea kupanga bajeti hizi na fedha zinatolewa katika Majimbo yetu. Ninaishukuru sana Serikali na ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninamshukuru mwasilishaji wa bajeti hii ambaye ni Waziri Mkuu, kwa jinsi ambavyo amefanya ziara ndani ya majimbo yetu na katika wilaya zetu mbalimbali, ameendelea kusimamia kile ambacho aliahidi hapa kuwa anaenda kusimamia katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali. Kama Mtendaji Mkuu wa Serikali, ameendelea kufanya haya kwa kumaanisha na kuendelea na ziara ambazo tunaamini zinaleta tija ndani ya majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba tu, kwa sababu ndani ya Jimbo langu aliahidi kurudi tena, basi ninaomba, kwa sababu hakufanya mkutano, aliahidi kurudi tena, ninamwomba pale atakapopata nafasi, aweze kurudi ili akafanye mikutano kama alivyokuwa ameahidi alipokuwa ameshindwa kufanya mkutano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo, nianze kuchangia pia kutoa pole kwa maeneo mbalimbali ambayo yamepata mafuriko kwa mvua ambayo ni neema ya Mungu, ametupatia, lakini pale ilipozidi, tutoe pole sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee sana nitoe pole kwa wananchi wa Jimbo langu ambao kwa sehemu kubwa wameathirika na

mafuriko hayo ya mvua zinazoendelea. Nitoe pole sana kwa walioathirika, baadhi ya Kata za Katumbasongwe, Bujonde, Ngonga, Kanjunjumele, Lusungo na baadhi ya maeneo ya Mapwale ambayo yameathirika sana na mvua hizi zinazoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa pole hizo, ninaomba kutoa mchango kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hotuba aliyowasilisha Waziri Mkuu, ninapongeza pia kwa jinsi ambavyo *TARURA* wamekuwa wakifanya kazi nzuri sana, na Mheshimiwa Prof. Shemdoe, Waziri wetu wa TAMISEMI, lakini baada ya mvua hizi na maeneo mengi yameathirika na mvua hizi, hasa Jimbo langu la Kyela, kwa sababu ni Jimbo ambalo lipo ukanda wa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kipekee sana *TARURA* wapewe fedha za dharura ili kuweza kwenda kuirekebisha ile miundombinu ambayo imeharibika kwa sehemu kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majimbo yetu na hasa katika Jimbo langu, Kata za Nkokwa, Katumbasongwe, Lusungo ambazo mpaka sasa hivi baadhi ya maeneo kama daraja la Ngana - Ushirika ambapo wanafunzi wamelazimika kuahirisha kusoma eneo moja na wamehamia shule nyingine kwa sababu ya kushindwa kuvuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Ofisi ya Waziri Mkuu, ichukue jambo hili na iipe udharura wa pekee ili tuweze kujenga lile daraja la Ngana na wanafunzi wa Ushirika waweze kwenda masomoni kama ambavyo walikuwa wanaendelea na masomo kama kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu kuwa kuna mpango mkubwa wa *TARURA* kupewa fedha za dharura, lakini nilikuwa ninaiomba Serikali kuwa ichukue kipaumbele katika yale maeneo ambayo yana athari kubwa kwa wananchi ili kuweza kurudisha ile furaha ya wananchi wa maeneo husika hasa katika majimbo ambayo yameathirika na mvua hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na mvua ambazo zinaendelea kunyesha kila wakati, Jimbo letu la Kyela linakuwa inaathirika kwa ukanda wa kusini. Kuna mradi mmoja ambao kama Serikali itauwekea kipaumbele na kuanza kuutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kabisa kwamba tutaondoa kero kwa wananchi wa Jimbo la Kyela. Mradi huo ni wa *Songwe Basin* ambao uko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Ninaomba sana ule mradi wa *Songwe Basin* ambao una *components* nyingi ndani yake, ambao tukizungumza, leo utakuwa mkombozi kwa sehemu kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu kuwa Serikali ipo katika hatua za kumtafuta mkandarasi au tunamwita *transaction advisory*. Ninaomba katika ile *PPP,* tuangalie zile *components* ambazo zinaweza zikawa zinakubalika kwa watu ambao wanataka kuwekeza kwenye *PPP,* ili twende haraka, ule mradi uanze kufanya kazi kwa sababu unahusisha ukanda wa kwetu na nchi jirani ya Malawi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi ule tukiusimamia vizuri, ninaamini kabisa utakuwa ni suluhisho la mafuriko ya kata zote ambazo ziko ukanda wa Katumba Songwe na mpaka wa kati ya Malawi na Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba mradi huo upewe kipaumbele, kwa sababu sasa hivi walikuwa wanaendelea na mchakato huo. Nilikuwa ninaomba waongezewe nguvu kwa sababu mradi huo utakuwa ni ukombozi kwa Wilaya ya Kyela na wilaya nyingine nne ambazo zitakuwa zimepitiwa na mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali kupitia kwa Waziri Mkuu, na alivyofika Kyela, tulimwambia na tulimshauri kuwa mradi huo upewe kipaumbele katika miradi ambayo Serikali itatoa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa muda wetu unakimbia, ninaomba nizungumzie upande wa zao letu la kokoa. Zao letu la kokoa tunaendesha kwa Mfumo wa Stakabadhi Ghalani, lakini kupitia stakabadhi za ghala, bei imeendelea kushuka kwa jinsi ambavyo huko nje wanaendelea kupigana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali angalau waone uwezekano, kama alivyoahidi Mheshimiwa Rais katika hotuba yake na katika kampeni za uchaguzi wa mwaka huu kuwa atatujengea kiwanda cha kuongeza thamani zao la kokoa. Zao la kokoa lilifika zaidi ya shilingi 32,000 kwa kilo moja. Sasa hivi ninavyozungumza, mnada wa jana ulikuwa shilingi 7,020. Hivyo, wananchi wa Kyela wamekuwa wakiathirika sana kwa kushuka kwa bei ya zao hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwa kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, waone uharaka wa kujenga kiwanda ndani ya Jimbo la Kyela ili zile tani 9,000 mpaka 10,000 tunazozalisha za zao la kokoa ziongezewe thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini, kwa kuongezewa thamani kule, kutafanya kuwa wakati pale ambapo bei zitakuwa zinashuka katika soko la dunia, zao liweze kuendelea kupatikana na kuwasaidia wananchi wa Kyela kuendelea kupata bei nzuri ya zao lile. Hii ni kwa sababu kwa uchumi na biashara kubwa, sisi Kyela zao la kokoa ndilo dhahabu yetu na ndiyo uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika baadhi ya maeneo sasa hivi Tanzania yameanza kulima zao lile kwa sababu limekuwa likiingiza fedha nyingi za kigeni, hasa kwa wakati ule ambapo bei inakuwa juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba jambo hili lipewe kipaumbele kikubwa ili angalau kuweza kuanza ujenzi. Maeneo yapo tayari ambayo ni kwa ajili ya uwekezaji wa kiwanda cha zao la kokoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninakushukuru sana. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Baraka Ulimboka. Nilimtaja Mheshimiwa Silvery Salvatory, Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, ajiandae.

MHE. SILVERY L. SALVATORY: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hotuba ya bajeti ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai na kwa kunijalia afya njema kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu asubuhi hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, niwashukuru wananchi wa Jimbo la Misungwi kwa kuniamini na kunichagua kuwa mwakilishi wao. Ninaomba niwaahidi utumishi uliotuka, na sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikishukuru Chama changu cha Mapinduzi chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kunidhamini kuweza kupeperusha bendera ya Chama cha Mapinduzi kwenye Uchaguzi Mkuu na hatimaye kuwa Mbuge wa Jimbo la Misungwi. Aidha, ninawashukuru wananchi, kila mmoja kwa kadiri alivyohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa ninawashukuru wazazi wangu; Marehemu baba yangu Mzee Salvatory, na Marehemu mama yangu Letisia. Mwenyezi Mungu awape pumziko la milele. Ninaamini kwa imani yangu huko waliko wananiombea, kwani mafundisho ya imani yangu yananiambia mwili pekee ndio unaokufa, lakini roho zipo na wanaona kinachoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, kwa vile ni mara yangu ya kwanza kuzungumza, lakini nimekuwemo humu Bungeni tangu Mheshimiwa Rais alipozindua Bunge la Kumi na Tatu Tarehe 14 Novemba. Kwa hiyo, nitapita kwenye nyaraka mbalimbali nikianza na hotuba ya Mheshimiwa Rais, Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka 2026/2027 na Dira ya Taifa ya 2050 pamoja na hotuba ya bajeti ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachangiaji waliozungumza huko nyuma walisisitiza kwamba mawasilisho ya Serikali yamenyooka na yametulia na yanajieleza, shida ni utekelezaji. Kwa muda mfupi ambao nimekuwa hapa, nimefanya utafiti mdogo nikatafuta Ma-*CEO*

wanne. Ma-*CEO* wawili wanapatikana kwenye nyumba hii, ma-*CEO* wawili wako nje ya jumba hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ma-*CEO* wawili ninaomba niwapongeze, maana kupitia hizi nyaraka mbalimbali ninaona wanaenda kwa vitendo. Mmojawapo, sisi wote Wabunge ni mashahidi, tukiamka asubuhi tunakutana na *message* inatuelekeza leo tutaanza na nini na tutamaliza na nini? Ninaomba nipongeze sana taasisi ya Bunge, kwani tangu niingie humu nime-*appreciate* huduma zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *CEO* wa pili, niipongeze Wizara ya Nishati. Siku chache nikiwa hapa Bungeni nilipata taarifa ninambiwa nini kinaendelea kwenye jimbo langu kuhusiana na suala la nishati, ambapo kwenye Jimbo langu la Misungwi nilipewa vitongoji 121 na kufanya tubakiwe na vitongoji 280 pekee kati ya vitongoji 724. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Wabunge wenzangu, kama Watanzania watafanya kazi kwa mifano hiyo miwili niliyoitolea, kuanzia hotuba ya Mheshimiwa Rais, Mpango wa Maendeleo wa Taifa pamoja na hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu vinaweza vikatekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kushangaza, ndani ya huo muda nimeenda mahali nikawa ninatafuta huduma. Kutolewa tu barua, na wakijua mimi ni Mbunge na ni mwenzao, imechukua mwezi mmoja, na hiyo taarifa nilimpa Mheshimiwa Prof. Shemdoe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haikuwa nia yangu kuyazungumza hapa. Nikaenda kwa ma-*CEO* wengine ambao wana *chain* ambayo inaungana, nikahitaji huduma ambayo ilikuwa inahusu pia nilipe kodi ya Serikali, lakini tunavyoongea leo ni miezi minne utekelezaji wake haupo. Maana yake ni nini? Kama vitu tunavyoviongea humu haviwezi vikatekelezwa kwa vitendo, hatuwezi tukatoboa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nipongeze hotuba zote hizi tatu kama ambavyo nimeziainisha, kwa maana ya kwamba hizi

hotuba zinasomana kuanzia hotuba ya Mheshimiwa Rais, na hotuba ya mipango hadi hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba nijielekeze kwenye hotuba ya Waziri Mkuu. Kwenye ukurasa wa 176 hotuba ya Waziri Mkuu inaelekeza kwamba tunaenda kusambaza maji vijijini kwenye vijiji 225 ambapo shilingi bilioni 449 zinaenda kutumika. Ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, na kwa maelezo yangu niliyoyatoa kwa namna ambavyo hatuwajibiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninao mradi wa Ilujamate – Buhingo ambao una vijiji 16. Chanzo cha maji kilizinduliwa mwaka 2009 na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Awamu ya Nne. Leo ni miaka 17 maji hayajafika kwenye vijiji vya jirani ambavyo viko karibu na chanzo, haizidi kilometa tano mpaka 20, ilhali maji yanapatikana kilometa 600 kutoka kwenye chanzo. Hiyo siyo haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mmoja wetu aliyepewa dhamana kwa nafasi yake aweze kutekeleza wajibu wake, kwani mwenye macho haambiwi tazama, lakini pia mwenye akili hawezi kuambiwa jiongoze. Hapo kuna dosari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaomba kupitia hotuba ya Waziri Mkuu, tunao mradi wa maji wa Ukiliguru unaopita kwenye vijiji 19 vya Bulemeji, Ngudama, Nyang'holongo, Nyamle, Usagara, Idetemya, Nyangomango, Ntende, Koromije, Ibondo ya A na B Mamaye hadi Bugomba. Vijiji hivi viko *connected* na chanzo cha maji, hakihitaji hata usumbufu wa aina yoyote. Kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu tunaomba miradi hii sisi Wana-Misungwi ikaweze kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti ...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Silvery Salvatory, kengele ya pili imeshalia.

MHE. SILVERY L. SALVATORY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba dakika moja. Tunayo miradi ya kimkakati ambayo imetajwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kutokana na jiografia ya Mwanza, tunaomba basi upanuzi wa barabara ya njia nne kutoka Usagara kwenda Mjini ukaweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia barabara inayotoka Kaluluma kupitia Mwasonge hadi Buhongwa yenye urefu kilometa 6.6 nayo ijengwe kwa kiwango cha lami, bila kusahau njia inayotoka kwenye *Dry Port,* Fella inayopita Ngeleka - Fella hadi Nyashishi nayo ijengwe kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. SILVERY L. SALVATORY: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana, ninakushukuru Mheshimiwa Silvery Salvatory. Nilimtaja Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, Mheshimiwa Zena Maulidi Katambo ajiandae.

MHE. ZUENA A. BUSHIRI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kutufikisha sote siku hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaifanya katika hali ya kulijenga Taifa hili la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Waziri Mkuu kwa kazi kubwa ambayo anaifanya ya kumsaidia Rais na ziara ambayo ameifanya katika halmashauri zetu zote ambayo imeleta tija kubwa sana, bila kuwasahau Mawaziri wote na Manaibu Waziri kwa kazi kubwa ambazo wanazifanya za kumsaidia Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo katika hotuba ya Waziri Mkuu nitachangia mambo matatu kama muda utaniruhusu. Nitaanza na afya, nitakuja na shilingi bilioni 200 kwa vijana na nitakuja na mikopo ya 10% ya halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na afya. Hakuna Taifa bila afya. Ili Taifa liweze kusonga mbele kwa kazi zake zote, ni lazima wananchi wake wawe na afya ya kutosha. Tumemwona Mheshimiwa Rais kazi aliyoifanya katika sekta ya afya, kuanzia ngazi ya zahanati hadi hospitali za kikanda. Hii inaonesha wazi kwamba Mheshimiwa Rais anawajali sana na anazijali sana afya za Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 64 imeeleza, kwamba mwaka 2024 tulikuwa na wastani wa 80% katika vituo vya kutolea huduma. Hadi Februari, 2026 tuna wastani wa 89%. Hii ni hatua kubwa sana. Watanzania tumpongeze sana Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais amehakikisha tiba za kibingwa na bingwa bobezi zinapatikana hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani tulikuwa tunasafiri kwenda nchi za nje, hasa India, kwenda kutafuta matibabu na vipimo, lakini kwa sasa hivi Mheshimiwa Rais amejitahidi sana. Kwa mfano, kipimo cha saratani aina ya *Pet/CT scan,* bei yake ni shilingi bilioni kumi na nane na pointi. Mheshimiwa Rais ameguswa na shida za Watanzania ambao wanaumwa ugonjwa huu wa saratani, akahakikisha kipimo hiki anakileta katika nchi yetu, ambacho kimesaidia sana Watanzania. Tumpongezeni sana Mheshimiwa Rais kwa hatua hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna huduma ya upandikizaji wa figo. Mwanzo ilikuwa inapatikana katika nchi za nje. Tulikuwa tunaenda Nairobi na nchi nyingine za nje kupata huduma hii, lakini kwa sasa hivi huduma hii iko Muhimbili, na hapo Benjamini Mkapa. Ni hatua kubwa sana. Watanzania tumpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayofanya katika sekta hii ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii imefungua njia mpaka nchi za nje sasa zinakuja kupata matibabu nchini kwetu, ikiwemo nchi za

Comoro, Congo, Malawi Zambia, Burundi na nchi nyingine. Ni hatua kubwa sana kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali, ninaiomba sana Serikali iongeze ajira ya watumishi katika kada hii ya afya ili iendane na vituo vya kutolea huduma, iweze kuwasaidia. Pia ninaomba mfumo wa tiba mtandao ushuke kutoka katika hospitali za rufaa na mikoa hadi katika hospitali za wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili, utakuja katika shilingi bilioni 200 za vijana. Tarehe 5 Februari, 2026 Serikali imetoa shilingi bilioni 200 kwa ajili ya mikopo kwa vijana. Vijana wetu wametafutiwa kila njia ya kujikwamua kiuchumi. Ukiingia katika mikopo ya halmashauri ya 10%, vijana wapo. Hata hivyo, Mheshimiwa Rais akaona haitoshi, atakawatafutia shilingi bilioni 200 ili kuwawezesha kiuchumi waweze kufanya biashara zao. Hongera sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe vijana wakiwemo vijana wangu wa Mkoa wa Kilimanjaro wachangamkie sana fursa hii. Kazi aliyoifanya Mheshimiwa Rais ya kutafuta hizi fedha ni sababu ya kuhakikisha kwamba kila kijana anajikwamua kiuchumi. Watumie fursa hii ili walete maendeleo katika familia zao na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu katika fedha hizi, tumeona changamoto iliyokuwepo mwanzo katika fedha za 10% za halmashauri. Utaratibu ule wa mwanzo haukuwa mzuri mpaka Mheshimiwa Rais alifika mahali akaona abadilishe utaratibu ukaja utaratibu wa pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa fedha hizi shilingi bilioni 200 ninaiomba Serikali isimamie na iratibu utoaji wa fedha hizi ili zikatumike vizuri kwa lengo lile ambalo limekusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije sasa katika 10% za halmashauri, wenzangu wameongea, zipo changamoto. Changamoto kubwa ambayo inaonekana ni ujazaji wa lile dodoso.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dodoso lile ni wachache ambao wanaweza kulitumia. Ukizingatia kuwa asilimia kubwa ya walengwa wa mikopo hii ni wale akina mama wanaoishi vijijini ambao hawawezi hata kufanya biashara kubwa, lakini utakuta Maafisa Maendeleo ya Jamii wanawatuma na kuwaambia waende wakajaze dodoso, kitu ambacho hawawezi. Matokeo yake wanaondoka wanaenda kwenye *stationery* wanatozwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanamke wa kijijini wakati mwingine hata fedha ya kununua mchicha hana, ukimwambia habari ya kwenda kulipa *stationery* ili apate mwongozo wa kujaziwa lile dodoso kwake ni msalaba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali yangu sikivu isimamie kwa makini suala hili na kuwatoa Maafisa Watendaji wa kata maofisini washuke chini wakiiga mfano wa Waziri Mkuu alichokifanya juzi. Waende wakawaone wananchi makundi yote, vijana, walemavu na wakina mama wawasaidie ili waweze kupata fedha hizi kwa ajili ya kufanya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amegusa sana mikopo hasa kwa vijana. Sasa kama sisi Serikali tukiisimamia vizuri, hawa vijana wetu ambao wanazunguka mitaani kila siku hawana kazi za kufanya, wakitumia mikopo hii watajikwamua kiuchumi na hatimaye Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri. Nilimtaja Mheshimiwa Zena Maulidi Katambo, Mheshimiwa Sheila Edward Lukuba na Mheshimiwa Dkt. Catherine Joachim wajiandae.

MHE. ZENA M. KATAMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia fursa na mimi kuchangia leo katika hotuba ya Waziri Mkuu. Kwa kuwa leo ni mara yangu ya kwanza, ninaomba nitumie fursa hii kuwashukuru wanawake wa Mkoa wa Lindi ambao wameniwezesha kunifikisha hapa leo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatumia jukwaa hili kuwaeleza kwamba nitawapa uwakilishi ambao umetukuka na nipo tayari kuwatumikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, kwa dhati ya moyo wangu ninampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya kwa kujitolea kwake kwa hali na mali kuhakikisha kwamba nchi yetu inapata maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee, ninamshukuru Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, tumemwona katika kipindi ambacho yupo kwenye nafasi hii amezunguka katika maeneo mbalimbali nchini na kufanya ziara ambapo katika ziara hizo amefanya shughuli mbalimbali na kutatua kero mbalimbali za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumtia moyo Waziri Mkuu, nimweleze kwamba wananchi tunafurahishwa na kasi yake ya utendaji kazi na kwamba aendelee hivyo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, mchango wangu kwa siku ya leo katika Wizara hii ninauelekeza kwenye barabara. Mkoa wa Lindi tunazo changamoto kubwa sana za miundombinu ya barabara. Barabara hizi changamoto inaanzia barabara kuu ambayo inaunganisha Mkoa wa Lindi na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika barabara hii tumepitia changamoto mbalimbali ambapo katika msimu wa mvua wa mwaka 2024 ambao nchi yetu tulikumbwa na Kimbunga Hidaya, Mkoa wa Lindi, barabara hii iliathirika kwa kiasi kikubwa na kuharibika kwa madaraja, na pia sehemu kubwa ya barabara kuharibika vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali hiyo, ninaipongeza Serikali kwa jitihada zake ambazo imefanya kwa kurekebisha yale madaraja makubwa ambayo yalikuwa yanaathiri matumizi ya barabara ile ambapo kwa kipindi cha mwaka 2025 wananchi wa Mkoa wa Lindi ni

mashahidi kwamba baadhi ya nyakati tulilazimika kukaa kusubiri kungojea maji yapungue ili tuendelee na safari zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali imemaliza changamoto ile ya upande wa madaraja na kwamba sasa angalau tuna uhakika wa kusafiri moja kwa moja kutoka Dar es Salaam mpaka Lindi. Hata hivyo, tunayo changamoto nyingine katika barabara hiyo ambapo ile athari ya mvua iliharibu maeneo mengi ambapo barabara ile ina mashimo mengi, kwa kweli haipitiki vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, katika changamoto hii Serikali imejitahidi kuziba viraka katika barabara ile ili angalau wananchi waendelee kuitumia. Kutokana na uharibifu ule mkubwa, ninaiomba Serikali, sisi wananchi wa Mkoa wa Lindi suluhisho la kudumu tunaomba tujengewe barabara mpya ili kusudi iendane na mahitaji ya sasa tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba barabara hii mpya kwa sababu tunafahamu kwamba Mkoa wa Lindi kwa sasa kuna miradi mbalimbali ya kimkakati ambayo inafanyika. Miongoni mwa miradi hiyo ni pamoja na bandari ya uvuvi iliyopo Wilayani Kilwa. Bandari hii Serikali imewekeza shilingi bilioni 280.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uwekezaji huo, tunaiomba Serikali itutengenezee hii barabara kuu ili jitihada ambazo zimetumika kuwekeza kwenye mradi ule ziendane na miundombinu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, tunazo changamoto za barabara za ndani ya mkoa. Mkoa wa Lindi hauna wilaya ambazo zimeunganishwa kwa lami kati ya wilaya na wilaya. Hivi hapa tunavyozungumza, wananchi wa Wilaya ya Liwale ambao wanapitia barabara ya Nangurukuru kwenda Dar es Salaam hawawezi kusafiri siku ya leo, tangu jana barabara zimeharibiwa na mvua kubwa ambazo zinaendelea kunyesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Wilaya ya Nachingwea, wananchi wa Kilimalondo - Mbondo, wananchi wa Kilimalondo - Kiegei - Namapwia - *Nero Mission* hawawezi kusafiri kati ya maeneo hayo kwa

sababu mvua hizi zinazoendelea zimekata madaraja katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Wilaya ya Kilwa tunazo kata za Kandawale, Njinjo, Kipatimu, Kibata ambapo katika kata hizi wananchi hawawezi kuingia wala kutoka nje ya maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Wilaya ya Ruangwa tunazo changamoto katika kata ya Matambalale, Chunyu, Nambilanje na Mandawa. Kwa ujumla tunaomba Serikali itusaidie kupitia *TARURA* kujenga madaraja na kwa awamu ya kwanza ituletee madaraja katika barabara hizi kwa sababu kiujumla hizi changamoto zimekuwa ni zile ambazo zinaendelea. Hizi changamoto ni zile ambazo zinatokea kila mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika harakati za kutibu tatizo hili, tunaomba Serikali itujengee madaraja ili wananchi waendelee na shughuli zao za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni umeme. Utakubaliana na mimi, Mkoa wa Lindi huenda ndiyo mkoa pekee au labda imebaki mikoa miwili mitatu ambayo bado haijaunganishwa kwenye gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kutokuunganishwa na gridi ya Taifa mkoa wetu una changamoto kubwa ya ukosefu wa umeme wa uhakika. Kwa Mkoa wa Lindi, umeme kukatika mara 10 mpaka 20 kwa siku ni jambo la kawaida. Hali hii inatuathiri sana wananchi wa Mkoa wa Lindi, lakini pia tunapata athari za kiuchumi ambapo tunakosa wawekezaji ambao wapo *serious* kwa ajili ya kufanya miradi mbalimbali ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali, kwa kuwa sasa hivi nchi yetu tunazalisha umeme zaidi ya mahitaji yetu, ninaiomba Serikali ituunganishe na sisi wananchi wa Mkoa wa Lindi ili kusudi na sisi tuweze kunufaika na hii keki ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, nimalizie kwa kuipongeza Serikali katika mradi wa *LNG*. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sasa hivi ipo kwenye hatua za mwisho za kusaini makubaliano ya utekelezaji wa uzalishaji wa gesi ya asilia kupitia mradi wa *LNG* Mkoani Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu una thamani ya shilingi trilioni 100. Huu ni mradi mkubwa kuliko mradi wowote ambao nchi yetu ya Tanzania imewahi kuutekeleza. Mradi huu unasubiriwa sana na wananchi wa Mkoa wa Lindi, kwa sababu hii ilikuwa ni ahadi tangu Serikali ya Awamu ya Nne; ilituahidi kutekeleza mradi huu, lakini hatukufanikiwa, Serikali ya Awamu ya Tano na mpaka sasa ya Sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wananchi wa Mkoa wa Lindi kwa kweli tumeusubiri sana mradi huu, tunatamani na tunaiomba sana Serikali iharakishe zoezi la usajili na kusaini *documents* za makubaliano ili kusudi mradi uanze kazi, na pia uweze kuchangia kwenye Taifa na dunia kwa ujumla kwa sababu unalenga kuuza gesi ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Zena Maulidi Katambo, kwa kutumia muda wako vizuri. Nilimtaja Mheshimiwa Sheila Edward Lukuba, Mheshimiwa Dkt. Catherine Joachim na Mheshimiwa Mohamed Mussa Utaly, wajiandae.

MHE. SHEILA E. LUKUBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninapenda kumshukuru Mungu Mwingi wa Rehema kwa kutujalia afya njema nami leo nimeweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kumshukuru kwa dhati ya moyo wangu Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi na vikao vyake vyote anavyoviongoza kwa kuniteua mimi na hatimaye nikachaguliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninasema, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru wananchi wa Mkoa wa Morogoro hususan wanawake wa Mkoa wa Morogoro kwa kumchagua Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kura nyingi za kishindo na mimi kunituma Bungeni kuwa mwakilishi wao. Ninawaahidi sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, gwiji wa mapinduzi ya uchumi wa kilimo Adam Kighoma Malima. Huyu Mkuu wa Mkoa anafanya kazi usiku na mchana bila kuchoka kumsaidia Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa aliyoifanya na anaendelea kufanya makubwa chini ya uongozi wake, miradi mingi imetekelezwa.

Mama piga kazi, wewe ni nguvu ya wanawake, tumaini la Taifa na chachu ya maendeleo endelevu. Mama ninakupa mstari kwenye Biblia ambao utakutia nguvu. Isaya 41:10, "Usiogope, maana mimi ni pamoja nawe, usifadhaike maana mimi ni Mungu wako, nitakutia nguvu nami nitakusaidia." Mheshimiwa Rais ninakutia nguvu, sisi ni jeshi kubwa. Tutakulinda chini ya Mwenyekiti wetu mama Marry Chatanda. Piga kazi Mama tupo pamoja na wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia nimpongeze sana Waziri Mkuu, ndugu yangu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kwa kuonesha mfano wa kuigwa wa kuwafuata wananchi kwenye maeneo yao na kuwasikiliza kero zao na kuzipatia majawabu hapo kwa hapo. Hongera sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi wanaomsaidia Mheshimiwa Rais, hasa wale wateule, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameonesha njia. Njia hii itawafanya wananchi kuendelea kuwaamini viongozi wao na

Serikali kwa ujumla, pia itawasaidia wananchi kupata suluhisho sahihi la matatizo yao, na pia itasaidia kusikiliza kero mara kwa mara na kupunguza migogoro hiyo. Ameonesha mfano wa kuigwa, kwa hiyo, nanyi Wizara ninawaomba msibaki nyuma, fuateni nyayo zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaungana na Wabunge wenzangu wa Mkoa wa Morogoro ambao wameshachangia. Sisi Mkoa wa Morogoro kipaumbele chetu cha kwanza kwa sasa ni barabara, hasa ukizingatia Morogoro ni ghala la chakula na sasa tumepata ghala la pili, Bwawa la Kidunda ambalo litahudumia Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na maeneo ya jirani na mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ninaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, Morogoro iangaliwe kwa jicho la kipekee kuhusu suala zima la barabara. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alikuja na falsafa zake nne za *4R*, lakini Waziri wa Maendeleo ya Jamii pia naye ana kauli mbiu yake, "kaza kazawa" (kasi zaidi, karibu zaidi na wananchi).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami leo ninakuja na kaulimbiu yangu ya 4K kwenye suala zima la mikopo. 'K' ya kwanza, ni kutenga fedha za mikopo kwenye bajeti. Kuhakikisha halmashauri zetu zinatenga fedha za mikopo kama ilivyoelekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, 'K' nyingine ni kutoa mikopo yenye tija kwa walengwa. 'K' nyingine ni kufuatilia wakopaji ili kufahamu maendeleo yao na pia waweze kusaidiwa kupata masoko ndani na nje ya nchi. 'K' nyingine ni kuhakikisha kurejeshwa kwa mikopo hiyo kwani mikopo hiyo ni *revolving fund*. Ameonesha mfano wa kuigwa, kwa hiyo, nanyi Wizara ninawaomba msibaki nyuma, fuateni nyayo zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuchangia Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu na Watu wenye ulemavu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama ulivyoshuhudia katika ziara zako, matatizo mengi yaliyowasilishwa kwako na wananchi ni masuala ya ustawi wa jamii. Mfano migogoro ya ndoa, mirathi, matunzo ya watoto na vitendo vya ukatili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nimefanya utafiti wangu usio rasmi na nimegundua kwamba kada hii ya ustawi wa jamii ina watumishi takribani 2,238, lakini pia ina upungufu wa watumishi takribani 18,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali yangu Tukufu iweze kuiangalia kada hii ya ustawi wa jamii waweze kuongeza na wakishaongeza, watu hawa watakwenda mpaka kwenye kata na vijiji kufanya kazi na ustawi wa jamii. Pia watatusaidia katika suala zima la mmomonyoko wa maadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilhali tumeshuhudia kwenye maafa mbalimbali Maafisa Ustawi wa Jamii hawa wakitumika, mfano mafuriko ya Hanang', janga la Kariakoo na mafuriko ya Kibiti, kada hii ni muhimu sana kwa makundi maalum ikiwemo watoto walio katika mazingira magumu, wazee na watu wenye ulemavu. Wote hawa wanahudumiwa na Maafisa Ustawi wa Jamii katika ngazi mbalimbali ikiwemo Serikali za Mitaa, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wizara ya Afya na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosekana kwa mamlaka moja inayosimamia huduma za ustawi wa jamii kuanzia ngazi ya juu hadi ya chini, kunapunguza ufanisi wa huduma hizo. Je, Serikali sasa haioni umuhimu wa kuwa na Idara ya Ustawi wa Jamii katika ngazi za mikoa na mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuweka vipaumbele vyao na bajeti zinazotekelezeka ili kuimarisha huduma za ustawi wa jamii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kwa sasa hivi wanategemea bajeti ya *DMO* ambaye naye anazidiwa anakuwa na vipaumbele vyake. Hivyo, ninaiomba Serikali ione umuhimu wa kuanzisha Idara ya Maafisa Ustawi wa Jamii.

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. SHEILA E. LUKUBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba dakika moja nimalizie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Maafisa Ustawi wa Jamii wanafanya kazi zao chini ya Ofisi ya Mganga Mkuu. Wengi hawana ofisi na wanashughulikia masuala mbalimbali na kusikiliza masuala nyeti ya kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba basi, kwenye halmashauri zetu Maafisa Ustawi wa Jamii hawa wapewe ofisi ili waweze kufanya kazi zao vyema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Sheila Edward Lukuba. Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Catherine Joachim, Mheshimiwa Mohamed Mussa Utaly, na Mheshimiwa Juma Ramadhani Mustafa wajiandae.

MHE. DKT. CATHERINE C. JOACHIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kutufikisha sote siku ya leo. Kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuchangia katika Bunge Tukufu la Kumi na Tatu, nianze kwa heshima na unyenyekevu kumshukuru Mwenyezi Mungu, na pia nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuridhia nikaweza kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Viti Maalum Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninawashukuru Wajumbe wa Mkutano Mkuu Maalum wa Wazazi kwa kuweza kunichagua. Ninaomba kutumia fursa hii kuwaahidi uadilifu mkubwa, usikivu na ushirikiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Wabunge wengine kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri, lakini pia ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa mafanikio makubwa ya Serikali kwa mwaka huu wa fedha. Pia ninampongeza kwa kuweza kutoa hotuba ambayo imesheheni vipaumbele vya Serikali vinavyokwenda kutekelezwa tunapokwenda kuanza utekelezaji wa dira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu katika hoja hii utajikita katika ukurasa wa 66 hadi 68 wa hotuba hiyo ambayo imejadili au imewasilishwa masuala yanayohusu lishe na mapambano dhidi ya *VVU* na UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa lishe, nianze kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu, kwa kuendelea kuwa kinara wa lishe. Tumemwona Mheshimiwa Rais kuanzia mwaka 2017 ameweka msukumo mkubwa katika masuala ya lishe, lakini kikubwa zaidi msukumo wake umekuwa katika masuala ya kutatua changamoto kubwa ya udumavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ameendelea kuweka mikataba na Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na kuweka viashiria mbalimbali ambapo tulipomsikiliza Mheshimiwa Waziri Mkuu, imeonekana kwamba tatizo la udumavu limepungua kutoka 34% mwaka 2015/2016 hadi 30% mwaka 2022. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Mheshimiwa Rais wetu, ametambulika kama kinara wa masuala ya lishe katika Bara la Afrika, na pia ni miongoni mwa Marais sita waliopo katika *Presidential Dialog Nutrition*. Jukwaa hili nimeleta lishe kama ajenda kuu ya maendeleo ya rasilimali watu na uchumi Barani Afrika. Ushiriki huu unaipa nchi yetu nafasi kubwa ya uongozi unaosukuma mabadiliko ya kisera na utekelezaji katika lishe katika ngazi ya kikanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwani sote tunafahamu uratibu wa kisekta ya lishe unafanyika katika ofisi yake vilevile, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambaye ndiye msimamizi mkuu wa masuala ya lishe katika utekelezaji wa ngazi ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Wamefanya kazi hii ya usimamizi kwa mafanikio makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio ambayo yamepatikana. Tunaona kwamba Tanzania ina watoto takribani 3,400,000 ambao bado wana changamoto ya udumavu. Hii ina

maana kwamba katika kila watoto watatu tunaowaona, mtoto mmoja ana changamoto ya udumavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, bila kushughulikia changamoto za lishe kwa uzito unaostahili, tunaweza tusilifikie lengo la Taifa, lenye uchumi shindani unaotegemea rasilimali watu yenye afya, ujuzi na uwezo wa kushiriki katika uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kwa kuwa changamoto hii iko na watoto, inakwenda kuathiri watoto hao ambao wana udumavu, watashindwa kufuatilia masomo yao vizuri. Pia tafiti zinaonyesha, watoto ambao wamekuwa na hali ya udumavu, mchango wao katika uzalishaji unapungua kwa 20%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ninapenda kushauri maeneo ya kisera ambayo yamewekewa msukumo mkubwa. Tunafahamu kwamba halmashauri inatakiwa kutenda shilingi 1,000/= kwa kila mtoto kwenye halmashauri husika. Hivyo, nilikuwa nashauri takwa hili liwe la kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, changamoto ya udumavu iko katika halmashauri ambazo zina changamoto, zinazalisha chakula kwa kiwango kikubwa. Hivyo, nilikuwa nashauri, uzalishaji wa chakula ufungamanishwe na masuala ya lishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, nilikuwa nashauri tafiti za masuala ya lishe zitengewe fedha, kwani mila na desturi katika mikoa zinatofautiana. Takwimu hizi zitaweza kuelezea nini mikoa ifanye ili kutatua changamoto za udumavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka, nitakwenda kujielekeza katika mapambano dhidi ya *VVU* na UKIMWI. Nianze kuipongeza Serikali kwa kuendelea kutoa huduma bure kwa watu wote ambao wana maambukizi ya *VVU* na UKIMWI, kuanzia mwaka 1983 janga hili lilipogundulika hapa nchini. Vilevile, ninaipongeze Serikali kwa kuweza kuanzisha tozo kwa ajili ya kugharamia gharama za *UKIMWI. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tulisikia mwaka 2026 kwa mara ya kwanza, Serikali imeanzisha tozo ili kuweza kukabiliana na changamoto ya kupungua kwa fedha. Hivyo, ninaipongeza sana Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwani suala hili limekuwa likifanyiwa kazi kwa takribani miaka kumi iliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, pamoja na mafanikio ya kupunguza maambukizi mapya na vifo vitokanavyo na UKIMWI, bado tuna changamoto kubwa ya maambukizi mapya kwa vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utafiti uliofanyika mwaka 2022 maambuki ya UKIMWI kwa mwaka yamekuwa kwa watu 56,000, lakini tukiangalia katika taarifa ile 70% ya watu wanaopata maambukizi mapya ni vijana wa kike. Hivyo, kundi hili liko katika hatari ya kutoweza kuchangia katika shughuli za uzalishaji mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine kikubwa ambacho tunakiona ni gharama kubwa za dawa. Mgonjwa anayetumia dawa za UKIMWI, gharama yake ni shilingi 550,000 kwa mwaka. Hivyo, ukiangalia kwa sasa hivi, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ilionesha tuna watu takribani 1,500,000 wanaohitaji dawa hizi za Virusi vya UKIMWI. Hivyo, kama nchi tunahitaji zaidi ya shilingi bilioni 800 kugharamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, nilikuwa nina ushauri wa kisera katika maeneo makubwa matatu. Cha kwanza, ni kuongeza vyanzo ili tuweze kujitegemea zaidi; cha pili, ni kuweza kuwa na mkakati maalumu wa kinga ili kuweza kuzuia vijana wetu wa kike kupata UKIMWI; cha tatu, ni kuweza kufungamanisha huduma za UKIMWI katika bango kitita la mafao la Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ninakushukuru Mheshimiwa Dkt. Catherine Joachim, tunaendelea na Mheshimiwa Mohamed Mussa Utaly, Mheshimiwa Juma Mustafa Kawamba na Mheshimiwa Twaha Said Mwakioja, wajiandae.

MHE. MOHAMED M. UTALY: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii muhimu ili niweze kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema mwenye kurehemu kwa kunijalia afya njema na kuwa na uwezo wa kusimama katika Bunge hili kwa mara ya kwanza kutoa mchango wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hii ni mara yangu ya kwanza, naomba nitumie fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na vikao vyote vilivyohusika katika kupitisha jina langu ili niweze kuwa mgombea wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninachukua fursa hii kuwashukuru sana wapigakura wa Jimbo la Lindi Mjini, ambao wamenipigia kura nyingi za kutosha, na hapa ninawaahidi kwamba nitatumia uwezo wangu wote na nguvu zangu zote kuwatumikia ili kukidhi haja ya matarajio yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie fursa hii kumpongeza Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi kubwa anayoifanya katika nchi hii. Ninampongeza kwa namna ambavyo amepokea maono na mwongozo wa Mwenyezi Mungu, kuweza kumteua Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kuwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, tunamwona namna ambavyo anafanya kazi zake. Ukimwangalia katika utendaji wake wa kazi, ukimwangalia katika ziara zake, unaona ni namna gani matatizo ya wananchi wa Tanzania yanamshughulisha, na yeye anayashughulikia ipasavyo. Hongera sana kwa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yake Waziri Mkuu, pamoja na mambo mengine, ameeleza namna ambavyo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ndani ya siku 100 ametekeleza

ahadi zake zote alizoahidi. Hii ni kuonesha ni namna gani Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni mtekelezaji wa ahadi tena kwa wakati. Hili linatupa matumaini kwamba ilani yetu hii ya Chama Cha Mapinduzi, itatekelezwa ipasavyo. Tunampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba nichangie hotuba hii kwa kuyaangazia matatizo au changamoto zilizopo katika Jimbo langu la Lindi. Kwanza tunamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuweza kutupatia mambo yafuatayo: ujenzi wa shule mpya za kisasa, ujenzi wa hospitali ya wilaya, ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Ndaki ya Kilimo Tawi la Lindi, na ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wana-Lindi tunamshukuru Rais kwa miradi ambayo sasa hivi inaendelea katika mji wetu. Miradi ambayo inaendelea sasa hivi ni suala la ujenzi wa soko la kisasa, ujenzi wa stendi ya mabasi ya kisasa na ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii yote ni miradi ambayo ipo chini ya *TACTICS* yenye thamani ya shilingi bilioni 19.061. Pamoja na nia njema ya Mheshimiwa Rais, utekelezaji wa miradi hii unasuasua mno. Hili, pamoja na mambo mengine ni utaratibu uliotumika kumpata mkandarasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkandarasi aliingia mkataba tarehe 5 Februari, 2025. Mkataba huu ni wa kutekeleza mradi kwa muda wa miezi 15 na kulipwa malipo yake ya awali shilingi bilioni 2.8 ambayo ni sawa na 15% ya thamani ya mkataba. Miezi mitatu baadaye tarehe 7 Novemba ndipo mhandisi mshauri ambaye moja ya majukumu yake ni kufanya *project review* alisaini mkataba, lakini mpaka sasa, mradi huu utekelezaji wake ni 15% wakati muda uliotumika ni 60%. Tunaomba TAMISEMI wamhimize mkandarasi huyu ili kuweza kutekeleza mradi huu kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la pili, ambalo ningependa kuelezea ni ujenzi wa Barabara ya Mtange, Kineng'ene hadi Kibaoni. Barabara hii imekuwa ni barabara ambayo ipo kwenye

ilani katika vipindi vyote. Mwaka 2022 ilijengwa meta 1,000, mwaka wa fedha 2023/2024 ilijengwa meta 600.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla, barabara hii kwa muda wa miaka miwili imejengwa kilometa 2.3. Hivyo, kama *trend* ya ujenzi wa barabara itakuwa hivi, maana yake barabara hii ya kilometa 19 itakuwa inajengwa kwa muda wa miaka 25. Jambo ambalo ukiangalia, hata huku kunakojengwa mwanzoni kutakuwa kumeshaharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninawasihi, Mheshimiwa Waziri Mkuu, na Ofisi ya *TAMISEMI,* barabara hii iongezewe kasi ili ijengwe. Barabara hii imeshapewa majina chungu mzima. Kuna eneo ambalo ni bovu kuliko kawaida wanachi wamelipa jina kwamba ni *Mashimo 40,* eneo hilo. Kuna eneo ambalo limesababisha ajali nyingi sana, wananchi wa Lindi wameita eneo hilo *Kadamba Ulumuke* ambayo maana yake kwa Kiswahili, Kanyaga uvunjike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana eneo hili liweze kurekebishwa, barabara hii iweze kupitika kila mwaka na sasa iwe ni mara ya mwisho kuoneka katika ilani, iweze kuwa imekamilika, kwa sababu ni muda mrefu sasa tunaomba barabara hii ijengwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo ningependa kuzungumzia ni suala la afya. Tunalo eneo katika Mji wa Lindi, la Kata ya Kitumbikwela. Eneo hili liko ng'ambo ya barabara. Ili mwananchi wa eneo hili aweze kupata huduma za afya, analazimika kuvuka ng'ambo ya bahari kuja mjini ili aweze kupata huduma za afya, kule hakuna kituo cha afya. Mwaka 2024, kule kulijengwa msingi wa kituo cha afya, lakini tangu wakati huo hakuna kilichoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee na kwa hali waliyokuwanayo watu hawa ambao huduma zao za afya zinawalazimisha wapande pantoni ambayo inafanya kazi kuanzia saa 12.00 asubuhi mpaka saa 12.00 jioni. Tunaomba Serikali ione umuhimu wa kuwajengea kituo cha afya ili kunusuru maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie na suala la Shule ya Sekondari Lindi. Shule ya Sekondari Lindi, ni shule ambayo viongozi wengi sana wamesoma pale, akiwemo mama yetu Mheshimiwa Mama Salma Kikwete. Shule hii mwaka 2016 ilipata janga la kuungua moto. Madarasa kadhaa yaliungua, tumefanya harambee, lakini haikukidhi haja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka katika Ofisi ya Waziri Mkuu, tulishauriwa tujenge majengo ya ghorofa mbili. Tumeanza ujenzi, fedha tulizozipata zimetuwezesha kujenga msingi tu. Tunaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu na Ofisi yake waone namna ambavyo wanaweza kutusaidia kujenga shule hii ambayo imeungua.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. MOHAMED M. UTALY: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mohamed Mussa Utaly, nilimtaja Mheshimiwa Juma Mustafa Kawamba, Mheshimiwa Twaha Said Mwakioja na Mheshimiwa Zuberi Yahya Mfaume ajiandae.

MHE. JUMA M. KAWAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia Hotuba ya Waziri Mkuu yenye mwelekeo na mapitio ya kazi za Serikali kwa mwaka 2026/2027. Kwanza kabisa, ninaanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenijalia afya njema na ametujalia Wabunge wote kufika hapa siku hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani zangu za kipekee nazipeleka kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri na maono yake mazuri anayoendelea kulitumikia Taifa hili. Hakika uzalendo wake hauna mfano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, kwa hotuba yake nzuri

inayoakisi mwelekeo chanya kwa kazi nzuri za Serikali na ziara zake anazoendelea kuzifanya ndani ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, ninaomba niwashukuru wananchi wa Jimbo la Igalula kwa heshima kubwa waliyonipa na kunichagua kuwa Mbunge wao wa Jimbo la Igalula. Ninaahidi hapa sitawaangusha, na sitakubali kuona Igalula haipigi hatua za kimaendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichangie. Ninaanza kwenye sekta ya afya. Serikali imeendelea kuwekeza miradi mingi ndani ya sekta ya afya. Hotuba inaeleza miradi 113 inatekelezwa, miradi 45 inatekelezwa ndani ya hospitali za mikoa, na miradi 48 inatekelezwa ndani ya hospitali za halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi 5,000 wameajiriwa ndani ya siku 100 za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, na Serikali imewekeza kwenye vifaatiba na dawa kutoka 80% mwaka 2024 mpaka sasa 89% mwaka 2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo, bado kuna changamoto zifuatazo ndani ya Jimbo langu la Igalula. Upungufu na ukamilishaji wa vituo vya afya na zahanati, uhaba wa wataalamu wa afya, na umbali mrefu wa wananchi kufuata huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Igalula, ninapenda kuishauri Serikali yafuatayo: kukamilisha ujenzi wa vituo vya afya katika ngazi ya kata zenye upungufu ikiwemo Kata ya Igalula, Goweko, Kizengi, Loya, Tula na Lutende; na ujenzi wa vituo vipya katika kata ambazo hazijafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kupeleka watumishi wa afya ngazi ya msingi kwenye kata, vijiji na vitongoji, kuboresha upatikanaji wa dawa hususan katika vituo vya afya na zahanati, na kupandisha kituo cha afya walau kimoja katika Jimbo la Igalula kuwa na hadhi ya hospitali ya wilaya ili kuweza kuepuka adha za akina mama na watoto kutembea umbali mrefu kufuatana na *nature* ya Wilaya ya Uyui jinsi ilivyo kimuundo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mapambano dhidi ya UKIMWI, Serikali imeendelea kuwekeza fedha nyingi kwenye mapambano dhidi ya UKIMWI. Takwimu zinaonesha kwamba watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI ni takribani milioni 1.7. Uelewa wa watu wa hali ya maambukizi juu ya UKIMWI umefikia 92%, matumizi ya dawa za *ARV* yamefikia 98.5%, ufanisi wa dawa umefikia 98.1%, na vituo vya kutibu magonjwa ya UKIMWI vimeongezeka kutoka 7,803 mpaka 82,005. Dawa za *ARV* zinatolewa bure kwa 100%. Serikali pia imekusanya fedha shilingi bilioni 26.8 kupitia Mfuko wa Hifadhi ya UKIMWI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na haya mafanikio, ninapendekeza yafuatayo kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Igalula. Serikali kuongeza utoaji elimu kwa vijana juu ya masuala ya UKIMWI, Serikali kutoa elimu kwa vijana juu ya masuala ya UKIMWI, kuimarisha ushirikiano na wadau wa sekta ya maendeleo, kuunganisha huduma za VVU na huduma za magonjwa yasiyoambukiza kama vile kisukari, presha, moyo na afya ya akili, na Serikali kuongeza kwa kasi kuendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ukamilishaji wa Kiwanda cha kutengeneza *ARV* kilichopo Arusha - *TPI* ili kuendelea kuwa na uhakika wa upatikanaji wa dawa za *ARV* ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali kuwapatia *support (moral and material support)* watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI wanaotengeneza vifaa mbalimbali ili kutambulika na *TBS* na bidhaa zao kupata soko kwa uhakika zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, magonjwa yasiyoambukiza. kama vile Kisukari, Shinikizo la Damu, Saratani, na Afya ya Akili yanaongezeka kwa kasi hapa nchini na kuwa tishio kubwa kwa afya za wananchi wetu. Jambo la kupongeza ni kwamba Serikali imeendelea kuwekeza katika huduma za kibingwa na ubingwa bobezi pamoja na kuwekeza kwenye vifaatiba na dawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ninaiomba Serikali kutengeneza mkakati maalumu wa kitaifa wa kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza, kuanzisha uchunguzi wa mara kwa mara katika vituo

vya afya, kutoa elimu ya lishe bora na mtindo wa maisha kwa vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichangie sekta ya miundombinu. Serikali imeendelea kuwekeza katika sekta ya miundombinu ya nishati na huduma za kijamii. Hadi kufikia Februari 26 vitongoji 39,003 sawa na 61% vimeunganishwa na umeme. Hii ni hatua kubwa, lakini bado maeneo mengi ya Jimbo la Igalula hayajafikiwa kikamilifu na huduma hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali kuhakikisha upanuzi wa umeme vijijini ikiwemo jimbo la Igalula, kuboresha barabara kupitia Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini ikiwemo barabara ya Isuli – Miyenze, Misole – Miyenze – Nyahua, Malongwe – Mabeshi, Goweko – Kigwa, Miswaki – Loya, Goweko – Igalula Mpakani na Igalula – Kigwa. Kujenga madaraja maeneo korofi ikiwemo eneo la Loya, Vumilia Kata ya Igalula, Mbulumbulu Kata ya Mmale, Mdaki kata ya Kizengi na Tulieni, Kata ya Tula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vijana na ajira, Serikali imetoa shilingi bilioni 200 kwa ajili ya kuwekeza kwa vijana kiuchumi. Aidha, zaidi ya vikundi takribani 12,977 vimepatiwa mikopo ya 10% na ajira zimeongezeka kwa 31.4%. Pamoja na mafanikio hayo ...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa, muda wako umemalizika.

MHE. JUMA M. KAWAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalizie. Pamoja na mafanikio hayo ninapenda kushauri, kwa ujumla ninaipongeza Serikali kwa kazi kubwa inayofanya katika kuwaletea wananchi maendeleo. Hata hivyo, utekelezaji wake unapaswa kulenga zaidi wananchi wa vijijini ili kuleta usawa wa maendeleo mijini na vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, ninaunga mkono hoja kwa 100%.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Juma Mustafa Kawamba, Mheshimiwa Twaha Said Mwakioja ajiandae.

Mheshimiwa Juma Mustafa Kawamba, hayupo? Amemaliza, *okay*. Mheshimiwa Twaha Said Mwakioja atajiandaa Mheshimiwa Zuberi Yahya Mfaume.

MHE. TWAHA S. MWAKIOJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nitumie nafasi huu kumshukuru sana Muumba wangu kwa neema hii ya uhai, afya na baraka ya kuwepo katika ukumbi huu wa Bunge letu Takatifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninakushukuru wewe kwa nafasi hii muhimu ya kuwasemea wananchi wenzangu wa Tanzania na kwa umaalumu wa kipekee wananchi wa Jimbo la Mkinga. Tatu, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna alivyotekeleza vyema Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi iliyoishia mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza pia alivyomalizia utekelezaji wa Dira ya 2025 ambayo inamalizika Juni na alivyotekeleza kwa umahiri Mpango wa Tatu wa Maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo matatu ya mfano yaliyonigusa kufikia kusema, ninampongeza sana, eneo la kwanza, pamoja na changamoto nyingi za mwenendo wa uchumi duniani, lakini nchi yetu uchumi wake umeimarika na kuweza kufikia asilimia sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna alivyosimamia vyema ukusanyaji wa mapato, mapato yanayotokana na kodi na mapato yasiyotokana na kodi. Taarifa iliyopo katika hotuba ya Waziri Mkuu kuanzia Juni mpaka Februari, 2026, tuna ufanisi wa 103%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu, ninalompongeza Daktari ni kwa namna alivyoimarisha mahusiano ya Kitaifa na Kimataifa hadi miradi zaidi ya 927 yenye thamani zaidi ya shilingi trilioni 28, imesajiliwa.

Kwa kweli pongezi kubwa kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Waziri Mkuu wetu kwa namna anavyotekeleza vyema majukumu yake, na kwa namna Wizara zake zilizopo katika ofisi yake zinavyotekeleza vyema majukumu yao na namna alivyotoa dira na mwelekeo wa nchi yetu wa mwaka 2026, katika hotuba aliyoitoa katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maeneo mahsusi ninayoweza kuchangia, ninapenda nijikite katika maeneo matano yanayohusu Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo mimi kwa maoni yangu ninatambua kwamba nchi yetu hatuna upungufu wa mipango mizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna upungufu wa bajeti nzuri, hatuna upungufu wa mikakati, ila haya maeneo matano yakiimarishwa katika Ofisi ya Waziri Mkuu, ninaamini utekelezaji wa Dira inayoanza Julai na utekelezaji wa Mpango wa Nne unaweza kuleta matokeo tarajiwa makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza ni namna ya kuboresha uratibu katika Ofisi ya Waziri Mkuu, uratibu ndani ya Bunge na uratibu nje ya Bunge. Serikali yetu imekuwa na changamoto kubwa ya *coordination* imekuwa na *duplication* ya *effort* ya sekta na sekta, imekuwa na mwingiliano wa majukumu, imekuwa na namna ya kunyang'anyana *resources*, imekuwa na namna ya kila mtu anavuta kwenye sekta yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili litawezekana tu pale ambapo Ofisi ya Waziri Mkuu itakapoweza kuunganisha kwa mfumo wa ki-*digit* usimamizi wa bajeti, usimamizi wa *resources* ili kuondoa utekelezaji wa majukumu uliopo kama vile kila sekta inafanya kama ipo kwenye kisiwa chake, kila mtu anafanya kama ni mpiga ngoma anawapigia watu wake peke yake ilhali sote tunamhudumia mwananchi mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninatamani Ofisi ya Waziri Mkuu iwe kama *Policy Coordination Hub* yenye mfumo mmoja wa kidigiti unaoweza kuiangalia nchi moja, kwenye *dashboard* moja namna ya kutekeleza majukumu ya kila sekta ya *MDAs* na *LGAs*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo ninataka nilizungumzie, ni eneo la ufuatiliaji na tathmini. Tumekuwa na utamaduni ambao kwa maoni yangu, ninauona siyo utamaduni mzuri. Tunaangalia ufuatiliaji na tathmini kwa kuangalia nimeweka fedha shilingi milioni 10, nimepata darasa moja hapo tumemaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatupimi matokeo yanayotokea kwa wananchi. Je, madarasa haya yanaleta matokeo gani kwa wananchi? Barabara hii tuliyoijenga inaleta matokeo gani? Kwa hiyo, hapa ninashauri tuimarishe mfumo wetu wa ufuatiliaji na tathmini ili kupima *outcomes*, kupima *impacts* na siyo kuishia kupima *input* na *output* kama inavyofanyika sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili, ninashauri vipengele vitatu, tuimarishe au tutengeneze Mfumo wa *Real Time Tracking System*. Tuwe na mfumo ambao unakuonesha mradi huo uko sehemu fulani, uko hatua fulani, unatekelezwa na watu fulani, unaleta matokeo fulani mpaka wakati huu. Kuliko sasa hivi tunatumia sana *physical monitoring* ya kukimbizana, ya kukimbiza magari mengi, lakini tungekuwa na Mfumo ambao ni *Real Time Tracking System,* haya yote yangepungua, yangeleta ufanisi, yangepunguza gharama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine katika eneo la ufuatiliaji na tathmini, ninatamani tuwe na *Performance Contracts* za viongozi wetu mbalimbali wanaotarajiwa kutoa matokeo mbalimbali. Sasa hivi tunafahamu kiongozi fulani hajafikia matokeo yake, akifika Mheshimiwa Waziri Mkuu, au akifika Mheshimiwa Rais ndiyo tunaona kiongozi huyu hajakamilisha majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa na *Performance Contracts* ambazo zitakuwa zimeunganishwa na Mfumo wa *Real Tracking System,* hapa mapema kabisa ataonekana Mkurugenzi fulani, Mkuu

wa Wilaya fulani, Waziri fulani hajatimiza wajibu wake, na hii inatosha kabisa kuchukuliwa hatua za wazi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu katika eneo la *Monitoring and Evaluation*, ninashauri kwa miradi mikubwa ya kimkakati, tuwe na kitu kinaitwa *Independent Evaluation*. Tuwe na taasisi za nje ya mfumo wa Serikali ambazo zinaweza zikatufanyia tathmini ili tujione namna gani tunafikia matokeo, kuliko sisi wenyewe ni wachezaji na sisi wenyewe ni marefa na sisi wenyewe tunasema kwamba tumefikia hatua fulani. Kwa hiyo, jambo la pili ninashauri tuimarishe mfumo wetu wa *Monitoring and Evaluation*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu ninaloshauri katika Ofisi ya Waziri Mkuu ni eneo la kukabiliana na maafa, majanga na matukio ya dharura. Mfumo wetu umekuwa ni *reactive* sana kuliko *proactive*. Tunasubiri janga litokee halafu tunaanza kukimbizana *resources* zote zinaelekezwa huko badala ya kutekeleza bajeti iliyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tukiwa *reactive*, tukiimarisha mfumo wetu wa *Early Warning System* tukawekeza hapo, basi tutaweza kukinga zaidi kuliko kuwekeza *resources* pale majanga yanapotokea. Eneo hilo la Waziri Mkuu ninashauri liweze kuimarishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la nne ni urasimu, ucheleweshwaji wa maamuzi na uwajibikaji wa wazi. Kweli ninatambua urasimu ni sifa nzuri ya Serikali, lakini kwa maoni yangu urasimu umezidi, tunachelewesha utekelezaji, na maamuzi. Unakuta bajeti imefika katika taasisi husika ndani ya miezi mitatu hakuna hatua hata moja iliyochukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona fedha za Serikali, Mheshimiwa Dkt. Samia anapeleka nyingi, tunasingizia Mfumo wa *NeST* kwamba unatuchelewesha siyo kweli, watendaji wetu hawachukui maamuzi. Tuimarishe eneo la maamuzi, tuimarishe eneo la kupunguza urasimu na uwajibikaji wa wazi. Hili tutaweza kwa kutumia takwimu sahihi, kwa kutumia teknolojia na watu wachukuliwe hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tano kwa Ofisi ya Waziri Mkuu na la mwisho, na kisha nitasema eneo mahsusi kwa Ofisi ya TAMISEMI, ni namna gani tunaisimamia sekta binafsi? Tumeipa sekta binafsi jukumu kubwa sana la kutoa ajira zaidi ya 85%. Tumeipa jukumu kubwa katika utekelezaji wa dira itutafutie fedha zaidi ya 70% ili tufikie uchumi wa kati wa juu wa zaidi ya shilingi trilioni moja, tufikie uchumi wa mtu mmoja wa dola 7,000. Je, sekta hii binafsi tunaiamini kwamba inaweza kuyafanya hayo? Je, sekta hii binafsi tunaiwezesha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, sekta hii binafsi tunaiweka kwamba ndiyo mhimili; tuipunguzie milolongo ya urasimu, tuipunguzie tozo, tuipunguzie namna wawekezaji wanavyobambikiwa kodi, tuipunguzie mambo mbalimbali ili iwe mhimili mkubwa wa uchumi ...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. TWAHA S. MWAKIOJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, bila sekta binafsi kuwa imara, hatutaweza kufikia matokeo tarajiwa ya utekelezaji wa Dira yetu. Haya ni maeneo matano nilitamani niyachangie katika Ofisi ya Waziri Mkuu. Nijielekeze katika eneo moja katika Ofisi ya TAMISEMI ...

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante sana, kengele ya pili imelia.

MHE. TWAHA S. MWAKIOJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba dakika moja, nimalizie eneo moja, la elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua Mheshimiwa daktari ameajiri walimu wengi zaidi ya 40,000 kwa miaka yake, madarasa mengi yamejengwa, shule nyingi zimejengwa, lakini tuna changamoto ya ubora wa elimu. Tujikite sasa kwenye ubora, miundombinu iboreshwe, walimu wetu wapewe stahiki zao, shule zetu zinavuja, watoto wanakaa chini, vyoo, madarasa na kadhalika ili tupate elimu bora. Bila elimu bora hatutaweza kuondoa umaskini ...

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante sana.

MHE. TWAHA S. MWAKIOJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha, na ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Twaha Said Mwakioja, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea, ninaomba nikumbushie Kanuni zetu ili twende vizuri tusije tukaonekana kwamba hatuelewi Kanuni ama tunazipuuza kanuni zetu. Kanuni ya 70 (1) inatakiwa michango yote inayotolewa na Wabunge ielekezwe kwa Spika ama kwa Kiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Kanuni ya 70 (7) Mbunge haruhusiwi kusoma maelezo yake, Mbunge anatakiwa arejee tu kama ana neno moja ameandika kwamba sasa ninataka kuzungumzia hili, anaweza akarejea, lakini kusoma yote ambayo umeandika kwa mujibu wa Kanuni ya 70 (7) hairuhusiwi.

Kwa hiyo, kuna wenzetu kule nje, wananchi wanaelewa kwamba Mbunge akiwa ndani ya Bunge hatakiwi kusoma maelezo yake. Kwa hiyo, tusije tukaonekana hatuelewi ama tunavunja Kanuni zetu. Ninaomba hilo lisirejee.

Waheshimiwa tunaendelea na Mheshimiwa Zuberi Yahya Mfaume, atafuatiwa na Mheshimiwa Asha Hussein Saleh.

MHE. ZUBERI Y. MFAUME: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia fursa hii ya kuchangia hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia sisi sote fursa ya kuwa hapa leo na kufanya Shughuli za Bunge. Kipekee kabisa ninapenda nimpongeze Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Makamu wa Rais Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa ushindi mkubwa walioupata katika uchaguzi uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kipekee kabisa ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kushinda kwa kishindo Uchaguzi Mkuu uliopita na leo hii kuwa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze mchango wangu kwanza kwa kutoa pole nyingi kwa wananchi wa Jimbo la Morogoro Kusini. Kwa sasa tumepata baraka ya mvua mfululizo kwa wiki tatu. Mvua hii sasa imesababisha mafuriko makubwa kiasi ambacho mawasiliano yamekuwa magumu kwa wananchi wa Jimbo la Morogoro Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni katika kipindi hiki takwimu za vifo vya mama na mtoto inakuwa inaongezeka kwa kiasi kikubwa jimboni kwetu kwa sababu mawasiliano kutoka kwenye makazi ya watu kwenda kwenye zahanati yanakuwa magumu kwa sababu mito imejaa na hawawezi kuvuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ni likizo maalumu kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari, watakuwa nyumbani kwa kipindi cha takribani miezi miwili kwa sababu pia ya kushindwa kuvuka kwenda kupata elimu. Kwa sababu hiyo pia takwimu za ufaulu katika Jimbo la Morogoro Kusini zinakuwa ziko chini sana. Moja ya sababu ni kwamba tuna mito mingi, lakini hatuna vivuko. Kwa hiyo, tunashindwa kupata huduma za afya na tunashindwa kupata elimu kwa sababu ya changamoto hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata huku katika maeneo ya bondeni, watu wengi wanaliwa na mamba, kwa sababu hata wanapojaribu kuvuka kwenda kutafuta mahitaji, wanakutana na changamoto hiyo. Ninaiomba Ofisi ya Waziri Mkuu, Kitengo cha Maafa iliangalie jambo hili kwa namna ya kipekee kabisa na hasa kutuangalia katika vivuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa nilete agizo aliloniagiza Mheshimiwa Waziri Mkuu tulipokutana katika Bwawa la Kidunda pale, wakati wanafanya malipo ya wananchi wa Kijiji cha Bwira Chini, pamoja na Kiburumo, ili wahame kupisha ujenzi wa Bwawa la Kidunda, waliwahamisha na kuwapeleka eneo linaoitwa Mji Mpya na kuvifuta vijiji vile. Tangu wawe hapo hawana huduma yoyote ya msingi ya Serikali za Mitaa, Serikali za Vijiji hazipo. Kwa hiyo, tulipeleka

ombi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ya kwamba, tunaomba Kijiji cha Bwira Chini na Kijiji cha Kiburumo virejeshwe katika mji mpya kwa majina yaleyale, pamoja na vitongoji vilevile, ili waweze sasa kupata huduma na Serikali pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu aliniambia nililete Bungeni na nilieleze hapa na leo nimelileta na ninalieleza, nikiomba Ofisi Waziri Mkuu ilichukuwe liende likalifanyiwe kazi. Pia kama haitoshi, vijiji hivi ambavyo viko katika Kata ya Selembala kuna vijiji vingine vitatu, ambavyo ni Bwila Juu, Kiganila na Magogoni; hivyo navyo sasa vinamezwa na mafuriko na mmomonyoko wa Mto Ruvu, wanaomba kwa sababu, wanapakana na Hifadhi ya Mkulazi, basi Serikali ione namna inavyoweza kuwahamisha katika sehemu ya hifadhi, ili kuepukana na adha hiyo. Kwa taarifa nilizonazo watu wawili wameliwa na mamba wiki moja nyuma kutokana na hali hii ya mafuriko na maji kuingia huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia Ofisi ya Waziri Mkuu, naipongeza Serikali, inafanya kazi kubwa sana, lakini pia, sisi sote humu ni mashahidi kwa sababu, kila aliyesimama ametambua juhudi kubwa anayofanya Mheshimiwa Rais katika kutuletea maendeleo, lakini sisi tunamsahau Mheshimiwa Rais. Mimi ni Mbunge ambaye miongoni mwa wananchi ninaowawakilisha katika Bunge lako Tukufu ni pamoja na Dkt. Samia Suluhu Hassan. Yeye ni mkulima katika Jimbo la Morogoro Kusini, analima katika Kata ya Mvuha, lakini yeye na wananchi wenzake katika kata ile hawana maji, pamoja na sifa kubwa ya pesa nyingi anazopeleka katika Wizara ya Maji, lakini hana maji katika Kata ya Mvuha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nafikiri alipokea taarifa ya ku-*erect* minara zaidi ya 750 ya mawasiliano, lakini akiwa katika shamba lake pale Kijijini Msonge, huwezi kumpata kwa simu, hana mawasiliano ya simu. Kwa hiyo, ninaiomba Wizara sasa ika-*elect* mnara kule, kama kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anazozifanya katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais anapotoka Dar es Salaam kwenda shambani kwake, kutoka kwenye Kata ya Tununguo,

ni kilometa tano, ili afike Kijiji cha Msonge, lakini haiwezekani kwa sababu, eneo hilo halijaunganishwa kwa daraja. Inambidi Mheshimiwa Rais asafiri kilometa 60 zaidi, ili kuweza kufika sehemu ambayo ndiyo anafanya shughuli zake za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba basi, wale wenye dhamana ya ujenzi wa madaraja na barabara wawafikirie wananchi wa Kijiji cha Msonge, lakini zaidi wamsaidie pia, Mheshimiwa Rais. Anakwenda kustaafu, muda mwingi atakuwa yuko shamba, basi awe na usafiri mwepesi na wa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine...

MWENYEKITI: Mheshimiwa, muda wako umemalizika.

MHE. ZUBERI Y. MFAUME: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Asha Hussein Saleh na Mheshimiwa Khalid Mussa Nsekela ajiandae.

MHE. ASHA HUSSEIN SALEH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwanza kabisa ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia neema ya uhai kuweza kufika hapa tukiwa wazima wa afya. Pia, ninapenda kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuchaguliwa na wananchi kwa 98%, ili kuweza kuiongoza Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika wananchi wamefanya maamuzi sahihi, kwani wameamua maendeleo. Wamechagua maendeleo kwani Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni shupavu na mbobezi wa kuweza kuiletea maendeleo Nchi ya Tanzania. Kwa vile, ukiangalia, ameweza kumtua mama ndoo kichwani pamoja na mtoto, ameweza kuwekeza katika vituo vya afya pamoja na kuimarisha diplomasia ya uchumi ndani ya Tanzania na kuendeleza katika sekta ya usafirishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, amefanya haya kwa kujua kwamba, hili ndilo suala linaloweza kusababisha kukua uchumi wa Taifa letu, pamoja na kipato cha wananchi na kuwaondolea shida wananchi wake. Aidha, ninapenda pia, kumpongeza Dkt. Hussein Ali Mwinyi na yeye kwa jitihada zake za kuleta maendeleo ndani ya Nchi ya Zanzibar. Hakika amefanya mengi ndani ya Jimbo la Fuoni katika kutuletea elimu bora na shule za ghorofa, hospitali, pamoja na kutujengea barabara zinazopitika kwa kila kona ndani ya Jimbo la Fuoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuishukuru Kamati Kuu. Kwa vile ni mara ya kwanza kusimama katika Bunge hili Tukufu, ninapenda kuipongeza Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi kwa kupendekeza jina langu, ili kuweza kugombea na leo hii kuwa Mbunge wa Jimbo la Fuoni. Pia, bila kusahau, ninawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Fuoni kwa kukichagua Chama Cha Mapinduzi na kusababisha leo hii kuwepo ndani ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba nijelekeze katika mchango wangu kwa Ofisi hii ya Waziri Mkuu, nitachangia katika suala la mazingira. Jimbo la Fuoni limejaliwa kupata bahari na niliposoma wasilisho la Waziri Mkuu, amezungumza juu ya mazingira na tabianchi na sisi pale Fuoni tunayo bahari, lakini pia, Waziri Mkuu alisema ametoa mafunzo, pamoja na kuwanunulia boti wananchi ambao wanahusiana na idara ya mazingira. Kwa hiyo na sisi pale Fuoni kwa kuwa, tunayo bahari na pia, tunaathirika kwa kiasi fulani na mazingira, basi ninachukua fursa hii kumwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kuwapatia vijana pale wavuvi ambao wanajielekeza katika ufugaji wa kaa, awapatie mafunzo, pamoja na boti, kama alivyoelekeza ndani ya hotuba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili la mazingira pia Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, alipokuwa Makamu wa Rais alitembelea ndani ya Jimbo la Fuoni kujionea hali halisi ya wafugaji wa kaa. Kwa hiyo, sasa ninamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa vile na yeye anatembelea Tanzania nzima kupokea changamoto, basi atembelee katika Jimbo la Fuoni. Aje kuwaona

wananchi wa pale wanaofuga kaa, apokee changamoto zao na suala hili kwa vile lipo ndani ya ofisi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa hapo hapo katika hiyo idara ya mazingira, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aweze kutembelea katika Jimbo la Fuoni, katika Wadi ya Fuoni Mambosasa kwa sababu, kule tuna Bonde la Jangamizini, ambalo linajaa maji na wananchi wake wanahamahama. Wakati mwingine linasababisha hata watoto wadogo wanaweza kufariki kwa kupita katika eneo lile. Eneo lile ni sugu katika kujaa maji pale, basi ninaomba kupitia Bunge hili Tukufu, Mheshimiwa Waziri Mkuu afanye ziara mahususi ili aweze kututatulia changamoto zilizoko pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa busara na hekima zake za kuweza kutenga shilingi bilioni 200, kwa ajili ya vijana. Shilingi bilioni 200 hizi Mheshimiwa Rais alizielekeza ili kuweza kutatua changamoto za ajira, vijana pamoja na wanawake. Kutokana na vijana wenyewe kutojua au kuweza kuwa na ule uelewa wa kufanya katika kuomba yale maombi imefikia mpaka zoezi lile limefungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi ninaiomba Serikali kwa makusudi mazima kuweza kulifungua dirisha hili la maombi ya fedha zile za Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu, ili waweze na wao kujitatua kiuchumi, kwani vijana hawana ajira, lakini fedha zile zimetegwa kwa ajili yao. Likifunguliwa dirisha hili, basi wananchi, vijana na wanawake, hususan vijana wa Jimbo la Fuoni watachangamkia fursa hizi za kuweza kuomba mikopo hii ili waweze kujinasua kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijielekeze kidogo katika eneo la usafiri yaani barabara. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria; tulipata fursa ya kutembelea Mkoa wa Geita katika Mji wa Nyang'hwale, tulikwenda pamoja na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete. Katika ziara ile tulipokuwa tunalekea Mji wa Nyang'hwale, basi ilikuwa kusema kweli ni guburu guburu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, guburu guburu tangu tunaingia ndani ya Mji wa Nyang'hwale mpaka tumefika Nyang'hwale. Kama

tunavyojua Mji wa Geita ni wa madini, ambapo wapo wawekezaji wadogo wadogo. Ripoti ya Waziri Mkuu imesema kwamba, sekta ya madini kwa Julai, 2025 mpaka Januari, 2026 imekusanya mapato ya 64.3%. Kwa hiyo, Mkoa wa Geita unachangia pato hili la Taifa. Basi ninaiomba Serikali kwa makusudi mazima iweze kuwajengea barabara Mji wa Nyang'hwale kwa sababu, barabara yake ni mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajielekeza katika suala la Muungano. Ninawapongeza kwanza Waheshimiwa Marais wetu wawili walioadhimisha suala hili. Ninampongeza Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere pamoja na Hayati Sheikh Abeid Amani Karume kwa kuanzisha suala hili. Kwa kweli, suala hili ni zuri na kama wana wa Tanzania basi inatupasa kudumisha na kuuenzi Muungano huu kwa nguvu na hali zote. Zile kero za Muungano zilizobaki, basi ninamwomba Waziri Mkuu aweze kuchukua juhudi za makusudi, ili kuweza kumaliza kero hizi za Muungano. Baada ya hapo naomba nijielekeze kwenye Mfuko wa Jimbo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Asha, muda wako umekwisha.

MHE. ASHA HUSSEIN SALEH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalize kwa dakika moja. Katika Mfuko huu wa Jimbo, basi ninaomba idara zinazohusika watume kwa wakati, Wabunge tunapopeleka miradi yetu waweze kututekelezea kwa wakati, ili fedha hizi za Mfuko wa Jimbo zisiweze kukutana na fungu lingine linalokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Fuoni, ninaunga hoja kwa asilimia mia moja.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Asha Saleh. Nilimtaja Mheshimiwa Khalid Mussa Nsekela. Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo ajiandae.

MHE. KHALID M. NSEKELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa nafasi hii ya kuchangia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai na afya ya kuweza kuwa hapa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua nafasi hii kukushukuru wewe hapo na ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa ambayo ameifanya, hasa ya kuzunguka ndani ya Nchi ya Tanzania, mikoa mbalimbali na kutatua kero. Nichukue nafasi hii, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kyerwa, Mkoa wa Kagera kumwomba kwamba, angalau tunashukuru kama tutawekwa kwenye ratiba atutembele Mkoa wa Kagera na Jimbo la Kyerwa na sisi tuna kero nyingi sana, tunapenda tumwambie uso kwa uso. Hili ninamshukuru Mheshimiwa Rais, ninakumbuka wakati anafungua Bunge hili alielekeza kwamba, uongozi wake utajikita sana kwenda kuwasikiliza Watanzania na kutatua kero zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichangie kidogo kwenye hotuba hii nzuri kabisa ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ninachangia maeneo matatu, eneo la kwanza ninaomba nichangie kwenye suala la barabara, miundombinu ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatokea Jimbo la Kyerwa, sisi ni wakulima wa zao la kahawa, zao kubwa kabisa, zao la kimkakati. Sisi tuna athari kubwa sana kutokuwa na barabara nzuri, hasa barabara ya lami, barabara za vijijini. Kutokuwa na barabara za vijijini ni tatizo kwa sababu, tunatambua kwamba, barabara siyo tu kwa ajili ya kusafirisha mazao na watu, lakini ni uti wa mgongo wa huduma za jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia suala la afya, Mheshimiwa Rais ameleta vituo vya afya vya kutosha. Tunavyo vituo vya afya vitano katika Jimbo la Kyerwa, lakini kitendo cha kutokuwa na barabara imara inakuwa ni changamoto kwa mwananchi kutoka nyumbani kwake kwenda kupata huduma kituo cha afya kwa sababu, hawezi kupita ile barabara na hasa katika hali hii ya mvua, unakuta kuna sehemu huwezi kuvuka. Mvua ikianza lazima wananchi wakae hapo mpaka iishe ndiyo waweze kuvuka. Barabara kama sehemu za Munchwekano kule, ukienda Kihea, ukienda Rwabwere, vijiji ni vingi sana ukisema uvitaje huwezi kupata muda wa kutosha, lakini barabara zile ni mbovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda vilevile kwenye suala la kilimo. tunajua wakulima, ili waweze kupata tija ni lazima waweze kupeleka mazao yao sokoni. Kitendo cha kutokuwa na barabara imara, mkulima anapata changamoto na sana sana, tunakuja kupata tatizo la *post harvest loss*, mazao mengi sana hayafiki sehemu za masoko. Barabara ni muhimu sana na katika suala la uchumi wa Tanzania nzima, tumeona nchi nyingi sana zimetoka hatua moja kwenda hatua nyingine baada ya kuwa na miundombinu imara ya barabara, tunatambua hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la maji. Tunatumia gharama nyingi sana kupeleka mitambo, sijui wataalam kwenda kutengeneza miradi ya maji, lakini kitendo cha kutokuwa na barabara ni shida kubwa sana, hasa katika Jimbo la Kyerwa ambalo jiografia yake kidogo imekaa vibaya, milima na mabonde. Kutokuwa na barabara unakuta ni changamoto sana kupeleka miradi sehemu ambayo inatakiwa kwa sababu, wataalam wa mradi huo hawawezi kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kuhudumia ile miradi vilevile inakuwa ni ngumu pale tunapokuwa na changamoto ya hiyo miradi. Kwa hiyo, rai yangu ni kwamba, tunaomba *TARURA* iongezewe nguvu ya kuweza kuhudumia hizi barabara, tunatambua umuhimu wake, tunatambua umuhimu katika uchumi na katika kutoa huduma. Tukiwa na barabara imara hatutatumia gharama nyingi kupeleka zile huduma pale zinapotakiwa. Ninatoa rai kwamba, ni muda sasa hizi halmashauri ziongezewe nguvu na kujengewa uwezo wa kuhudumia hizi barabara za *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni sehemu ya vijana. Tunatambua tuna zaidi ya 60% ya vijana katika nchi hii. Hii ni *asset* kubwa sana kwa Nchi ya Tanzania, hasa tunapojiandaa kwenda katika Dira yetu ya 2050. Tukiwekeza vizuri katika hawa vijana, tukawapa ujuzi na tukawatengeneza, tunaamini kabisa kwamba, sisi tutafika vizuri katika hiyo dira yetu na hapa namshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa jitihada na *initiative* ambazo amezifanya katika kumkomboa na kumnyanyua kijana wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona ameanzisha Wizara ipo chini yake, lakini bado ametoa shilingi bilioni 200 ambazo nyingi zinaenda kwenye sekta ya vijana. Hii ni dhahiri kwamba, Mheshimiwa Rais ana maslahi mapana ya vijana wa Tanzania. Mimi hapa, kama kijana, ninaomba nitoe rai kwamba, hizi hela zinakwenda kwa vijana ambao tayari wameanza kuwa na biashara ndogondogo kuwawezesha kuwa na mtaji mdogo, lakini wapo vijana wengi sana mtaani ambao hawana uwezo wa kuanza biashara hata ndogondogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu ni kwamba ni muda sasa hizi halmashauri ambazo ziko mikoani na halmashauri zote nchi nzima ziwe na kitengo ambacho kitawaruhusu vijana waje pale watoe mawazo yao yanayohusu TEHAMA, kilimo na biashara. Halafu sasa Serikali ione ni jinsi gani ya kuwezesha yale mawazo ili kuwanyanyua, kwa sababu tunajua wapo vijana wengi, tukiwawekea chumba maalum bila hata kuwalipa na kuwaambia vijana njooni hapa, toeni mawazo yenu ya TEHAMA, kilimo, biashara, chochote wewe elezea, wazo lako likoje wataeleza. Tukae pamoja, tuwape na mwalimu au *mentorship* wa kuwaongoza vizuri, tutapata mawazo mazuri, tutaweza kuanzisha vijana ambao tayari watakuwa kwenye biashara na kuendelea juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu, ninaomba nichangie kwenye suala la dira kulingana na hii hoja au hotuba ya Waziri Mkuu. Hii ni bajeti ya kwanza kuelekea Dira ya 2050 na ninamshukuru sana Waziri Mkuu ameelezea vizuri uelekeo wa Dira hii ya 2050, lakini hoja yangu ni jinsi gani mipango yetu inaakisi hii Dira ya 2050? Je, sekta zetu zote zinajielekezaje kumfikisha Mtanzania wa leo kwenye 2050? Kwa sababu tunapokaa hapa Bungeni ninaona kabisa Mawaziri wetu, ukimwona Waziri Profesa Shemdoe na timu yake wapo kwenye *field* wanahakikisha tupate matokeo lakini nani yuko ofisini kwa ajili ya kuandaa TAMISEMI ya 2050?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukimwona Mheshimiwa Waziri Aweso anashughulika na maji ameenda China, amekuja wapi, lakini nani kabaki ofisini kuhakikisha kwamba Wizara ya Maji ya 2050 itakuwa hivi? Kwa hiyo, rai yangu hapa ni kwamba kuna haja sasa rasmi tuwe na kitengo maalum kwenye kila Wizara, kila Taasisi cha ubunifu na mabadiliko makubwa ya kuziandaa sekta zote za Tanzania kwa ajili ya

2050, maana yake ninasema *future ready economy au future ready government*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tuwe na vitengo ambavyo vinakaa ofisini kwamba wakati hawa wako *field* wanafanya kazi hii, lakini hatoki kwenye mstari, tunataka sekta ya afya iwe hivi kwa 2050, sekta ya ujenzi, sekta ya maji, tuwe nazo tayari na mwelekeo mzuri ambao unatuongoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili ninaomba tunapokuwa tunafanya kazi au Wizara zetu tunaambiwa Waziri Mkuu aje na ajenda ya kuchangamana au ku-*incorporate* hizi Wizara zishirikiane kwa sababu, kwa sasa unavyoweza kuangalia kila Wizara inafanya kazi pekee yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aliwahi kuongea Mheshimiwa Musukuma pale, alitoa mfano mdogo akasema Barabara ya kutoka *Airport* kuja Posta - Dar es Salaam ina kona nyingi sana ambazo hazina umuhimu wa kuwa nazo. Lakini ukiangalia ni kwamba Wizara ya Ujenzi haina mahusiano na Wizara ya Utalii. Sisi tunavyotoka kwenda Dubai tunashangaa Barabara za *Sheikh Zaid Road* ni barabara tu. Kwa hiyo, barabara hii nayo ni utalii siyo mpaka uende msituni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Wizara ya Kilimo au tubaki hapa kwenye Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Ujenzi lazima ishirikiane na Wizara ya Nishati, siyo unajenga halafu ndiyo anakuja kuvunja anapitisha nguzo. Wizara ya Maji barabara imejengwa huyu anakuja kuvunja apitishe bomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kabisa mfano tu Wizara ya Kilimo, lazima ikae na Wizara ya Elimu, haiwezekani muda huu hatuna *graduate* anaweza akasema au wanatoka *graduate* saa hizi wanakuja, hana elimu inayohusu madini. Wapo *graduate* hawana elimu kuhusu kilimo, wapo hawana elimu kuhusu utalii. Hii maana yake hatushirikiani Wizara ya Kilimo na Wizara ya Elimu kuona kwamba tunatoa *graduate*s gani kwa ajili ya kuiandaa Tanzania. Uchumi wetu wote uko kwenye kilimo, upo kwenye utalii, upo kwenye madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni hayo ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo na tutamalizia na Mheshimiwa Patrick Adkin Mwalunenge.

MHE. SUMA I. FYANDOMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye bajeti hii ya Waziri Mkuu. Kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa kibali hadi nimeweza kusimama mahali hapa kwa ajili ya kuchangia. Ninakwenda moja kwa moja kwenye mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mbeya tunacho kilio na msiba mzito. Barabara ya Mkoa wa Mbeya kuanzia Igawa mpaka Tunduma ipo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi iliyopita, barabara ile mpaka sasa hivi ina sintofahamu. Barabara ile tunamshukuru sana Rais aliongea kwa unyenyekevu na upendo mkubwa kwamba, barabara hii acha basi tuanzie Uyole mpaka tufike *Airport* Songwe, tulimshukuru sana Mheshimiwa Rais lakini ile barabara inakwenda kwa kusuasua sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba tumeanzia katikati Uyole, Rais ametujengea hospitali kubwa nzuri ya rufaa iko katikati ya Jiji la Mbeya, lakini pia bado ametujengea hospitali ya wanawake ambayo ni ya kujifungua wanawake wa Mkoa wa Mbeya kubwa sana ya Meta ukiachilia mbali vituo vya afya, Rais amejali sana wanawake, ameweka majengo ya mama na mtoto kwenye vituo vya afya vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya za Mkoa wa Mbeya ukianzia Mbalali ukienda Kyela, ukienda Rungwe, Jimbo la Busokelo, Mbeya *DC,* unapokwenda kuzifikia zile hospitali lazima upite katikati ya ile barabara. Barabara ile tunashukuru Serikali iliruhusu fedha kiasi cha shilingi bilioni 183 ili iende kujenga barabara ile. Mpaka sasa hivi miaka mitano ile iliyopita na sasa tumeingia awamu nyingine, barabara ile imejengwa kwa 44%. Ninaomba sana hiki kilio cha wananchi wa Mkoa wa Mbeya barabara sasa hivi katikati ya jiji pale ni vumbi tupu. Mvua

ikinyesha ni matope matupu, jua likiwaka ni vumbi, yaani hakuna usalama wowote juu ya wananchi wa Mkoa wa Mbeya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mkoa wa Mbeya tuna kilio kikubwa sana juu ya barabara ile, tunalia kilio hicho, ajali zinatokea za mara kwa mara, ndugu zetu wanapoteza Maisha, wanakufa, lakini pia wanaopata ajali wengine wanaumia wanabaki kuwa ni walemavu wanaugulia mahospitali mpaka sasa hivi. Ninaomba sana kwa ridhaa yako nimwombe sana Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan atuone wananchi wa Mkoa wa Mbeya, atuone kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mama yetu huyu tunavyomjua, ana hekima ana busara wakati wowote, hapendi kuona wananchi wake wanateseka, tunaamini kwamba kwa kuliona hili atatusaidia wananchi wa Mkoa wa Mbeya ili tuache misiba pamoja na walemavu kwenye Mkoa wetu wa Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mbeya tunajua Tanzania nzima inaombea Taifa amani, inaombea Serikali amani, inamwombea Rais, lakini Mkoa wa Mbeya ndiyo tunaongoza kwa maombi Tanzania nzima. Mkoa wa Mbeya una makanisa mengi sana tunapoanza kuomba lazima tumwombee Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, yeye pamoja na Serikali yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, achilia mbali makanisani hata misibani, wananchi wa Mkoa wa Mbeya misiba inavyotokea alfajiri tunapoanza kulia lazima tuombe sala, hiyo sala lazima wanawake wale wanavyoomboleza, wanamtanguliza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan wakimweka kwenye maombi, namna anavyoongoza Taifa hili la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mkoa wa Mbeya, kawaida yetu tunavyoomba, tunaomba kwa unyenyekevu tukipiga magoti.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. SUMA I. FYANDOMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa sababu ninaheshimu Siwa ipo pale, nilipaswa niende pale nipige magoti…

MWENYEKITI: Mheshimiwa Suma, kuna taarifa. Mheshimiwa Musukuma.

TAARIFA

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kumpa taarifa mzungumzaji kwamba suala la maombi ni siri ya mtu, akisema Mkoa wa Mbeya wanaomba sana, mimi kwa imani yangu ninaamini Mkoa wa Geita ndiyo tunaomba kuliko Watanzania wote.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Suma unaipokea hiyo taarifa?

MHE. SUMA I. FYANDOMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo taarifa siipokei. Ninaomba sana Mheshimiwa Musukuma ninakuheshimu nipo *serious* hapa, kilio cha wananchi wa Mkoa wa Mbeya hajakijua na namna tunavyomwombea Rais hatuongei mdomoni tunamwombea kutoka moyoni, ninaomba sana atambue wananchi wa Mkoa wa Mbeya tukisema tunaomba, tunaomba kweli kweli, hatuombi kwamba tunafanya mizaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza kwamba hapa ninaheshimu Siwa kwa sababu ipo, Siwa isingekuwepo ningekuomba kwa imani yangu ningepiga nikuombe nipite pale mbele nipige magoti ili wajue wananchi wa Mkoa wa Mbeya tunaomba barabara ya Mkoa wa Mbeya kwa kumaanisha, tunaomba sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Rais alichukue hili Mbeya jamani tuna kilio, tuna msiba, ninaamini Rais wetu kwa sababu ni msikivu amesikia, atatuondolea shida iliyopo katikati ya Jiji ambapo msongamano wa magari umekuwa mkubwa sana kwa sababu ya vumbi ile iliyopo pale, kwa sababu ya barabara mbovu na tope lililopo pale, *ambulance* zinavyotoka kwenye Wilaya zile kule kumkimbiza mgonjwa hospitali katikati ya Jiji hazipiti kwa wakati, sina namna ya kuongea zaidi ya hili ninaloliongea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dkt. Samia Suluhu Hassan ni Mama msikivu, wakati wote ninamwongelea hilo kwa sababu ninamwelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais alihamasisha nishati safi kwa ajili ya kupikia, wanawake ndiyo sisi wapishi wakuu, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ndiye Mheshimiwa Rais wetu, yeye Rais katika hili kulikuwa na kilio kwa upande wa mbolea. Kilio kikubwa mfuko wa mbolea ulikuwa unauzwa zaidi ya 155,000. Rais alivyosikia hili jambo alitoa ruzuku mpaka sasa hivi mbolea inauzwa kwa bei ya pungufu karibu 75,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Rais hii nishati safi ambayo ameshatuzoesha kwa sababu tuliitikia sana, wanawake wa Tanzania waliitikia hasa wa Mkoa wa Mbeya, tunaomba ruzuku kwenye gesi ili nishati safi hii iendelee kutumika.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. SUMA I. FYANDOMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona umewasha taa, ninaomba nisipoongea hili pengine ninaweza kuugua, ninaomba nijibu kuna swali moja la Watanzania ninaomba sekunde moja tu nijibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi cha uchaguzi tulikuwa na kikao wanawake, Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Mary Chatanda, Ndugu Zainab Shomari pamoja na Katibu ambao ni viongozi wetu upande wa wanawake, kuna swali ambalo wanajiuliza Watanzania, ilikuwaje Dkt. Samia Suluhu Hassan apate 98% za ushindi. Ninataka niseme hivi, mwanamke akiwa na jambo lake hashindwi, hafeli, wanaume wanalijua hili, Mama jinsi ambavyo anaku-*pet* Baba, kukuomba kitu ambacho anakihitaji hajawahi ku-*fail* hata mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kina baba ambao ni wanaume zetu lakini pia watoto wetu tunakuwa tunawaheshimu na tunawapenda na heshima ni kubwa sana pale ndani, tulizidisha heshima, tulizidisha upendo, akina baba tuliwaomba kura walitusikia wakatupa kura za

heshima za Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika wachache wale ambao wanajiuliza mpaka sasa, ninaomba niseme hivi kipindi kile hakukuwepo mama ambaye alikuwa mkali kwa baba kwamba, ulikuwa wapi? Kwa nini umechelewa? Hata baba akirudi saa sita za usiku alikuwa akipokelewa koti.

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. SUMA I. FYANDOMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, akikaribishwa kwa upendo, ndivyo ambavyo tulipata zile kura na tulitegemea zingepatikana kura asilimia mia moja, kura mbili ndiyo zilipotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo. Tunamalizia na Mheshimiwa Patrick Adkin Mwalunenge.

MHE. PATRICK A. MWALUNENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa fursa hii mchana na mimi niweze kuchangia bajeti ya ofisi ya Waziri Mkuu. Awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa uzima nikapata fursa hii leo ya kuweza kutoa mchango wangu na mawazo kwenye bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwanza ninamshukuru Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya, alishajipambanua wazi kupitia hotuba yake aliyolihutubia Bunge, maelezo aliyoyatoa na kazi kubwa anazozifanya kwenye nchi hii, Wabunge wengi wamezungumza, sitaki kurudia huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninampongeza Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa bajeti nzuri aliyoleta na kazi anazoendelea kuzifanya kwenye nchi hii, kwa ziara anazozifanya kwenye mikoa na kutatua kero za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaleta matumaini makubwa kwa wananchi wa Tanzania kwamba sasa Serikali yao ipo kazini. Ninasisitiza tu Wasaidizi wa Rais kwa maana ya Mawaziri, wasaidizi wa Waziri Mkuu sasa waige ile njia anayoifanya Waziri Mkuu kutatua kero za wananchi na hiyo ndiyo njia pekee ambayo wananchi wetu

wanataka. Wananchi wa sasa wanataka kuona matokeo tumeshazungumza sana, tumeshaandika sana makaratasi, hasa vijana waliopo sasa wanataka kuona matokeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ni nzuri, mambo ni mengi yamezungumzwa, nijikite kwenye Jimbo langu la Mbeya Mjini, pia niendelee kumpongeza na Dada yangu aliyetangulia kuzungumza hapa Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo ametuwakilisha vizuri wananchi wa Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru wananchi wa Mbeya Mjini kwa kunipa imani hiyo ya kuwa mwakilishi wao hapa Bungeni. Wanambeya mjini pale shughuli zetu kubwa ni biashara, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa maana Waziri Mkuu na Watendaji wake Mipango, TAMISEMI watakubaliana nami kwamba, umefika wakati muafaka sasa kwenda kuweka shughuli za biashara kwa maana kongani za viwanda kwenye Jiji la Mbeya, kwa sababu Jiji la Mbeya ni jiji la biashara na Jiji la Mbeya, ni barabara inayopitisha magari mengi na ndiyo lango la *SADC* kuelekea nchi zote za Kusini mwa Afrika, lakini hatuna viwanda Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kujibu tatizo la ajira la vijana wetu kaka yangu Kitila atuletee kongani za viwanda Mbeya, atuletee uwekezaji Mbeya ili tunufaike na jiografia ya Mbeya ilivyo, kwa maana Mbeya ni lango la *SADC,* lakini kuna wakulima wengi wa mazao, basi tupate viwanda ambavyo vinatokana na uzalishaji wa mazao ya kule kama vile viazi, machungwa, ndizi, mpunga ili yale mazao tuweze kuyaongezea thamani na watu wetu waweze kupata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameongea sana hapo dada yangu na mimi ninakazia kwenye suala la miundobinu. Mbeya tunao utalii mwingi sana lakini bado hatujautangaza vizuri kwa sababu ya hali ya miundombinu. Nikiongea *specific* Mbeya Mjini, barabara nyingi za Mbeya Mjini hazipitiki vizuri. Ikiwa wakati wa mvua mifereji inajaa na wakati mwingine inaziba, wakati wa jua vumbi kali. Sasa huwezi kuwa na Jiji la aina kama ya Mbeya lenye wafanyabiashara wengi ambao wanajituma, vijana wanaweza kufanya kazi halafu barabara hazipitiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ninaiomba Ofisi ya Waziri Mkuu watupatie barabara angalau hata kilometa 100 ya barabara za ndani ya Jiji la Mbeya, ninawahakikishia Mbeya itastawi na itashamiri na itavutia utalii na watu wa Mbeya ni wachapakazi wazuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasi tunajiongeza wakitupatia barabara hizo kilometa 100 tumeanza kuandika andiko hivi sasa kupitia viongozi wangu wa Mkoa kwa maana ya Mkuu wa Mkoa, Wakuu wa Wilaya na Mkurugenzi wa Jiji, tumeanza kuandika andiko ambalo kama watatukubalia Ofisi ya Waziri Mkuu kwa maana ya TAMISEMI waturuhusu tukope pesa kwenye taasisi za fedha ili tujenge hizo kilometa 100, kwa sababu Jiji letu linalo uwezo wa kukusanya mapato ya kulipa. Kwa hiyo, tutaandika hilo andiko na tutaliwasilisha kwao walione kama linakidhi vigezo waturuhusu ili sisi tuondoe vumbi Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao uwezo kwa sababu mapato tunayo, tupate mkopo hata wa miaka 20 tunao uwezo wa kulipa, sisi Jiji letu la Mbeya tuisaidie Serikali yetu, wakati wanahangaika kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga miradi mingine ya barabara ya njia nne, barabara za ndani ya jiji tunao uwezo wa kuzijenga kupitia vyanzo vetu vya mapato. Hilo linakuja na nitaomba waliangalie ili tuweze kuiweka Mbeya yetu katika hali nzuri na barabara ziweze kupitika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni ukarabati wa masoko. Mimi ninajikita sana huko kwa sababu watu wa Mbeya ni wafanyabiashara, masoko yetu mengi yana hali chakavu na tumesema tunataka watu wetu wakajiajiri na maeneo ya kujiajiri ni maeneo ya masoko, lakini masoko yetu mengi ya Jiji la Mbeya yana hali mbaya sana. Wakati wa mvua wafanyabiashara wananyeshewa mvua, wakati wa jua wanapigwa na jua. Kwa hiyo, tunaomba kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu watuwekee bajeti kwa ajili ya ukarabati wa masoko yote yaliyoko kwenye Jiji letu la Mbeya ili yafanane na hadhi ya Jiji la Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, Mbeya ni lango la *SADC*, tunaomba pale na sisi siku moja tuje tu-*host* mikutano mikubwa kama wanavyo-*host* wenzetu wa Arusha mikutano – *AICC,* basi na sisi tuwe na ukumbi mmoja pale mkubwa utakaoweza ku-*host* mikutano ya *SADC* badala ya watu kutoka Nchi za Kusini mwa Afrika wanapita kwenye anga letu wanaenda kufanya mikutano Dar es Salaam. Tunaomba sana Wizara kwa maana Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI na Ofisi ya Mipango watusaidie jambo hilo ili siku moja nasi tuweze ku-*host* mikutano mikubwa na hiyo itakuwa njia pekee ya kuutangaza utalii wetu tulionao kwenye Mkoa wetu wa Mbeya na Mikoa yote ya Nyanda za Juu Kusini na Mbeya itakuwa ni *center* ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo michango yangu itajikita sana kwenye biashara kwa sababu sisi pale Mbeya tunafanya biashara. Pia suala la mikopo kwa vijana, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais ametuundia mpaka Wizara ya Vijana na tunaye Waziri machachali kabisa sina mashaka na yeye, hofu yangu inanijia kwa wale watu watakaokuwa wanamsaidia kazi, je ni watu wabunifu? Kwa sababu vijana wanayo staili yao jinsi ya kuishi nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshapata Waziri mzuri, sawa Mheshimiwa Rais amefanya jambo jema ametuwekea pale bilioni 200 kianzio cha mtaji, lakini ninatamani ile bilioni 200 kuizalisha zaidi iwe mara tano ya ile bilioni 200, nayo inawezekana Wizara ya Vijana ijiongeze waweke vikao na hizi taasisi nyingine kwa maana hii Mifuko ya Hifadhi, ina pesa kule, lakini haiwekezi kwenye miradi ambayo itaongeza ajira kwa vijana wanawekeza kwenye kujenga majengo ambayo *return* yake ni ya muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninawaomba kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Vijana ikae na hii Mifuko ya Hifadhi, wana pesa nyingi kule wawekeze kwenye miradi itakayoleta matokeo kwa vijana kujenga mabwawa ya umwagiliaji ambako kule vijana wengi watahitaji kwenye kilimo, kujenga zile skimu za umwagiliaji na masuala ya ufugaji wa samaki, ufugaji wa ng'ombe kule ndiyo kwenye matokeo. Maana yake unakuta Mifuko ya Hifadhi inaenda kuwekeza kwenye majengo ambayo unakuta *return* yake ni ya miaka 100 na wakati mwingine pesa hiyo hairudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kuna hawa watu wa *TFS* na *TANAPA* imekuwa ni tatizo kubwa, ni mgogoro mkubwa sana kila mahali kwenye nchi hii, hii tu inatokana na kwamba wao *TFS* hawazalishi wao ni *regulator* ili kufanya udhibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja nikawauliza watu wa *TFS* kwa nini ninyi mnawaambia wananchi waulinde msitu tu, wataulinda kwa miaka mingapi, badala ya ule msitu utumike kwenye kufuga nyuki, wale wananchi wa eneo husika wakafuga nyuki wakaulinda wao ule msitu, wakawa na chanzo kipya cha mapato badala ya kuwakataza kukata kuni, kukata mkaa lakini wakati huo hamuwapi njia mbadala ya kuzalisha lakini wakati huo *TFS* ataongeza mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana unaona juzi tu hapa niliongea na Waziri Mkuu, watu wa *TANAPA,* watu wetu wa Mbarali wamelima mpunga ekari karibu 2000, wanakwenda kuziteketeza wanasema wamelima maeneo yaliyotunzwa na ni eneo oevu. Sasa unajiuliza, yule mtu alipanda lini mpunga, wao walikuwa wako wapi? Tunamshukuru Waziri Mkuu alilliingilia kati akazuia, lakini wale watu walikuwa wamejiandaa, wanatumia fedha za Serikali kwenda kuteketeza mpunga ambao mwananchi anatakiwa avune baada ya miezi miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaona hili si jambo jema, tunaongea hapa watu wakajiajiri, tutengeneze ajira, watu wajiajiri kupitia kilimo, leo ekari 2000 zimelimwa, watu wanachukua pesa ya Serikali kwenda kuteketeza ule mpunga! Sasa hii ni namna ya kuichonganisha Serikali na wananchi na kuwachonganisha na Rais.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. PATRICK A. MWALUNENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge huyo ndiyo mchangiaji wetu wa mwisho kwa kipindi hiki.

Waheshimiwa Wabunge, nitawataja wachangiaji ambao wataanza kuchangia jioni, tutaanza na Mheshimiwa Emmanuel John Khambay, Mheshimiwa Dickson Nathan Lutevele, Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, Mheshimiwa Clayton Revocatus Chipando, Mheshimiwa Esther Lukago Midimu na wengine watafuatia.

Waheshimiwa Wabunge, nitumie fursa hii kuwapongeza kwa kuwajibika vizuri tokea asubuhi na hivyo ninasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

(Saa 7.02 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)

Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae.

Katibu.

NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

(Majadiliano Yanaendelea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea na majadiliano ya hotuba ya Waziri Mkuu. Tuna wachangiaji ambao wamekwishatajwa. Nitaanza na Mheshimiwa Emmanuel John Khambay, atafuatiwa na Mheshimiwa Dickson Nathan Lutevele na Mheshimiwa Boniventura Kiswaga ajiandae.

MHE. EMMANUEL J. KHAMBAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi ili niungane na wachangiaji

waliokwishatangulia kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye amekuwa akiturehemu sote kwa kutujalia afya njema; lakini zaidi kuniwezesha kusimama hapa kuwawakilisha wananchi wa Jimbo la Babati Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kutoa pole za dhati kwa ndugu zangu wa Jimbo la Babati Mjini, hususani Kata mbili, ambao wamefiwa na wapendwa wao. Kata ya Bagara na Kata ya Maisaka ambapo jana asubuhi mwanafunzi wa kidato cha kwanza alipata ajali na akapoteza maisha na mwenzake na mmoja yuko Hospitali yetu ya Rufaa anaendelea na matibabu kwa kuvunjika mguu. Nitumie nafasi hii pia kutoa pole kwa familia moja ya kada mashuhuri wa Chama Cha Mapinduzi ambaye pia amekuwa akituvisha sare za chama katika Ofisi yetu ya CCM Babati Mjini na Mjumbe wa Baraza la Umoja wa Wazazi wa CCM, Wilaya ya Babati Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumpongeza Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jitihada zake za dhati kabisa za kuwaletea Watanzania maendeleo. Sisi watu wa Jimbo la Babati Mjini tunamshukuru kwa namna ambavyo alituletea fedha nyingi za maendeleo katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii pia kumpongeza Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ndugu yetu Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba kwa ziara zake ambazo amekuwa akiendelea nazo nchini; ziara ambazo zimekuwa na tija katika kutatua changamoto za wananchi. Binafsi ninamshukuru kwa ziara yake katika Jimbo la Babati Mjini ambapo baadhi ya changamoto zilizokuwepo ametusaidia zimeweza kupata utatuzi; hususani katika suala la ardhi ambapo Mheshimiwa Mkuu wetu wa Mkoa Queen Cuthbert Sendiga aliunda timu ya kushughulikia changamoto hiyo na changamoto hiyo imeendelea kutatuliwa. Tunaamini tutapokea ripoti mapema ya utatuzi wa changamoto hiyo na nini itakuwa njia ya kutatua mgogoro huo moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo niendelee kuishukuru Serikali; katika sekta ya elimu sisi watu wa Babati Mjini

tunaishukuru Serikali; kwanza kwa mitaala bora ambayo inakwenda kumwandaa mwanafunzi wa Kitanzania pindi amalizapo masomo kwenda kujiajiri. Ninaendelea kuipongeza hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kama ambavyo wenzangu pia wameipongeza. Ni hotuba ambayo inaakisi maendeleo katika sekta zote nchini. Kama hotuba hiyo na yale yaliyomo mle yatapata kusimamamiwa kwa weledi wa hali ya juu basi ni dhahiri maendeleo yatakwenda kuonekana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maboresho ya mitaala, tunapoelekea 2028 tutakuwa na ongezeko kubwa la wanafunzi. Sisi watu wa Babati Mjini tunatazamia kuwa na ongezeko la mwanafunzi 64,000. Tutakuwa na uhitaji wa madarasa 98. Hiyo kama haitoshi tuna shule ambazo zimezidiwa. Kwa mfano Shule ya Sekondari ya Komoto iliyopo Kata ya Bagara, ni shule ambayo kwa kweli imezidiwa kutokana na *population* kubwa katika kata hiyo, lakini pia kwa sababu mji wetu unakua kwa kasi. Hivyo, tutakuwa na uhitaji pia wa shule nyingine ya kui-*support* shule hiyo; eneo tayari tunalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kuiomba Serikali katika bajeti hii ya awamu hii, katika yale maeneo ambayo tunahitaji mabweni katika shule zetu basi tuweze kupatiwa mabweni. Sambamba na hilo tuna shule mbili ambazo watu wa Babati tunatamani kuona kuwa zinaenda kutoa *advance level*. Shule ya FT Sumaye ina eneo la kutosha; Shule ya Sekondari Wang'Waray tunatamani pia na yenyewe iweze kutoa watoto wa kidato cha tano na cha sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo nitumie nafasi hii kuishukuru Serikali. Tunatambua kuwa jitihada kubwa zimefanyika katika kulipa wakandarasi. Kwa hiyo ninaamini changamoto tulizonazo upande wa *TARURA* za uhitaji wa fedha katika bajeti hii tutakwenda kupata suluhisho. Sisi watu wa Babati tulikuwa tunapokea bilioni 1.8; tunaishukuru Serikali, lakini tumeongezewa imefika bilioni 2.5; tunaishukuru Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hivyo, Mji wa Babati ni mji ambao unakua kwa kasi, ndiyo Makao Makuu ya Mkoa wa Manyara.

Hapa nyuma barabara nyingi zimevurugika kutokana na hali ya mvua. Hivyo, tunaomba ikimpendeza tuweze kuongezewa fedha hizi ziweze ku-*double* ili tuweze kutatua changamoto hizo na hivyo tuendelea kuboresha barabara ambazo zipo katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika fedha za maendeleo tunaomba pia tukumbukwe kupata fedha hizo ili tuweze kufuingua Barabara kutoka stendi mpya kuelekea Chuo cha Uhasibu ambapo ni *Campus* mpya ya Chuo cha Uhasibu cha Arusha katika eneo la Wang'Waray.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii pia kuishukuru Serikali. Katika sekta ya afya tumeendelea kupokea fedha nyingi na Hospitali yetu ya Mji wa Babati imeendelea kuimarika, ikiwa ni pamoja na vifaa tiba, vituo vya afya na zahanati. Tunaishukuru Serikali kwa kututengea bilioni moja na milioni themanini kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Nangara, Zahanati ya Singi ambayo tunatazamia kwenda kupanda kuwa kituo cha afya, lakini na Hospitali ya Mji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kuiomba Serikali, tutaandika ombi maalum kwa ajili ya kupata fedha za kuboresha majengo mengine katika hospitali yetu ya mji kwani Serikali imetupa zaidi ya bilioni 12, lakini bado tuna majengo mingine ambayo ni chakavu katika Hospitali yetu ya Halmashauri ya Mji. Ikumbukwe kuwa Mji wa Babati ni mji ambao unakua kwa kasi, hivyo tunahitaji kuboresha huduma ya afya katika maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongeze kuchangia kuhusu suala la Mfumo wa *NeST*. Ninaipongeza Serikali kwa kuwa na Mfumo wa *NeST* katika kwa ajili ya manunuzi ya umma. Lengo la Serikali ni kuweka uwazi, kuweka usawa katika *competition* ya *tender*, lakini ili pia fursa zilizopo wananchi wote waweze kuzipata au kushiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri kwamba, katika mfumo huu pawepo na ongezeko kidogo katika kubaini wakandarasi ambao mara pengine, wana *tender* zaidi ya moja na wanapopata zabuni zingine, wakati mwingine wanachelewa kukamilisha kwa wakati zabuni ambazo wamezichukua. Wakati mwingine wanaweza kuchukua fedha za zabuni mpya aliyopata akapeleka kuwenda

kukamilisha zabuni nyingine ili apate *certificate* itakayowezesha fedha hizo; apatapo kwenda kumalizia tena mradi mwingine. Kwa hivyo, niombe Serikali kufanya maboresho katika mfumo wetu wa *NeST*, pia kuboresha mfumo wa TEHAMA ili maeneo yote watu ambao wana-*bid* hizo zabuni waweze kupata *access* ya mfumo wetu na kuondoa lawama ambazo pia sio za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ninachangia ni katika suala zima la *force account*...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa muda wako umekwisha, kwa hiyo usichangie lingine.

MHE. EMMANUEL J. KHAMBAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba dakika moja. Katika suala la *force account* ni utaratibu mzuri ambao Serikali inautumia katika punguza gharama kwa kutumia vyanzo vya ndani pia. Kutokana na mfumo huu ninaishauri Serikali kuangalia ni miradi ipi ambayo tunapaswa kwenda kutumia moja kwa moja *force account* na miradi ipi ambayo tunaweza kuwaachia wazabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivyo kwa sababu tusipokuwa na *monitoring* ya majengo au uwekezaji ambao Serikali imetoa fedha ni vigumu kuweza kuona fedha hizo zinatumikaje. Kwa hiyo ni dhahiri kadiri itakavyotupendeza basi tuweze kuwa na mfumo wa ki-*electronic* wenye lengo la kuingiza, kutoa au kuweka udhibiti wa fedha zote ambazo zinakwenda kwenye ujenzi wa majengo ya Serikali. Kuwe na *monitoring* tusisubiri...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Khambay ninaomba umalizie.

MHE. EMMANUEL J. KHAMBAY: ...tusisubiri kufanya *postmortem* wakati mtu ameshakufa. Majengo ya Serikali wakati mwingine ni chakavu, lakini fedha zimetumika za kutosha. Hivyo, tuwe tunafanya ufuatiliaji wa kina ili kuweza kubaini changamoto kuliko kusubiri mpaka tunapofikia mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Nilimwita Mheshimiwa Dickson Nathan Lutevele, atafuatiwa na Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, Mheshimiwa Clayton Rovocatus Kipando ajiandae.

MHE. DICKSON N. LUTEVELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwanza kabisa nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu; na nijielekeze moja kwa moja kwenye kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwa heshima na taadhima niipongeze sana hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo kusema ukweli imesheheni mambo mengi sana. Tayari kwenye hotuba hii Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia, hasa wakipongeza sana kazi kubwa ambayo tayari viongozi wetu wanaendelea kuifanya. Sasa ninaomba nijikite kwenye maeneo matatu muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, ninaomba nimpongeze sana Rais wetu kwa kuendelea kuchapa kazi. Anachapa kazi kubwa na sisi tunaiona. Rais wetu ametuteulia Waziri Mkuu ambaye kwa kipindi hiki ndiye tuliyekuwa tunamtaka; Dkt. Lameck Mwigulu Nchemba, kwa sababu sote tumeona namna anavyofanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo mengi ambayo yamechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wenzangu; sisi kwa ujumla hatuna mashaka na utendaji kazi wa Serikali yetu. Tumeona namna ambavyo Mawaziri wanafanya kazi usiku na mchana, wanafanya ziara wakienda maeneo yote katika idara zote kuhakikisha kwamba Watanzania tunaendelea kupata huduma kama ilivyo katika lengo la Serikali la kutupatia huduma. Tumemwona yeye mwenyewe Waziri wetu Mkuu akienda katika maeneo kadhaa na kutenda kazi kubwa sana katika kuibua na kujibu kero za Watanzania. Sasa, yako maeneo ambayo ninaomba nishauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tukirejea kwenye namna ambavyo tunaona kwenye maeneo yetu; viongozi wakubwa wanafanya kazi kubwa sana lakini wale wanao *deliver* zile huduma kule chini utendaji kazi wao kila Mheshimiwa Mbunge humu ndani anaulalamikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta Afisa wa Kilimo amepewa kishikwambi, amepewa pikipiki lakini akiondoka asubuhi ofisini kwa Mkurugenzi, akifika kule kijijini kuna sehemu maalumu ameweka, pale wanamjua, huwa anafika saa mbili na nusu, atakunywa supu, chakula cha mchana huwa anakula saa nane, hajaenda kule ambako Serikali imemuwezesha na imemnunulia vifaa kwa ajili ya kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa mtindo huu hatuwezi kusubiri hadi Waziri Mkuu aje, au hadi Mkuu wa Mkoa ashuke kule chini. Tutafute namna ya kuwafanyia tathmini ya namna wanavyofanya kazi hawa wataalam wetu. Sisi kule kwetu yako maeneo ambayo wananchi wanahitaji ng'ombe watibiwe; lakini Mganga wa kutibu ng'ombe mpaka apigiwe simu na pengine atoe ratiba mwezi mzima hajakanyaga; ng'ombe wanakufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe ushauri kwa Serikali. Kwa kuwa tuko kwenye mpango wa dira ya miaka hamsini, yawezekana Mheshimiwa Waziri Mkuu tuanze kuangalia; mfumo tunaoutumia wa ajira unamfanya mtu asiwajibike. Kumbe sasa, ikiwezekana tuweke mfumo kwenye dira yetu. Tuweke mfumo wa ajira ya mkataba. Mtu akifanya kazi miaka mitatu, amefanya vizuri, ataendelea. Hajafanya vizuri, wasomi wako wengi nje wanasubiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo huu tunaoutumia sasa hivi ulifaa sana wakati ambao wasomi ni wachache. Sasa hivi kila nyumba ina mtu anamiliki *masters*. Watu wafanye kazi kwa mikataba, wasisubiri kustaafu *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijielekeze katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ameeleza kwamba katika pato la Taifa sekta binafsi inachangia pato la Taifa kwa 70%. Sasa, ni lazima

tuangalie kwamba 70% hii tunaiendeleza vipi? Ninaomba nitoe ushauri kwamba; katika kuziendeleza sekta binafsi, lazima tupunguze utitiri wa mamlaka zinazokwenda kwenye sekta binafsi. Tutengeneze *one stop center*. Kama ni tozo, mtu anatakiwa alipe laki moja na nusu, basi ijumulishwe alipe mara moja, siyo kila baada ya siku imekuja mamlaka hii, kila bada ya siku imekuja mamlaka hii. Hii hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kubwa. Ni kweli kwamba Mamlaka yetu ya Mapato, *TRA*, inapongezwa na imekuwa ikifanya vizuri sana. Kila baada ya msimu wanapotutangazia wanakuwa wamevuka lengo na wameenda asilimia kubwa sana. Ni lazima kama Serikali pia tuangalie, asilimia kubwa hii je, wale kule wanakokusanya kodi maendeleo yao yakoje? Isije ikawa inakusanywa sana kodi, halafu kule wananchi wanafilisika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa mfano, leo hii, wafanyabiashara pale Kariakoo lazima takwimu zipo, tutazame miaka 10 nyuma biashara ilikuwa inafanyikaje? Watanzania walikuwa wana *import* kontena ngapi? Leo hii pale Kariakoo tunaanza kuwashangilia mawinga, kumbe wale mawinga kwa asilimia kubwa ni biashara ya wafanyabiashara wageni, wafanyabiashara wenzetu wenyeji wamefunga biashara wameondoka kwa sababu mitaji yao imekufa. Kwa hiyo ninaomba Serikali, pamoja na ukusanyaji mzuri wa mapato, lazima tuhakikishe ng'ombe huyu anaendelea kupata majani na furaha, anaendelea kufurahi kukusanya kodi. Vinginevyo tutajikuta tunazidi kubomoa kile ambacho tumekijenga jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninaomba nitoe ushauri. Kama ikimpendeza Waziri, ninashauri mamlaka zetu zipite kuangalia namna ambavyo wafanyabiashara wetu nchi nzima wanavyofanya biashara zao. Wachukue hata rekodi ya miaka mitatu nyuma, waangalie ili tunapokusanya kodi tukusanye kwa watu ambao wanafurahi kulipa kodi kwenye nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, ningeomba na ningeshauri; Watanzania wanafurahishwa sana na kasi ya Serikali, wamefurahi, wanafurahi mno, lakini wana jambo moja ambalo

wanaliomba, kwamba kazi kubwa zinafanyika matibabu, afya, barabara na kila kitu. Barabara zetu za vumbi zitengenezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, Watanzania wanaomba mtaani kidogo shilingi iongezeke. Mtu akifanya biashara basi aone hela inapatikana kwa wingi mtaani. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa...

MHE. DICKSON N. LUTEVELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kiswaga, atafuatiwa na Mheshimiwa Revocatus Chipando na Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, ajiandae.

MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nishukuru kwa kunipatia nafasi hii na mimi niweze kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Nimshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha sisi sote kusimama mahali hapa tukiwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nipongeze Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo inaendelea kutatua changamoto za Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri na namna ambavyo anaendelea kushughulikia matatizo ya Watanzania pamoja na Mawaziri wote walioko chini ya Wizara yake, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Manaibu Makatibu Wakuu na Wakurugenzi wa Wizara hii ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya Waziri Mkuu ni shilingi trilioni 12. Kule nje, Watanzania wanadhani ni hela ya mfukoni ya Waziri Mkuu kuweka kwenye mambo yake. La hasha! Inabidi Serikali ijielekeze pia kuwaeleza wananchi kwamba fedha hizi zinatumika kwa namna gani. Mfano, tuna miaka 10 TAMISEMI ilikuwa Ofisi ya Rais na sasa TAMISEMI imerejeshwa Ofisi ya Waziri Mkuu. Maana yake huko TAMISEMI ndiko

kuliko na mzigo mkubwa wa watumishi wa Serikali wanaowahudumia wananchi wa kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo lazima bajeti iongezeke na iwe ya kutosha. Kwa sababu mwananchi huduma nyingi anazipata kwenye ngazi za chini kabisa za Serikali. Kama ni afya, kuna zahanati; watumishi wa zahanati ni wengi. Kama ni elimu, kuna shule, watumishi wa elimu ni wengi. Kama kuna watendaji wa vijiji wako wengi, kama ni kilimo wako wengi. Kwa hiyo, Ofisi ya Waziri Mkuu shilingi trilioni 12 ni fedha nyingi, lakini zinakwenda kutatua changamoto za Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo tulilonalo sasa hivi ni barabara. Niungane na wewe wakati unachangia hapa asubuhi na wengine, tuna matatizo makubwa ya barabara. Tuone namna ambavyo tunaweza kutatua. Nimesoma bajeti ya *TARURA*, ni fedha kidogo bado ukilinganisha na mahitaji ya Watanzania kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulipokuwa unazungumzia jimbo lako lina mjini na vijijini. Mimi nina Mji wa Kisesa pamoja na Mji wa Bujora, hauna barabara kabisa, zimekufa zote. Kuna maeneo ni mji, lakini wananchi wanapaki gari zao kwenye sheli. Kuna maeneo akifariki mtu, wananchi wakibeba mwili kwenda Igeye kutokea uwanja wa Mkapa, wanabeba kwa mabega, si sawa. Kuna maeneo, Mwaholi, hawawezi kufika wananchi. Kwa hiyo kama mtu anabeba mwili kwa mabega kwa karne hii, si sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubaliana kwamba kazi nyingi zimefanyika, lakini bado kuna kazi nyingi zinatakiwa kufanyika. Kwa hiyo, alivyokuwa anachangia asubuhi lazima tuangalie, hii ni miji iliyokua sasa hivi. Mji wa Bujora una barabara moja tu ya lami ambayo imejengwa kilometa 1.7 ambayo inakwenda kwenye makumbusho ya Wasukuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wote wa Bujora, Mji wote wa Kisesa, hauna barabara ya lami hata moja. Hapo mwisho wakati tunakwenda kwenye uchaguzi, tuliahidiwa hapo na Serikali kwamba tutaleta fedha za dharura, wakaleta na barua. Manunuzi yakaandaliwa, mikataba ikaandaliwa, mikataba mpaka leo

haijasainiwa. Tumewaeleza wananchi hapo tutajenga kilometa 1.2, tutajenga kwa mitaro, tutajenga kwa lami. Mambo mengine haya tunatakiwa lazima tuone namna ya kumaliza matatizo ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, humu mjini hata kama utajenga barabara za kupanguka weka *gravel*, kama hujaweka mitaro ni kupoteza fedha. Hatuna sababu ya kuwa tunapoteza fedha kila mwaka badala ya kutengeneza mitaro tukatengeneza barabara ikaimarika angalau hata miaka miwili watu wakaitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapata tabu sana. Barabara za *TANROADS* zinaimarika, barabara za *TARURA* haziimariki, lakini nimepiga hesabu kwa Jimbo la Magu au ukiangalia Mkoa wa Mwanza mzima na mikoa mingine, barabara za *TARURA* ni nyingi kuliko barabara za *TANROADS*. Kwa hiyo, lazima tuangalie kwenye mgawanyo wa fedha hapo ama tutoke kwenye 30% *TARURA*, 70% *TANROADS*, twende *50/50* ili tuweze kutekeleza vizuri barabara zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitoka kona ya Kayenze leo kwenda Shule ya Mwanza *Girls,* kwenda Kayenze kule kilometa 19, wananchi hawapiti. Ukionyeshwa kwa *drone*, unaweza ukashangaa kwamba hii barabara iko wapi. Kwa hiyo, yako mambo lazima tuyakabili, lakini wakati mwingine wilaya zetu zinaungana na wilaya nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Itilima nilitegemea Waziri Mkuu siku amekuja Bariadi kule Itilima, akitokea Bariadi apite Mahaha, tukutanie pale Mwamnemha, hakuna barabara. Kwa hiyo kama anakuja Magu lazima aende Lamadi, si sawa. Kama anataka kutokea Bariadi, kuna ule Mto Gudama, unahitaji daraja, Gudama pale Mahaha kwenda Itubukilo, likipata kuunganishwa; halina gharama zaidi ya shilingi milioni 500. Nimekuwa nikilizungumza humu kila mwaka, lakini tuna barabara ya kutoka Kabila kwenda Nyasato, Nobola, Kabale kwenda Mahaha kilometa 25.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna miaka mitatu hatujaitengeneza hiyo barabara. Kwa hiyo, uhitaji wa fedha za barabara zinahitaji fedha nyingi. Tuangalie Serikali namna ya kuweza kurekebisha, kuongeza

fedha ili tuweze kurekebisha barabara hasa za vijijini. Hizi barabara ni vikwazo vya kiuchumi. Kuna maeneo mchele ulipaswa kununuliwa 1,800 lakini kwa sababu ya barabara, mchele unauzwa 1,300. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba ni vikwazo vya kiuchumi kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo ndipo ninapotaka kujenga hoja yangu. Fedha za tozo tunazozipata shilingi bilioni 1.5 kila jimbo, lazima tuangalie namna ya mgawanyo. Huwezi kulinganisha mwenye dumu la lita 20 na mwenye pipa, namna ya ujazaji wa maji lazima uende tofauti. Kwa hiyo, lazima tuangalie wenye majimbo makubwa, fedha hizi ziongezwe tusilinganishe na majimbo madogo. Ninataka kusema kwamba, tukifanya hivyo hakuna atakayelalamika humu kuhusu ukubwa wa jimbo au ukubwa wa wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kuna fedha inaitwa fedha ya *service levy*. Inaweza kuwa kubwa sana kwa Njombe, inaweza kuwa kubwa sana kwa Jiji la Mwanza, inaweza kuwa kubwa sana kwa Jiji la Dodoma. Fedha hii ni mapato ya ndani. Ushauri wangu…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa malizia, muda wako ulikuwa umekwisha.

MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini fedha hii tusiitenge kama fedha maalum kwa ajili ya kwenda kwenye barabara? Ikawa fedha lindwa, mapato lindwa kama ambavyo yako mapato ya Wizara ya Afya lindwa, ili fedha hizi zikaenda moja kwa moja kutengeneza barabara ambazo zinaonekana ni kichocheo cha uchumi kwa nchi yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kiswaga. Nilimwita Mheshimiwa Clayton Revocatus Chipando, atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, Mheshimiwa Aziza Ally, ajiandae.

MHE. CLAYTON R. CHIPANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Hotuba ya Waziri Mkuu na bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninaipongeza Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Moja, kwa kutupa nafasi vijana. Nimeona Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amemaliza lawama kuhusiana na vijana katika Bunge hili. Asilimia kubwa ni vijana. Ametupa nafasi twende tukawasaidie wananchi. Lawama yoyote ambapo tulikuwa tunalaumu kwamba vijana hatupewi nafasi, haya Bunge hili hapa, tuko wengi kuliko watu wenye umri mkubwa. Sasa huu ni muda wa sisi kuweza kuonyesha Tanzania kwamba vijana tunaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia idadi kubwa ya Mawaziri wamepewa vijana. Mama amemaliza kwenye hilo. Ni muda wetu wa kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, nimeangalia 97% ya Wabunge wote ambao wameongea katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuchangia Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, wameongelea barabara. Tafsiri yake ni kwamba suala la barabara ni tatizo, ni kama janga lingine. Ni kwa nini tusifanye maamuzi Bunge hili tukaliweka suala la barabara kama janga la Taifa na tukatafuta namna bora ya kuweza kutatua shida ya barabara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukimpelekea mkulima mbolea shambani halafu usipompa barabara ya kufikisha hayo mazao ambayo anayatoa shambani kuyaleta mjini, ni sawa na kazi bure. Ukijenga hospitali ya wilaya, usipowapa wagonjwa njia ambayo watapitishwa na hiyo *ambulance* kwenda hospitali, hiyo ni sawa na kazi bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Kigoma Mjini, hospitali ya wilaya ilipojengwa, hakuna barabara ya kuwafikisha watu pale. Ni mashimo, mabonde na kuinama. Tafsiri yake ni nini? Utampeleka mzazi kwenda kujifungua wakati unampeleka unampiga kwenye

mashimo, afike kwanza atengenezwe kwanza nyonga uliyovunja kwenye mashimo; haiwezekani. Lazima tufanye maamuzi. Vijana tuko humu ndani, tufanye maamuzi kuhusiana na suala la barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimwambie ukweli Mheshimiwa Waziri Mkuu. Suala la *TARURA* kuna mtego huo huwa wanatuingiza; mkenge. Ukisikia wataalam wanakushauri upeleke barabara ya vumbi kwenye jimbo lako, tafsiri yake ni kwamba wamejitengenezea kitengo cha kuwa wanakutana na mkandarasi kila mwaka kuchukua 10%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu utatengeneza barabara ya vumbi mwaka huu kwa shilingi milioni 400, ikifika mwezi Desemba mvua zikinyesha, zinazoa milioni 400 yote zinaipeleka ziwani au kwenye mto. Mwaka kesho wanatenga tena milioni 400 kwa ajili ya kujenga barabara ile ile. Wale watu wa *TARURA* wanakutana na mkandarasi kila mara wanachukua 10%, maisha yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muda wa kufikiria kujenga barabara za lami na tuachane na barabara za vumbi. Wamerahisisha lugha kuiita barabara za vumbi. Mzee ni barabara za vumbi wakati wa kiangazi, ikifika wakati wa masika ni barabara za tope. Nadhani tuzibadilishe jina tuziite barabara za tope.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Kigoma Mjini, tulipata ufadhili wa Nchi ya *Belgium* mwaka 2018 mimi nikiwa Diwani. *Belgium* walikubali kutujengea kilometa 42 za barabara za *pavement blocks* ambazo zingeenda kufuta shida yote ya barabara katika Jimbo la Kigoma Mjini, lakini mpaka leo hakuna kinachoendelea na mkandarasi alikuwepo, upembuzi yakinifu ulishafanywa na kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilienda kwa Mheshimiwa Profesa Shemdoe, nyumbani kwake, sikumkuta. Nilienda kwake sikumkuta, nikauliza hata shemeji yangu nae sikumkuta. Nilikuta watoto wake, maana niliona sura zinafanana na Profesa Shemdoe mtupu, nikajua ni watoto wake. Lengo nilikuwa ninataka nikae na Profesa Shemdoe tuongee kifamilia kuhusiana na barabara za Kigoma Mjini. Jimbo la

Kigoma Mjini ndio jimbo la mjini ambalo lina barabara za vumbi kuliko jimbo lolote duniani, siyo Tanzania, dunia nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nikuhakikishie, ukienda Kata ya Mwanga Kaskazini, kuna barabara inaitwa Barabara ya Serengeti ambayo inaunganisha Kata ya Mwanga Kaskazini na Kata ya Gungu. Hiyo barabara ina makorongo ambayo ukifika Mheshimiwa Waziri Mkuu, utasema *Inna lilahhi wa inna ilahhi raji'un*. Ukienda Kata ya Buzebazeba, kutokea uwanja wa *Lake* Tanganyika, ukipita barabara hiyo ambayo inaenda ku-*connect* mpaka soko la Buzebazeba, ina-*connect* Kata ya Rusimbi, ina-*connect* Kata ya Kasingirima, ina-*connect* Kata ya Majengo, ina-*connect* Kata ya Machinjioni, barabara zote hizo ni vumbi tupu. Ifikie hatua watusaidie watu wa Kigoma na sisi tupate barabara ambazo zitaenda kuchochea maendeleo ya mji wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunaenda pale na Mheshimiwa Waziri Mkuu ninadhani kesho kutwa kwenda kukutana na wafanyabiashara kutoka Congo, Burundi na sehemu nyingine tofauti tofauti. Wanaenda kuona aibu iliyopo pale Kigoma Mjini. Wanaenda kushuhudia barabara za vumbi zilizotaradadi pale ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu wakishaona hizo fursa, baadaye wataanza kuzinunua nyumba za wapiga kura wangu kwa bei ndogo kwa sababu nyumba iko kwenye korongo, utamuuzia nani bei kubwa? Watazinunua bei ndogo, baada ya kuja kujenga barabara, wananchi wetu watakuwa wamepoteza *opportunity*. Huu ni muda, wameniamini, kibarabara, mtoto wao. Nimekuja kuwaombea barabara kwa ajili ya Jimbo la Kigoma Mjini katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. watusaidie barabara, watupe barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tukifanya maamuzi ya pamoja Wabunge wote, ninawaambia ukweli; mama alivyokuja kuhutubia Bunge hapa, Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wetu, alivyotaja tu barabara, Bunge zima likapiga makofi, akajua hapa kuna tatizo na ndiyo maana ameongeza hela kwenye upande wa barabara, lakini

bado tunaomba sana utusaidie watu wa Kigoma tuweze kupata barabara. Hiyo ni tabu kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida ya pili, mafuriko. Jimbo la Kigoma Mjini limekumbwa na mafuriko. Yapo mafuriko ambayo yanatengenezwa na Mwenyezi Mungu; Mwenyezi Mungu analeta mvua nyingi, mafuriko yanatokea. Hilo hatuwezi kumlaumu mtaalam yeyote, lakini yapo mafuriko ambayo yanasababishwa na uzembe wetu sisi ambao ni viongozi tuliopewa nafasi ya kuwaongoza wale wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, sehemu ambapo maji yangefuata mtaro yangeenda ziwani moja kwa moja, hujajenga mtaro. Tafsiri yake maji yanachagua sehemu ya kupita, aidha yachague sebuleni au chumbani kisha yapitilize yaendelee na shughuli zake. Kwa hiyo, kuna makosa mengine hata mimi kwenda kuwapa watu pole ninaona aibu. Huwezi kwenda kuwapa watu pole sehemu ambapo ungejenga mtaro mkubwa, maji yasingeleta mafuriko kwenye nyumba za watu. Siwezi kwenda na nikimwona Waziri anakwenda aende yeye, wakamzomee yeye mwenyewe, mimi siwezi kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka niende na Mheshimiwa Profesa Shemdoe, twende tukazindue mitaro, tukazindue barabara, hapo tutashirikiana kwa pamoja. Ninawaomba sana, namwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu atusaidie watu wa Kigoma tuweze kupata barabara, lakini pia suala la mafuriko ya Bwawa la Katubuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Bwawa linaitwa Katubuka. Hili Bwawa liko miaka yote tangu tumezaliwa, halikuwahi kufurumia kiasi kile, lakini wataalam wetu walitengeneza mitaro wakaelekeza maji yote ya mji kwenye hilo bwawa. Sasa hivi limebadilika limekuwa ni bwawa ambalo linaleta mafuriko kwenye Mji wetu wa Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna mtu alikuja kutudanganya siku aliyosema ni uongo au ni ukweli akasema Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameelekeza shilingi bilioni nne kwa ajili ya kwenda kutengeneza mtaro wa kuyatoa maji pale Katubuka. Tukamwona

mkandarasi anaanza kazi, nami nikaenda kuitisha mkutano, nikasema mnaona kazi ya mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mwezi mmoja na nusu mkandarasi ametoa vifaa vyote anasema hana hela. Nikamuuliza shida ni nini? Akaniambia pesa nilizokuwa ninazitumia kujenga hapa ni pesa ambazo nilipewa kwa ajili ya Barabara ya kutoka Katonga kwenda Ujiji. Sasa barabara ile inatakiwa kwisha na hapa siwezi kuendelea kwa sababu hela ya huu mtaro sijapewa. Mzee wangu Prof. Shemdoe, anisaidie. Mimi ni mmoja kati ya mashabiki wake, ninamkubali, anatusikiliza, tunamheshimu, anatuheshimu na hata 2030 akichukua fomu yoyote tuko nyuma yake mzee wangu.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Malizia kwa kuunga hoja.

MHE. CLAYTON R. CHIPANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamalizia suala la mwisho, ni suala la fidia. Wananchi wa Kata ya Majengo pamoja na Machinjioni walikubali kupisha upanuzi wa *airport* pale Kigoma Mjini na wakazuiliwa baada ya kufanyiwa *valuation*, wakazuiliwa wasijenge tena kwenye nyumba zao kwa sababu wanasubiri kulipwa. Sasa tunakwenda mwaka wa pili; tofali liking'oka mtu anashindwa kurudishia kwa sababu anaamini kwamba hilo tofali litaongeza gharama ambayo hatalipwa. Ni muda umefika sasa twende tukawalipe wale wananchi fidia pale Kigoma Mjini ili maisha mengine yaweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo machache, ninamalizia na hili la wavuvi mzee wangu; ninaomba Mwenyekiti wangu anisaidie Wabunge wenzangu si wanaona kama kidogo mambo ni mazuri?

MWENYEKITI: Malizia, ninaomba umalizie kwa kuunga mkono hoja, ninadhani nimekuongezea muda wa kutosha.

MHE. CLAYTON R. CHIPANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, sawasawa kwenye suala la wavuvi, ninaunga sana mkono hoja baada ya kuona Ziwa Tanganyika ni moja ya...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chipando.

MHE. CLAYTON R. CHIPANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa nilikwishamwita Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, atafuatiwa na Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally na Mheshimiwa Asha Ramadhani Baraka, ajiandae.

MHE. ESTHER L. MIDIMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri iliyosheheni matumaini ya Watanzania. Mheshimiwa Waziri Mkuu amefanya kazi nzuri sana. Tunamwona anazunguka, anaenda kwenye mikoa, anapita wilaya zote, anasikiliza kero za wananchi na kuzitatua. Hongera sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini pia ninawapongeza Mawaziri wote na Manaibu Waziri kwa kazi nzuri wanazofanya, Mwenyezi Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, anafanya kazi nzuri sana. Mheshimiwa Rais ni simba jike unayelinda watoto wako, unafanya kazi nzuri sana. Mwenye macho haambiwi tazama. Mheshimiwa Rais ni nahodha, usibabaishwe na mtu, kanyaga twende. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mkuu wangu wa Mkoa, Anamringi Macha, anafanya kazi nzuri sana pamoja na *cabinet* yake anafanya ziara majimbo yote kukagua miradi ya maendeleo lakini pia na kusikiliza kero za wananchi na kuzitatua. Hongera sana Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa Simiyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuboresha hospitali ya Muhimbili. Mheshimiwa Rais ameboresha hospitali ya Muhimbili, upasuaji wa kichwa unafanyika

hapa hapa Tanzania Muhimbili, upandikizaji wa figo hapa hapa Muhimbili, upasuaji wa moyo unafanyika hapa hapa Muhimbili, amepunguza adha ya wananchi kufuata matibabu India, vipimo vyote vipo. Hongera sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri unazozifanya mama; wewe ni simba jike hakuna mtu atakayepinga. Mwenye macho haambiwi tazama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa mkoa wetu ametupatia fedha tumejenga hospitali ya mkoa. Pia, akatutengea zaidi ya shilingi bilioni saba tukajenga majengo manne; jengo la kutakasa vifaa, jengo la kufulia, jengo la mochwari na jengo la mama na mtoto tena ghorofa la kisasa limekamilika na linafanya kazi; Mheshimiwa Rais Mungu akubariki. Ombi langu kwa Hospitali ya Mkoa Simiyu haina uzio; tunaiomba Serikali itupatie fedha ili tuweze kujenga uzio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais wangu kipenzi, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri. Ametutengea shilingi bilioni saba tukajenga Hospitali Mpya ya Itilima pamoja na kununua vifaa tiba, hongera sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Itilima nayo haina uzio. Niombe Serikali ifanye utafiti hospitali zote za wilaya na za mkoa ambazo hazina uzio itoe fedha zijengewe uzio kwa sababu ni hatari sana hospitali kukaa bila uzio. Utoroshwaji wa dawa na vifaa tiba ni rahisi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ninaendelea kuomba kwa Itilima, tuna Kituo cha Afya cha Zagayu; hakina wodi za kulaza wagonjwa. Tunaiomba Serikali itusaidie fedha ili tuweze kujenga wodi; kuna ujenzi wa Kituo cha Afya Itilima Mwanhunda unaendelea, lakini unasuasua. Tunaiomba Serikali itupatie fedha ili tuweze kukamilisha ujenzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea na pongezi kwa Hospitali ya Busega, Wilaya mpya ya Busega tumejengewa hospitali mpya, tumetengewa shilingi bilioni nne na Mheshimiwa Rais. Ombi langu kwa

Busega kuna Kituo cha Afya cha Mkula jengo la *OPD* limekamilika, lakini halina wodi za kulaza wagonjwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali iendelee kututengea fedha ili tuweze kujenga wodi katika Vituo vya Afya vya Mkoa Simiyu ambavyo havina wodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru Serikali kwa kuboresha jengo la hospitali ya Maswa, *theatre* nzuri ya kisasa, wodi zote zimejengwa na jengo la *ICU* limejengwa. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais, ila nina ombi Kata ya Buchambi na Kata ya Sukuma; hatuna vituo vya afya. Kata hizo zina wakazi wengi tunaomba tupatiwe fedha ili tuweze kujenga vituo vya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru kwa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Bariadi mpya alitupatia shilingi bilioni nne. Hongera sana Mheshimiwa Rais na kuendelea kuboresha hospitali ya Meatu. Kuna Kituo cha Afya cha Mboboko kiko kwenye ilani. Tunaiomba Serikali itupatie fedha ili tuweze kujenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maji ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutupatia shilingi bilioni 440 kwa ajili ya mradi wa maji. Mradi wa Maji wa kutoka Ziwa Victoria kuja Mkoa wa Simiyu na wilaya zake; Busega, Bariadi, Itilima, Maswa na Meatu. Mradi huo umeshaanza kujengwa, lakini bado unasuasua. Ninaiomba Serikali ije na majibu ni lini mradi huu utakamilika kwa sababu wananchi wa Simiyu wanasubiri kwa hamu maji ya Ziwa Victoria ili iweze kutimiza azma ya Mheshimiwa Rais ya kumtua mama ndoo kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaenda ujenzi; kuna Barabara ya kutoka Bariadi kwenda Itilima, Meatu, Sibiti na Singida kwa Waziri Mkuu, hii barabara ni *shortcut*. Hii barabara ikikamilika ijengwe kwa kiwango cha lami itafungua uchumi, lakini na barabara nyingine ya kutoka Bariadi kwenda Magu na hiyo tunaomba ijengwe kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kununua ndege, mpaka sasa ndege zimefika 16, hongera sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu sasa ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Mkoa Simiyu uko kwenye ilani. Eneo tayari limeshatengwa liko Igegu Sapiwi. Hilo eneo liko jirani na Mbuga ya Serengeti na Ngorongoro. Uwanja huo ukijengwa ukikamilika hata watalii watakuwa wanashuka pale. Hata sisi wananchi wa Mkoa wa Simiyu tuna hamu sana uwanja ule ukamilike. Sisi ni wachapakazi, wakulima na wafanyabiashara tutapanda ndege: ndege zitajaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu 10% ya akina mama, vijana, na walemavu. Bahati nzuri Wilaya ya Itilima walipata kibali fedha zipitie benki na akina mama, vijana na walemavu wakaendelea kukopa. Wilaya ya Itilima imefanya vizuri sana. Ombi langu; ninaiomba Serikali itoe vibali na wilaya zingine ili fedha zile ziwe zinapitia benki. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Midimu, hebu malizia.

MHE. ESTHER L. MIDIMU: Nimalizie?

MWENYEKITI: Muda wako umekwisha.

MHE. ESTHER L. MIDIMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninampongeza mama yetu Mheshimiwa mama Chatanda, mwanamke wa shoka ametuunganisha wanawake, anatupenda na anatushauri vizuri. Mama siyo siri unachapa kazi, tunakupenda mama yetu wanawake wote unatuunganisha tunapendana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tuna jukumu la kukumbushana. Ninaomba Waheshimiwa Wabunge tusikilizane. Tuna jukumu la kukumbushana; tukisema kwamba muda

wako umekwisha basi jitahidi hata kumalizia tu kwa haraka siyo kuanza hoja nyingine mpya kwa kirefu na tukumbushane kwa mujibu wa Kanuni ya 70(13) na (14), kama kuna mambo kuweza kuyamalizia kwenye mchango wako bado una nafasi.

Fungua kishikwambi ingia, toa maoni yako kwa maandishi; bado unayo nafasi hiyo siyo kwamba umeipoteza kabisa. Ili tuweze kutunza muda na tuweze kukamilisha mpangilio ambao wote tumewapanga siku ya leo.

Waheshimiwa tunaendelea, nilimwita Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally atafuatiwa na Mheshimiwa Asha Ramadhani Baraka na Mheshimiwa Kellen Rose Rwakatare ajiandae.

MHE. AZIZA S. ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuongea, lakini kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa siku ya leo kusimama hapa jioni hii na kuweza kuongea machache ambayo niko nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri yenye mpangilio na yenye utaratibu mzuri uliotulia. Pia ninampongeza katika hotuba yake mwanzo tu alipoanza alianzia kuongelea kuhusu masuala ya afya. Waziri Mkuu nina imani na Mheshimiwa Rais katika Ilani ya Uchaguzi aliahidi kuwajali wananchi wake katika idara ya afya hasa kwa magonjwa sugu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii nimesimama hapa ninapenda niseme katika Mkoa wetu wa Tabora tunasimama kifua mbele wa kumpongeza Rais wetu na kumshukuru mpaka hivi sasa tumeshapokea mashine za kusafisha damu na mashine za kusafisha figo. Ahadi yake amekamilisha ndani ya siku mia moja. Hongera sana Rais wetu tunakupongeza kwa kazi kubwa unayofanya na tuna hakika uongozi wako umetoka kwa Mwenyezi Mungu. Ndio maana unayafanya haya ambayo unayoyafanya kwa kuwa Mungu anakuongoza kwa yale mema ambayo unayafanya na nia yako ni njema na ni nzuri kwa wananchi wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niwashukuru wanawake wa Mkoa Tabora kwa kunichagua na kuniamini na kunipa kura za kutosha. Pamoja na hayo niweze kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa pesa alizotenga kwa wanawake ili waweze kupata mkopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tumefanya zoezi moja kubwa hapa Dodoma kupitia Mbunge mwenzetu Neema kwa kuwashukuru sana *CRDB Foundation* kwa Dr. Tuli msichana ambaye ni mwanamke; amefanya vizuri kupitia *foundation* yake. Amemuunga mkono Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa Dodoma wanawake wamepata shilingi bilioni moja wanazokwenda kufanyia kazi za mkopo; ambao mkopo huo hautakuwa na riba hata kidogo. Ninapenda kuwaambia wanawake wa Tabora tumeanza na Dodoma kinachofuata ni Tabora. Huyo ndio Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, mama yetu kiongozi wetu jemedari wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wetu wa Tabora katika kipindi ambacho Rais ameingia madarakani ameweza kupeleka pesa katika halmashauri zetu shilingi bilioni 12.2 hizo ni za vifaa tiba, lakini amepeleka shilingi bilioni 37 ambazo hizo ni kwa ajili ya majengo. Mheshimiwa Rais ameyafanya haya kwa ajili ya kuwajali wananchi wake katika huduma za afya, lakini Waziri Mkuu huyu yeye alikuwa ni Waziri wa Fedha na aliyaona haya na yeye pia alielekeza pesa hizo kwa namna yoyote kuweza kuzitafuta ili zikafanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapata shida sana na lazima niseme ukweli pesa nyingi zinapita kwenye halmashauri zetu, lakini bado shida ipo kule katika hospitali zetu za chini. Je kuna utaratibu gani Mheshimiwa Waziri Mkuu wakaangalia hili dudu la halmashauri, pesa hizi kama za Wizara ya Afya ziweze kutafutiwa mfumo mzuri, akafanye kazi huduma kwa wananchi wale wa chini ikafanye kazi vizuri na huduma ipatikane bila malalamiko yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila fedha utakayoiona inatengwa katika halmashauri zetu. Kwa hiyo, hili ni tatizo ambalo kwa nini iende moja kwa moja kwenye halmashauri kule wanawawekea mzigo

mkubwa zaidi. Tuje tubadilishe mfumo sasa tuweke mzuri ambao utapeleka kule na kwa usimamizi ambao utakuwa mzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani Serikali ina imani kubwa na halmashauri na hata sisi Wabunge tuna imani kubwa na halmashauri zetu, lakini je, kwa utaratibu huu huduma kule kwa wananchi wetu zitafika kwa utaratibu mzuri? Tunajua wafanyakazi wanafanya kazi yao vizuri, lakini lazima tuseme ya kwamba waweze kupata usimamizi uliokuwa imara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichangie kuhusu madaktari wetu bingwa na madaktari na manesi ambao wanahudumia binadamu. Leo ningependa kuwa balozi wa kujipa mimi mwenyewe ubalozi wa madaktari. Tunao madaktari bingwa katika nchi yetu; lakini madaktari wetu bingwa hao stahiki zao zikoje? Ni ndogo sana. Madaktari wetu bingwa huwezi kukutwa sehemu yoyote wanapewa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wanasiasa tuna nafasi yetu, wacheza mpira wana nafasi yao, wasanii wana nafasi yao, lakini hawa wanaojali wananchi, wanaotusaidia tukiwa na afya legelege humu ndani mtu akipata tatizo lazima akimbie pale hospitali. Je, wale nani anayewasimamia na kuwasemea? Kweli kazi ya udaktari ni kazi ya wito, lakini lazima tukubali tuwajali sasa hivi na kuwasemea na kuangalia stahiki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wetu wamesoma, vijana wetu wamesoma miaka minne Serikali imewahudumia lakini bado mapato yao ni madogo. Tukichukua tu *overtime* ya daktari ambaye yuko hapa Benjamin leo, ule muda wake wa *overtime* analipwa shilingi elfu ishirini na mbili, *overtime* yake ni elfu ishirini na mbili hapa Benjamin. Hapo ana mgonjwa ambaye ni wewe, mimi au ndugu yako. Yeye anamfanyia *operation* muda wa kazi umekwisha, lakini anaokoa uhai wake akitoka pale anapewa elfu ishirini na mbili ndiyo *overtime* yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo umepita na hatutoweza kuvumilia. Nilikuwa ninaomba wakija kuja kutoa majibu waje kueleza namna gani tunawainua madaktari wetu. Hawana nyumba hata za

kukaa, nyumba ni chache. Mheshimiwa Waziri Mkuu ninamwamini ni kijana anayefanya kazi na anayebuni mambo mengi kwa nini tusiwajengee nyumba madaktari wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Benjamin Mkapa hapa kuna nafasi kubwa ambazo tunaweza kutafuta hata ubia na sehemu nyingine yoyote wakafanyiwa hata *apartment* waweze kukaa wakiwa karibu. Hiyo Mheshimiwa itawasaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliwaahidi madaktari vijana wetu waende wakasome, watakaposoma tutawalipia ada na hatutowadai tena, Serikali itawasomesha, lakini sasa hivi kwenye kile kidogo cha mshahara anachopata hapo hapo anaenda kukatwa pesa itakayolipa ule mkopo ambao amesoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linasikitisha sana kwa vijana wetu madaktari wetu na manesi wetu. Wengi tunachukua nafasi hii kuweza kuwalaumu kwa kila siku hakuna tutakaowapa nafasi. Mheshimiwa Waziri Mkuu unashindwa nini siku moja ukawaandalia vijana wetu madaktari bingwa, ukakaa nao na kunywa nao hata maji; wao soda hawanywi kwa sababu wanaogopa sukari, lakini hata maji ya mia tano watakunywa. Kaa nao wasikilize shida zao watatulie matatizo yao. Utapata nafasi yako kwenye chama na Serikali, lakini pia utapata nafasi yako kwa Mungu pia kwa ajili ya kuwasikiliza watu na shida zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wa Tabora pia wameniagiza. Hawajapata pesa zao ambazo wameuza tumbaku, bado hawajalipwa pesa zao. Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuwalipa hawa wakulima wa tumbaku pesa zao wanazodai. Hivi sasa wananunua tumbaku nyingine ambayo tayari wana madeni ambayo bado wanadaiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue nafasi hii kuunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Aziza Ally. Nilimwite sasa Mheshimiwa Asha Ramadhani Baraka, atafuatiwa na Mheshimiwa

Kellen Rose Rwakatare na Mheshimiwa Kijakazi Yunus Mohamed ajiandae.

MHE. ASHA R. BARAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kabisa ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii na pia ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa salama na kuendelea na shughuli za Bunge kama kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakishukuru Chama changu Cha Mapinduzi hususan Kamati Kuu bila kusahau UWT Taifa - Mkutano Mkuu wa UWT ambao uliniwezesha kunipa kura nyingi chini ya Mwenyekiti wetu, Mama Mary Chatanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Raisi wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuweza kuiongoza nchi yetu mpaka tumefikia hapa tulipo na Bunge linaweza kufanya kazi zake kama kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumpongeza Waziri Mkuu kwa ziara zake ambazo amekuwa akizifanya mikoani. Ningependa zile ziara ziendelee ambapo wananchi wengi wanatoa kero zao kwa Waziri Mkuu kwa kuonana naye hapo kwa hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninarudia mapendekezo ya bajeti ya hotuba ya Waziri Mkuu, ninaipongeza Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwanza kabisa ninasema Serikali yetu ambayo imejenga shule pale *Kibaha DC*, hii shule ni ya watoto wenye ulemavu wenye uhitaji maalum, ni shule ya *primary* ambayo inakwenda kwa jina la *Kawawa Primary School*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumpongeza Waziri wa TAMISEMI kwa kuhakikisha kwamba ile shule imekuwa vizuri na iko nzuri na salama kabisa; ni shule ya *boarding school* inategemea kuingiza watoto 495 wa *boarding*. Sasa niiombe Serikali, kwenye bajeti hii kumekuwa na malalamiko sana ya watu wenye uhitaji maalum. Ile shule kwa sababu ni *primary school*, waweze kuwekewa vifaa vya kisasa na rafiki ili waweze kufanya mafunzo yao pale. Hata

ikiwezekana waongezewe na chuo cha pili cha *VETA* ili waweze kujifunza pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niko hapohapo *Kibaha DC*, ninampongeza Waziri wa Kilimo kwa mikakati yao ambayo ameiweka na Mheshimiwa Waziri Mkuu ameichakata vizuri. Pale *Kibaha DC* kuna kilimo ambacho kinaanzishwa, ni kilimo cha kisasa, ni kilimo cha mbogamboga ambacho kitasaidia ajira kwa vijana wetu na wanawake. Ninaomba tu kwamba kile kilimo cha mbogamboga kinategemea kulisha Mkoa wa Dar es Salaam na Kibaha yenyewe, hususan Mkoa wa Pwani na mikoa ambayo iko karibu. Ninaomba tu kwamba waweze kupatiwa ile mikopo ya 10% bila masharti yoyote hawa akina mama pamoja na vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale mbogamboga zitalisha Mkoa wa Dar es Salaam ni eka karibu 2,000 ambazo zimetengwa na Wizara ya Kilimo. Kwa hiyo, ninaomba hizi eka hizi 2,000 zigawiwe kwa uwiano, nikisema tuhakikishe kwamba vijana na wanawake wanapata na wanatengeneza hicho kilimo, kitakuwa tumenusuru ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaongezea jambo lingine ambalo liko chini ya taasisi zisizokuwa za Serikali. Taasisi Zisizokuwa za Kiserikali *(NGOs)* kutokana na matatizo ya vita na nini imekuwa ni ngumu kupata misaada na kuweza kusaidia jamii. Ninamwomba Waziri Mkuu afanye michakato kupitia hizi taasisi za mashirika tofauti tofauti ya umma au taasisi hizi za kifedha za kibenki na nini ziweze kuzisaidia hizi *NGO*. Kuziokoa zisiweze kufa na ziendelee kufanya kazi zake kama kawaida za kusaidia jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaenda kwenye *AFCON* ambayo inategemewa kufanyika mwaka kesho. Mwaka kesho kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu ni karibu sana. Ukiangalia barabara ambazo zinakwenda kwenye *AFCON*, kwenye viwanja ambavyo vimetumia pesa nyingi sana, barabara bado hazijakuwa nzuri na siyo rafiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hata Barabara ya Uwanja wa Mkapa kama unatoka Dar es Salaam pale kwenda Uwanja wa

Taifa, utaona kuna makontena mengi sana ambayo ni hatari kwa wageni wetu ambao watakuja kwenye *AFCON*. Tunaomba barabara hiyo iachwe wazi na yale makontena yatafutiwe sehemu nyingine ambayo ni rafiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazungumzia pia hivi vilabu vyetu. Vilabu vyetu vimekuwa vikicheza mashindano ya kimataifa, tunamshukuru Mheshimiwa Rais kutoa lile goli moja la mama, imekuwa ikivipa motisha hivi vilabu vyetu vinaweza kufanya vizuri na kujitahidi kuweza kusonga mbele kwa ajili ya Taifa letu. Pia, nilimwona pale Mheshimiwa Makonda alikuwa amekaa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, nikakumbuka kitu. Mheshimiwa Makonda alivyokuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam alitoa kiwanja kwa *Young Africa* na ameacha kumbukumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninamwomba tu Waziri Mkuu kwa heshima na taadhima. Waziri Mkuu ni mwanamichezo, lakini ninamwomba, Klabu ya Simba huko nyuma (zamani) ilikuwa inafanya mazoezi Jangwani, vilabu vingi vilikuwa vikifanya mazoezi Jangwani, kuna Tololo sijui *Pan - African* na nini, pale karibu na Klabu ya Yanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Yanga wamepata uwanja mwingine na wamepewa hati hapohapo. Kwa hiyo, ninamwomba Waziri Mkuu ni mwanamichezo, afumbe macho na aweke historia kwenye *Simba Sports Club* na yeye atupe uwanja wetu kama alivyofanya Mheshimiwa Makonda, yeye ni Simba lakini hakuwa na ubaguzi wowote, akasema hii ni michezo kwa ajili ya nchi yetu. Kwa hiyo, ninamalizia na ninakuomba kwa heshima na taadhima, tulishaandika barua Serikalini, kiwanja kile Simba hawajakabidhiwa na timu nyingine. Kwa hiyo, tunaomba Simba nao wapewe kiwanja ambacho kitaweka kumbukumbu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Asha Baraka. Nilimwita Mheshimiwa Kellen Rose Rwakatare, atafuatiwa na Mheshimiwa

Kijakazi Yunus Mohamed na Mheshimiwa Christina Solomon Mndeme ajiandae.

MHE. KELLEN R. RWAKATARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha hapa siku ya leo na kunisimamisha hapa mbele yenu ili niweze kuchangia kwenye hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ni kwa mara yangu ya kwanza ninasimama kwenye Bunge hili Tukufu ili niweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninachukua nafasi hii kuishukuru Halmashauri Kuu ya CCM Taifa ikiongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mwenyekiti wetu kwa kuweza kunichagua na kuniamini ili niweze kugombea Ubunge kwenye Jimbo la Mlimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua nafasi hii kuwashukuru Wananchi wa Jimbo la Mlimba kipekee kwa kumchagua Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kura nyingi sana za kishindo wakati wa uchaguzi ule ili awe Rais wetu. Pia, ninawashukuru wananchi kwa kunichagua mimi kuwa Mbunge wao wa Jimbo la Mlimba. Ninawaahidi kwamba sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa. Pia, ninampongeza kwa ziara ambazo anazifanya, ni ziara za tija, ziara zenye kuonesha vitendo. Kwa kweli Mheshimiwa Waziri Mkuu anaenda *site*, anatufundisha hata sisi tuweze kwenda *site* na kusikiliza kero za wananchi na kuzitatua pale tunapoweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumpongeza sana, sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu, kwa juhudi kubwa anazozifanya kutuletea maendeleo kwenye nchi yetu hususan kwenye Jimbo langu la Mlimba. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ametuletea bima ya afya zaidi ya watu 2,800 wameshapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru pia tumeletewa ajira 158 ambazo ni ajira kwenye *section* ya elimu na afya, kwa hilo tunashukuru. Mikopo ya 10%, Jimbo la Mlimba tumepata zaidi ya shilingi bilioni moja kwa 10%. Hizo zimeenda kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Kutokana na pesa hiyo ambayo wamepokea, ajira zaidi ya 10,000 zimepatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote hayo, Mlimba tuna changamoto, changamoto yetu ni barabara, barabara, barabara. Kama vile ambavyo wenzangu wameshasema, hili ni janga la kitaifa lakini nikiongelea Jimbo la Mlimba, barabara hii ni kipaumbele katika ukuaji wa uchumi wa Taifa letu. Barabara ya kutoka Ifakara – Mlimba – Njombe ni muhimu kwa sababu inaunganisha mikoa miwili ambayo ni Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Njombe. Kwa hiyo, imebeba uchumi wa mikoa hii miwili na ndiyo inayotumika kusafirisha mazao yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyojua, wananchi wa Mlimba na wananchi wa Njombe uchumi wao unategemea ukulima, tunalima mchele ambao ndiyo mpunga. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali iiangalie barabara hii kwa umuhimu wake ili iweze kujengwa kwa haraka zaidi kutokana na umuhimu wa barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyoongea sasa hivi barabara imepata mkandarasi, mkandarasi yuko *site* lakini anadai *advance payment*. Ninaiomba Serikali impatie *advance payment* ambayo imebaki, imempatia kidogo *partial payment*. Kwa hiyo, tunaomba aweze kupata *full payment* ile ya *advance payment* aweze kuanza kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa barabara za *TARURA*, ninapenda kuishauri Serikali iongeze pesa kwenye bajeti ya *TARURA* ili kuhakikisha barabara za vijijini nazo zinapitika kwa wakati wote. Pia, halmashauri niwashauri *TARURA* wapate pesa za dharura ili barabara hizi zilizoathiriwa na mvua hizi zinazoendelea kunyesha ziweze kutengenezwa angalau pia ziweze kupitika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa kwenye Jimbo langu la Mlimba, Barabara ya Mpanga – Kikowe – Ngalimila ambayo

inaunganisha Wilaya ya Mlimba na Wilaya ya Malinyi, haipitiki. Barabara ya Namwawala – Mofu haipitiki. Barabara ya Kamwene – Matema – Uchindile haipitiki. Barabara ni nyingi jamani ninazosema. Barabara ya Mlimba – Mwembeni – Msolwa pia haipitiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hapo madaraja pia yamekatika. Daraja la Chiwachiwa, Daraja la Mfuji, Daraja la Mto Londo, yote yamekatika na hayapitiki. Kwa hiyo, ninaomba Serikali yetu Tukufu iziangalie hizi barabara kwa jicho la ziada ili ziweze kutengenezwa na wananchi wetu waweze kuendelea na mawasiliano na kazi zao za kuinua uchumi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa afya, tunashukuru sana Serikali yetu Tukufu ilitujengea hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba. Hospitali inafanya kazi, lakini ina changamoto. Changamoto yetu katika upande huu wa hospitali yetu ni ukosefu wa watumishi wa maabara, ukosefu wa wataalam wa mionzi na ukosefu wa jengo la *emergency*. Pia, tuna ukosefu wa jengo la *theatre* na jengo la mama ngojea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali yetu Tukufu ituletee watumishi hawa na pia itujengee haya majengo ili wananchi waendelee kupata huduma na wapate huduma kwa karibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache, ninashukuru kwa nafasi hii na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Kijakazi Yunus Mohamed atafuatiwa na Mheshimiwa Christina Solomon Mndeme, Mheshimiwa Mgonto Kitima ajiandae.

MHE. KIJAKAZI Y. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili kuchangia kwenye hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninaungana na wachangiaji waliopita kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi

wa rehema ambaye ametuwezesha sisi sote kuwa wazima wa afya na kukutana hapa kwenye Bunge Tukufu siku ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa kibali na kuweza kusimama hapa mbele ya Bunge hili Tukufu na kuweza kuzungumza machache kwa niaba ya Wanawake na wananchi wa Mkoa wa Lindi kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatumia nafasi hii pia kuungana na waliotangulia kuchangia, kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninapenda kumwita malkia wa nguvu. Mheshimiwa Rais kama wengine walivyoeleza, amefanya kazi kubwa sana ya kuliletea maendeleo Taifa letu na sisi wanawake wa Mkoa wa Lindi na wananchi wa Lindi kwa ujumla tumekuwa sehemu ya kupata keki hiyo ya Taifa ambayo Mheshimiwa Rais ameendelea kuigawa katika maeneo yote ya Tanzania. Tunamshukuru lakini tunampongeza sana kwa kazi kubwa anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatumia nafasi hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Amefanya kazi kubwa sana, amebadilisha fikra za Watanzania, ameendelea kuwafanya Watanzania kuwa na imani na Serikali yao, kuwa na imani na viongozi wao na kazi kubwa aliyoifanya ya kuwasikiliza wananchi kero zao. Kitu hiki alichokifanya atalipwa na Mwenyezi Mungu kwa sababu mtu anapokuwa amejawa na mambo kifuani, tiba pekee ni kupata mtu ambaye atampa sikio na kumsikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili Mheshimiwa Waziri Mkuu amelifanya kwa umakini mkubwa sana, ametoa tiba kwa Watanzania tena wa hali ya chini kabisa na Mwenyezi Mungu kama nilivyosema atamlipa kwa kadiri ya haya aliyoyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki alichokifanya Mheshimiwa Waziri Mkuu kimesababisha mabadiliko kwa watendaji kule chini, sasa katika baadhi ya maeneo wameanza kusikiliza kero za wananchi. Wameanza kuwasikiliza kwa sababu wameona Kiongozi Mkuu wa

Kitaifa ameanza kufanya kazi hiyo, kwa hiyo na wao wameanza kuifanya kwa vitendo katika maeneo yao. Ninaendelea kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na kumshukuru sana kwa jambo hili ambalo analifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajielekeza sasa kwenye mchango wangu. Sisi Watanzania wote ikiwemo Wabunge tuliopo hapa ndani, wote tunatambua kwamba Mheshimiwa Rais amekuwa *champion* wa nishati. Siyo tu nishati ya kupikia, lakini nishati kwa ujumla wake na katika kuthibitisha hilo tumeona katika uongozi wake, awamu iliyopita amefanya kazi kubwa sana ya kuokoa maisha ya Watanzania ambao tunaambiwa kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, takribani wanawake 33,000 walikuwa wakipoteza maisha kwa mwaka kwa sababu ya matumizi ya nishati chafu ya kupikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amekuja na nishati safi ya kupikia na tumeona akina mama katika maeneo mbalimbali wameipokea, imewafikia. Kwa hiyo, hii unaona ni kwa namna gani Mheshimiwa Rais ameonesha moyo wa huruma, moyo wa upendo kwa wanawake wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi tulishuhudia hapa Tanzania, Januari 27 mpaka 28 hapa Dar es Salaam, tulikutanisha Wakuu wa Nchi za Afrika kwa ajili ya kujadili mustakabali wa nishati Afrika na moja kati ya maazimio yalikuwa kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkutano ule ulitambulika kama "*Mission 300*" na mkutano ule, kwa nini walikuja Tanzania? Ni baada ya kubaini kwamba, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, amefanya kazi kubwa ya kusambaza umeme mpaka vijijini. Sasa walikuja Tanzania, kwa ajili ya kujifunza nini tunafanya mpaka kuweza kufikia hatua zile ambazo tumezifikia. Walijifunza na waliweka maazimio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Mkoa wa Lindi tumekuwa sehemu ya wanufaika wa nishati na vijiji vyote 523 vya Mkoa wa Lindi tayari vimefikiwa na umeme. Sasa hii ni dhamira ya dhati ya Mheshimiwa

Rais kuhakikisha kila Mtanzania anafikiwa na umeme na kila mwanamke anapata nishati safi ya kupikia; unapozungumza umeme, unazungumza nishati safi ya kupikia. Pamoja na jitihada hizi za Mheshimiwa Rais, lakini kule Lindi umeme umekuwa kama koroboi, kwa wasiojua koroboi wengine wanaita kibatari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme unakatika zaidi ya mara 10 au 20 kwa siku. Sasa je, ile dhamira ya kumkomboa mwanamke anayetumia nishati chafu ya kupikia tunaifikia, hatutaifikia? Je, ile dhamira ya Mheshimiwa Rais ya kuhakikisha kila Mtanzania anafikiwa na umeme hatuwezi kuifikia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua kwamba, Serikali inaendelea kufanya jitihada, mikoa yote Tanzania imeungwa kwenye Gridi ya Taifa isipokuwa mikoa mitatu tu; bado Mikoa mitatu, ikiwemo Lindi na Mtwara. Naomba, pamoja na jitihada za Serikali, sisi Mkoa wa Lindi tuungwe kwenye Gridi ya Taifa, ndiyo uhakika pekee wa kuwa na umeme wa uhakika. Wanawake wa Mkoa wa Lindi wamenituma, wanaomba hii kero ya umeme wanayoipata, siyo tu inasababisha wawekezaji kutokuja katika mkoa wetu, lakini inaendelea kuharibu bidhaa za watu kwa sababu, umeme ukikatika, ukiwaka, ni kero kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba, Mheshimiwa Rais anayo dhamira ya dhati na nimesimama hapa kumwomba aendelee kutufikiria wananchi wa Lindi. Gridi imefika mpaka Mkoa wa Ruvuma na tunajua mkandarasi yuko kazini, lakini anakwenda taratibu sana. Umeme kuutoa Tunduru, Masasi mpaka Mahumbika ni kipande kidogo tu, tunaomba watufikirie sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la migogoro ya wakulima na wafugaji. Wanawake wa Mkoa wa Lindi wamenituma, wanasema wanawapenda sana wafugaji, wanaipenda sana mifugo, lakini inaleta adha kubwa sana kwao kwa sababu, sisi wananchi wa Mkoa wa Lindi ni wakulima kwa asilimia kubwa, kwa hiyo, ninajua muda wangu unaelekea ukingoni, ninaomba. Pamoja na kwamba, tunawapenda wenzetu, tumeona kule Morogoro Mheshimiwa Rais mwaka jana, kama sikosei, alizindua mpango mzuri sana wa

"Tutunzane"; tuufuatilie mpango ule kama umeleta manufaa twende tukautumie katika maeneo mengine ikiwemo Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili namwomba Waziri wa Mifugo na Uvuvi, baba yangu, kipenzi cha moyo wangu kabisa, Mheshimiwa Bashiru Ally, tuongozane kwa sababu, unapofika Mwezi Juni mpaka Mwezi Desemba hali kule Lindi inakuwa ngumu, akina mama wanateseka. Ukienda kwenye eneo linalopita Mto Mbwemkuru, Kilwa, Liwale, Nachingwea na Ruangwa, akinamama wanaishi kwenye taharuki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi hawalali, kwa ajili ya kuhakikisha akina mama wanakuwa salama. Mkuu wetu wa Mkoa, Mama Telack, anahangaika kuhakikisha kwamba, akina mama wale wakulima wanakaa kwenye hali nzuri. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Dkt. Bashiru twende akaone kuanzia Mwezi Juni mpaka Desemba jinsi akinamama wale wanavyoteseka. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Bashiru amesikia. Naomba maliza hoja yako. Unga mkono hoja. *(Makofi)*

MHE. KIJAKAZI Y. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Christina Solomon Mndeme, Mheshimiwa Thomas Mgonto Kitima atafuata. Mheshimiwa Onesmo Merdson Mkondya, ajiandae.

MHE. CHRISTINA S. MNDEME: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Ninaanza kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi, kwa kuniteua na kuruhusu mimi kugombea nafasi hii kuwawakilisha wanawake wa Mkoa wa Tabora. Kwa namna ya pekee ninawashukuru sana Wanawake wa Mkoa wa Tabora kwa kunipigia kura ya ndiyo na leo hii ninawawakilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee ninatoa pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutunukiwa Shahada ya Uzamivu ya Heshima kutoka Chuo Kikuu cha Jimbo la Nasarawa Keffi kilichopo Nchini Nigeria. Shahada hiyo ya uzamivu ya heshima kwa kutambua mchango wake, kama kinara wa nishati safi ya kupikia, afya ya mama na mtoto, taswira nzuri katika masuala ya uongozi kwa wanawake Afrika na kusimamia masuala ya biashara, hususan kwa vijana wa Kiafrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hongera sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, dunia inatambua kazi zako na uongozi wako mzuri, bora na thabiti. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu kipenzi na chaguo la Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua nafasi hii vilevile kumpongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Spika wa Bunge letu, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge. Mwenyekiti wa Wanawake wote wa Tanzania, Mary Pius Chatanda, Makamu Mwenyekiti Zainab Shomari na vilevile Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa wote nchini, pamoja na Mkuu wangu wa Mkoa, Mheshimiwa Paulo Chacha wa Tabora. Tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakuu wa Wilaya, Maafisa Tarafa, Watendaji wa Kata, Watendaji wa Vijiji, Watendaji wa Mitaa, Waheshimiwa Madiwani, Wenyeviti wa Serikali za Mitaa na wananchi wote kwa ujumla kwa kazi kubwa wanazozifanya. Hongera sana, kwani wao wanamuunga mkono Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizi tunasema Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kazi zake anatekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa vitendo. Ninachukua fursa hii tena kwa dhati ya moyo wangu kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Daktari huyu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa uongozi wake mahiri na bora wa kuwatumikia wananchi wa Tanzania na dunia inashuhudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema Rais huyu ana mapenzi ya dhati kwa Watanzania, ana moyo wa dhati kwa Watanzania, anafanya kazi kwa uhodari wa dhati, ili Watanzania hawa waweze kufurahia matunda ya nchi yao. Sisi sote ni mashahidi wa kazi kubwa anayofanya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuwaletea wananchi maendeleo. Tunashuhudia Tanzania ya leo, siyo Tanzania ya jana, imepiga hatua sana ya maendeleo, kila sekta imeguswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashuhudia kila mkoa umeguswa kimaendeleo, kila wilaya imeguswa, kila tarafa imeguswa, kila kata imeguswa, kila kijiji kimeguswa, kila mtaa umeguswa na tabasamu la mama linaonekana. Tabasamu la mama tunaliona kwenye madarasa, tabasamu la mama tunaliona kwenye vifaa vya afya, tabasamu la mama tunaliona kwenye hospitali, tabasamu la mama tunaliona kwenye barabara, tabasamu la mama tunaliona kwenye ma-*culvert*, tabasamu la mama tunaliona kwenye madaraja, tabasamu la mama tunaliona kwenye ruzuku ya pembejeo na tabasamu la mama tunaliona kwenye chanjo za mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tabasamu la mama pia tunaliona katika ujenzi wa *VETA* katika kila Wilaya. Tabasamu la mama tunaliona kwenye ajira, tabasamu la mama tunaliona kwenye ujenzi wa masoko, tabasamu la mama tunaliona kwenye mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Tabasamu la mama tunaliona kwenye umeme, tabasamu la mama tunaliona kwenye *SGR*, tabasamu la mama tunaliona kwenye uchumi wa bluu, tabasamu la mama tunaliona kwenye utalii, tabasamu la mama tunaliona kila sekta; nani kama Mheshimiwa Samia? Hakuna wa mfano wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa ujumla tuna kila sababu ya kumwombea Mheshimiwa Rais wetu huyu, ili Mwenyezi Mungu aendelee kumpa afya njema, Mwenyezi Mungu aendelee kumpa ulinzi, Mwenyezi Mungu aendelee kumpa nguvu, ili aweze kuwatumikia Watanzania hawa. Insha Allah Mwenyezi Mungu anasikia dua na sala zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anazozifanya za kuwafikia Watanzania. Ninamshukuru sana na kumpongeza kwa hotuba yake nzuri iliyoakisi hali halisi ya maendeleo ya Taifa letu. Hotuba yake nzuri ambayo inaakisi hali halisi ya bajeti na mpango wa maendeleo wa bajeti kwa Watanzania. Tunaliona tabasamu la mama katika hotuba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawapongeza pia, viongozi wote wakiwemo Waheshimiwa Mawaziri chini ya Wizara yake, kwa kazi kubwa wanayoifanya. Mheshimiwa Rais ameleta tabasamu kila sekta kupitia falsafa yake ya "Kazi na Utu, Tunasonga mbele". Ni kwa sababu, Mheshimiwa Rais wetu anathamini kazi, Mheshimiwa Rais wetu anathamini utu na Taifa linasonga mbele. Mheshimiwa Waziri Mkuu, yeye akiwa msimamizi wa shughuli zote za Serikali, sisi tunamwombea dua. Mwenyezi Mungu akusimamie kwani tunaona kazi zako na tunazithamini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi wewe umekuwa ukiwafikia wananchi, leo hii tunashuhudia maendeleo makubwa nchini kwetu. Sisi Wanatabora tunashuhudia Reli ya *SGR* kutoka Tabora – Isaka, Tabora – Kigoma inajengwa, maji kutoka Ziwa Victoria tumepata, ili kumtua mwanamke ndoo kichwani na hususan mwanamke wa Tabora. Ushauri wangu kwa Serikali ni, sisi Wanatabora tunaomba kujengewa hospitali ya kanda…

MWENYEKITI: Malizia Mheshimiwa Mndeme.

MHE. CHRISTINA S. MNDEME: …ili tuweze kusogeza huduma za afya karibu, lakini vilevile tunaomba *TARURA* waongezewe fedha ili wawe na fedha za kutosha na kuondoa changamoto ya barabara. Barabara zikiwa nzuri, mnufaika mkubwa ni mwanamke na mtoto. Tunaomba semina iendelee kupanuliwa wigo kwa wanawake kupitia mikopo na uwezeshaji wananchi kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri Serikali pia kupitia TAMISEMI, iendelee kuboresha mfumo mzuri wa kuhamasisha halmashauri kujiunga na biashara ya *carbon,* ili Serikali ipate fedha nyingi kupitia biashara hii iweze kuzalisha *credit* nyingi. Biashara ya *carbon* siyo

kupitia tu misitu, biashara ya *carbon,* halmashauri inaweza kupata fedha kupitia nishati safi ya kupikia, nishati mbadala, majengo endelevu, *green buildings*, usimamizi wa takangumu *(waste management),* kama ilivyo Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, kilimo himilivu *(climate smart agriculture)*, usafiri endelevu, uhifadhi wa ardhi oevu *(waste land conservation)* ili sasa hamashauri zetu…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. CHRISTINA S. MNDEME: …ziweze kupata fedha, kwa ajili ya kuzalisha *credit* nyingi na kupata fedha nyingi…

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mndeme.

MHE. CHRISTINA S. MNDEME: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Nilimwita Mheshimiwa Thomas Mgonto Kitima, Mheshimiwa Onesmo Merdson Mkondya atafuatia. Mheshimiwa Abubakar Ali Omari ajiandae.

MHE. THOMAS M. KITIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia japo kidogo kwenye hoja aliyoleta Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kifupi ameweka hoja ambayo imesheheni mambo mbalimbali. Kwa hiyo, ninachukua fursa hii kwanza kabisa kumpongeza yeye, kuipongeza Serikali hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Rais wetu, mama yetu, kwa hatua kubwa na katika kupanga safu ambayo ndiyo inakwenda kuweka msingi wa awali wa Dira yetu ya Miaka 25 ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hoja hii iliyoletwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa, maana ya bajeti ya kwanza kabisa, ndiyo inayoweka msingi imara. Wanasema, nyumba bila msingi imara, hiyo nyumba huenda isiwe imara, kwa maana hiyo, hapa ndiyo tunaanza kuweka ule msingi wa miaka 25 kwa Bunge hili. Bunge hili litaweka historia kama tukiweka msingi wa zege, msingi wa mawe,

basi msingi huu ndiyo utakaotuhakikishia hii miaka 25 tunaenda kuivuka vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza pia Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ziara yake aliyokuwa akiifanya mikoani. Pia, ninatumia fursa hii kumpongeza Mkuu wangu wa Mkoa na Mkuu wangu wa Wilaya kwa sababu, wamekuwa wakitembea kutatua kero na kuzisikiliza. Kwa namna nyingine wameweza kusaidia kuhudumia wananchi wa Mkoa mzima na Wilaya yetu ya Ikungi, ninawapongeza sana na watendaji wote wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda kwenye hoja aliyoleta Mheshimiwa Waziri Mkuu, amesema katika dhima hii ambayo ameiita "Mageuzi Katika Kukuza Uchumi na Kuzalisha Ajira" kwa maana ya Mpango wa Nne wa hii miaka mitano, ambayo tunaianza sasa hivi. Tunategemea kwamba, haya yote Waheshimiwa Wabunge waliyozungumza yataakisi haya mageuzi, ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu amekwishayataja, ambayo ni mageuzi katika uchumi, mageuzi katika kukuza viwanda vyetu na mageuzi katika kushirikisha sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaungana na wenzangu kwa suala ambalo wamelizungumza takribani Waheshimiwa Wabunge wote. Waheshimiwa Wabunge wote wameongelea kuhusiana na barabara na ninaanzia hapohapo; tuna Barabara ambayo inatajwa kwamba, inatokea Handeni kupitia Kiberashi – Chemba – Kwamtoro na hapo Singida, ambapo inagusa moja kwa moja Jimbo la Ikungi Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kwenye Jimbo la Ikungi Mashariki ni takribani kilometa 40 tu. Katika hizo kilometa 40, kama kweli tunataka kuwasaidia watu wetu, kuna kama kilometa 15 kutoka njia panda, kupitia Unyankhanya mpaka Siuyu na Makiungu. Pale Makiungu kuna hospitali kubwa ambayo mwekezaji huyo amejenga ile hospitali ambayo inahudumia watu kutoka mikoa mbalimbali, Simiyu, Manyara na mikoa ya jirani, lakini ni hospitali ya rufaa, ni hospitali kubwa sana ambapo, hata Serikali mle ndani tuna watumishi wetu ambao wanafanya kazi pale. Pamoja na yote ina upungufu wa watumishi upande wa Serikali, lakini ni hospitali kubwa ya Kitaifa,

ambayo inatumika kusaidia hospitali hizi ambazo tunazijua za rufaa, kama Muhimbili, Benjamin, pamoja na Bugando.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hiki kipande cha kilometa 15, kama kitawekwa lami, kitasaidia sana kuepusha adha ambazo wanakutana nazo wagonjwa, hasa mama zetu, wanapokuwa pale hospitali, wanapofanyiwa operesheni, wanapojifungua na wanaporudi makwao kupitia hiyo barabara, ina rasta nyingi, yaani ina mashimo mengi makubwa hata inafika wakati ile mishono inafumuka. Hawa wagonjwa wanapata tabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba hii barabara pamoja na kwamba ina urefu wa kilometa 340, hiki kipande cha takribani kilometa 15 kiangaliwe kwa jicho tofauti, kwa sababu huyu mwekezaji amewekeza pale na sisi tuna-*promote PPP* kwa maana ya ubia kati ya Serikali na sekta binafsi. Kama huyu amekwishawekeza hospitali kubwa pale tena ya rufaa inahudumia watu kutoka mbali, hiki kipande kifupi kuwasaidia hawa wagonjwa wasipate taabu ama wasidhurike na madhara yatokanayo na barabara, ninaomba sana katika hili liwekewe msisitizo mkubwa na hiki kipande cha kilometa 15 kiweze kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii barabara Wabunge wote inapopitia wamekwishaitaja, Mbunge wa Kilindi juzi alitaja, Mbunge wa Chemba juzi alitaja, lakini Mbunge wa Kiteto naye pia aliitaja na mimi pia kwa kumalizia kwa sababu inaenda kuishia kwangu, ninaomba kama ikiwezekana wapatikane wakandarasi tofauti tofauti; wengine waanzie huko Handeni lakini wengine waanzie hapa Singida pale njia panda ili huduma iweze kupatikana kwa wepesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakumbuka toka nipo darasa la nne mwaka 1997 huku, nyumba zilikwishawekwa X muda mrefu sana na kipindi hicho watu wakawa wanajua kuna matumaini makubwa ya kwamba hii barabara inaenda kuwekwa lami na watu wakawa wameshajiandaa kuhama. Bahati mbaya kwa sababu zile nyumba nyingi ni za tope kila mara ile X huwa inafutika na pengine watu wa sasa hivi wasijue kwamba zilishapigwa X. Zimeshapigwa X muda

mrefu toka 1997 huko mwaka 2000, mwaka 2005, lakini bado haikujengwa kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Rais tarehe Mosi Machi, 2025 akiwa Handeni aliitaja hii barabara, akaiagiza Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi wakae wamtafute huyu Mbia ili hii barabara iweze kujengwa. Sasa kama Rais anatoa maagizo, sisi watendaji huku hatuoni kwamba mfalme ameshasema na kauli ya mfalme huwa haipingwi na kauli ya mfalme huwa ndiyo *final? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilitegemea kwamba nione Wizara inakimbizina kuhakikisha kwamba hii barabara inajengwa mara moja kwa sababu ni agizo na ni kauli ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa kule Handeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kipindi hapa niliwahi kumshuhudia Mbunge mmoja, kipindi mimi sijaja Bungeni, huyo Mbunge aliwahi kupiga sarakasi hapa Bungeni, baada ya kupiga sarakasi muda siyo mrefu ile barabara yake ikajengwa. Sasa kwa sasa hivi tunaongea kwa upole kwa sababu tunaamini Serikali hii ni sikivu, inaenda kuhakikisha kwamba inasikiliza maombi ya Wabunge wote. Kwa hiyo, sina haja ya kupiga sarakasi kama yule alivyopiga kwa sababu ninaamini watakwenda kuijenga hii barabara ya lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza kwa upole ila wakati utakuja tutazungumza kwa nguvu kubwa… *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana muda wako umeisha, naomba uunge mkono hoja.

MHE. THOMAS M. KITIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana, kwa sababu kuna wakati mwingine tutapata nafasi ya kuzungumza na bado kuna Wizara nyingi, bado hoja ambazo ninazo nitazizungumza wakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Nimwite sasa Mheshimiwa Onesmo Mnkondya, atafuatiwa na Mheshimiwa Abubakar Alli Omari, Mheshimiwa Grace Elias Mkoma, ajiandae.

MHE. ONESMO M. MNKONDYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwanza kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu jioni ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo pengine ni siku ndefu kwangu au kwa sababu nitazungumza dakika karibu kumi, nichukue nafasi hii pia kumshukuru sana Mungu aliyenipa uzima na kunipa nguvu za kuweza kunifikisha siku ya leo ili niweze kuchangia. Pia ninawashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Mbozi walioamua kunichagua na kunifikisha hapa Bungeni ili niweze kuwasemea, kuwawakilisha niseme tu nitawakilisha uwezo ninao, nguvu ninayo na nia ninayo, nitafanya kazi usiku na mchana kwa ajili ya wananchi wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wengi tumemshukuru na ni kweli Rais wetu inawezekana hasemi sana, lakini kazi zake zinaonekana. Kazi zinaonekana anazozifanya Mheshimiwa Rais, Majimboni mwetu ni mashahidi wote Wabunge wanaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Waziri Mkuu ameanza ziara na kwangu ameshafika amefanya kazi kubwa na ile ndiyo ambayo tunataka hata kule chini kwa watendaji, kule chini wote wacheze mpira mmoja. Sina shaka na hilo Mawaziri wapo hapo watamsaidia Waziri Mkuu, watamsaidia Rais, sisi tutawakimbilia wao usiku tutakwenda kwao, mchana tutakwenda kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia Chipando anasema amefika mpaka nyumbani kwa Mheshimiwa Waziri, rafiki yangu Profesa Shemdoe, kama mambo hayaendi, mimi nitakwenda. Ninawashukuru Wabunge pia wamefika hapa kwa kweli wamefanya kazi kubwa, hongera sana Wabunge kwa kuchaguliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nichangie, wakati ninagombea nafasi hii, wakati ninaomba ridhaa kwa wananchi niliwaahidi jambo moja na wao walinituma kwa jambo kubwa moja ambalo limekuwa ni mfupa kwa Jimbo langu la Mbozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni suala la barabara. Barabara zetu za Mkoa wa Songwe za Jimbo langu hasa Jimbo langu nikianza na Barabara ya Mlowo – Kamsamba. Hii barabara imekuwa na shida miaka nenda rudi, ninaweza nikasema toka uhuru hii barabara, tunaomba ijengwe kwa kiwango cha lami, kilometa 130 toka uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan amevunja rekodi na alipokuja nilimwambia Mama umevunja rekodi endelea kushikilia hapo hapo. Tumesaini barabara ile kwa kiwango cha lami kilometa tano kutoka Jimbo langu na kilometa tano kutoka kwenye Jimbo la mwenzangu Condester Sichalwe, Jimbo la Momba ili mkandarasi aanze Momba na mwingine aanze Mlowo wakutane katikati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajiuliza kilometa tano, kilometa 10 barabara yenye kilometa 130 tutamaliza lini? Ni zaidi ya miaka 13 tukienda kwa mtindo huo, miaka 13 tunajenga tu. Sasa niiombe Serikali kwa kuwa barabara hii mimi kama Mbunge nilishawaambia wananchi wangu wanielewe kabisa, nitapambana na mambo mengine, lakini Barabara ya Mlowo – Kamsamba ndicho kitakachokuwa kipaumbele chetu kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka hii mitano tunaomba barabara hii ianze kujengwa ili iweze kuisha na wananchi waondokane na adha wanayoipata kilometa 130, tuipe mkakati siyo kilometa tano hizi, ninashukuru sana kwa hizi kilometa tano, lakini naomba sasa watupe kilometa za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo langu ni kilometa 65, Jimbo la mwenzangu ni kilometa 65 jumla 130, barabara hii Waziri wangu na rafiki yangu kutoka kule Mheshimiwa Deus Sangu, yeye anajua

barabara hii tunakutana naye kule, Wabunge hapa hakuna Mbunge hajala mchele wa kule Kamsamba, unatoka kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge hapa wanajua kabisa tuna dhahabu ya kahawa inatoka barabara hiyo, tuna mahindi yanatoka barabara hiyo, tunayo maharage na kila kitu, hilo ndiyo ombi langu tu nimesimama kuomba barabara hii, kaka yangu Naibu Waziri Kasekenya na Waziri Ulega wanaona ninavyowafuatafuata ofisini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge waliotangulia kwenye Jimbo lile kila mmoja alipiga kelele barabara ile, sasa sijui wanataka nifanyaje? Nitahakikisha ninagombana nao, anisaidie barabara ile kaka yangu Kasekenya. Rais alishaagiza ijengwe yote kwenye kampeni, Waziri Mkuu amekuja pale ameagiza mkandarasi alipwe fedha za kianzio bilioni 3.8 mpaka sasa hayajalipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tupo kwenye Bunge la Bajeti, ninaomba kabla hatujarudi mkandarasi ashuke pale *site* aanze kufanya kazi wananchi wanatusubiri, watatusubiri mpaka lini? Tutakuwa tunawaambia itajengwa itajengwa, sasa safari hii nimekuja Mbunge kijana. Nimeahidi kuchapa kazi, sijaahidi siasa ninataka tukafanye kazi barabara hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo pia barabara nyingine hasa hii ipo *TARURA* na nimeiombea Barabara ya Mlowo – Mpito – Isansa ina kilometa 13.6 iko chini ya *TARURA*. Kwa kweli, kwa upande wa *TARURA* tuombe sana waongezewe fedha za kutosha ikiwezekana kipindi hiki cha mvua Mawaziri wangefanya ziara kwenye Majimbo ndipo watatambua shida tulizonazo na barabara hizi za *TARURA,* tuna shida mno. Niiombe barabara hii tuipandishe hadhi kutoka *TARURA* iende *TANROADS. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi hiki mvua zinanyesha kule kuna hospitali, kuna kituo cha afya kimejengwa na Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan lakini barabara haipitiki. Wananchi wataendaje kutibiwa kule? Akina mama wajawazito wataendaje kule? Niombe

sana kipindi hiki tuhakikishe tunaipa *TARURA* fedha za dharura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawauliza jamani vipi? Wanasema hakuna fedha za dharura tunafanyaje, hivi hapa ninawaza ljumaa nirudi kwenda angalau nitafute hata chochote mfukoni mwangu nikaweze kurekebisha rekebisha mashimo kule, hivi kweli? Niombe tuziangalie hizi barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara zingine za *TARURA* ni Barabara ya Itepula – Shasya – Halungu iangaliwe barabara hii. Sisi ni wakulima tunataka tusafirishe mazao yetu kutoka vijijini kuja mjini barabara hamna, tunaomba sana tuangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wa Msanyira wananisikia hapa barabara yenu nimekuja juzi haipitiki, niko hapa kuhakikisha ninaiomba Serikali iweze kupitika. Watu wa Intentula, watu wa Isani, watu wa Isela barabara ile na yenyewe itakuja kupitika nitamfuata rafiki yangu, kaka yangu Profesa Shemdoe analifahamu, yeye ndiye mlezi wangu, ninaomba anisaidie sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kelele pekee sasa hivi kule ni barabara. Watu wa Mwanjelwa wamenipigia simu wanataka Barabara yao ya Mwanjelwa kwenda kule Shitungulu. Nitampeleka Waziri apafahamu, lakini nazo barabara nyingi na muda wangu umeniishia, ila kilio changu kwa miaka hii mitano ni Barabara ya Mlowo – Kamsamba ninahitaji ijengwe sasa.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. ONESMO M. MNKONDYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nichukue nafasi hii kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Ninamwita sasa Mheshimiwa Abubakar Alli Omari, atafuata Mheshimiwa Grace Elias Mkoma na Mheshimiwa Tamima Haji Abbass ajiandae.

MHE. ABUBAKAR A. OMARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninakushukuru sana kwa kunipa fursa hii na kwa kuwa leo ndiyo ninasimama mara kwanza mbele ya Bunge lako Tukufu, ninaomba kwa idhini yako nizungumze mambo mawili matatu yafuatayo kabla sijaingia kwenye uchangiaji wa hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenijalia afya na uwezo nimesimama hapa mbele ya Wabunge na mbele yako Mwenyekiti. Pili ninapenda kukishukuru Chama changu Cha Mapinduzi kwa kuniteua kuwa mgombea wa Chama Cha Mapinduzi. Tatu ninapenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Manonga kwa ujumla wao, walitupa kura za kutosha kwa wagombea wote wa CCM kuanzia Mwenyekiti ambaye ni Rais wetu, Mbunge na Madiwani wote 19. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kutoa pole kwa familia ya Mheshimiwa Sawawa, Diwani wa Kata ya Ziba, ambaye alifariki 1/1/2026 Mungu ailaze roho ya ndugu yetu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijikita kwenye hotuba ya Waziri Mkuu hii ni hotuba ambayo inaakisi ile hotuba ya Rais na hapa Rais kwenye hotuba yake aliweka *road map* ya uchumi wetu tunataka tutoke wapi tuende wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hotuba inatakiwa iangaliwe kwa makini kwa sababu haiwalengi Watanzania tu, hii hotuba inalenga hata wawekezaji ambao wanakuja kuwekeza katika nchi yetu, kwa hiyo ni lazima tuiangalie kwa makini na tuitafakari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya hayo yote, nchi yetu ni kubwa sana na maendeleo yamekuwa yapo tofauti tofauti katika kila sehemu. Ili sehemu zote ziwe kwenye safari ya kuelekea kwenye pato lile la Taifa la dola 7,000 kwa kila mtu. Kwa mfano, sasa hivi kwa ripoti ya mwaka jana tu 2025/2026 ambayo ilitolewa na Benki Kuu, pato la mtu mmoja kwa Mkoa wa Tabora ni shilingi 6,000. *Statistics* ambazo zimetolewa na Idara ya Takwimu *(National Bureau of Standards)*

inaonesha kila mtanzania mmoja ana watu watano wanaomtegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukiangalia pale watu kipato cha mtu mmoja ni shilingi 6,000 ukigawanya kwa watu watano inakuja kwenye 1,000 na kitu. Sasa tuna safari ndefu sana kutoka hapo kwenye 1,000 mpaka Mtanzania apate dola 7,000 na leo tunavyozungumza ile dira yetu ya miaka 25 tayari mwaka mmoja umeshapita, tunatakiwa tufanye kazi kweli kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Rais yeye ameshanyoosha njia, kaonyesha barabara tunatakiwa tupite hapa ni jukumu letu sasa tuliobakia hapa kila mtu kivyake. Waheshimiwa Wabunge na Mawaziri *lets do our best,* tuna kazi ndefu sana siyo masihara. Hapa tunasikia Wabunge wote wanalalamikia masuala ya pesa, sasa mimi kama mtu wa kodi, mwenye asili ya kodi na jambo ambalo kwa ajili ya muda nitakwenda nalo haraka tu tuweze kwenda pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maeneo ambayo yako nyuma kwa mfano Jimbo langu la Manonga, liko nyuma kweli na kwa sababu ya vichocheo vya uchumi havipo hasa barabara, tuna Barabara moja kuu inatoka Choma – Ziba – Nkinga mpaka Puge, Jimbo zima kwa ujumla halina lami hata moja hata kilometa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninashukuru kwamba Awamu ya Sita pesa zimeletwa kuanzia ile awamu ya kwanza, katika awamu ya sita na sasa hivi na tunakokwenda tunaenda kuona barabara ya lami inaenda kujengwa. Nimshukuru sana Waziri, Naibu Waziri wa Ujenzi tumesumbuana sana, nimemsumbua sana lakini hatimaye tumepata kilometa kadhaa kuanzia Ziba kwenda Nkinga na kuanzia Puge kwenda Ndala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe tu pale atuongezee angalau kwa awamu ya kwanza hizo kilometa zifike Nkinga na za huku zitoke mpaka Puge mpaka Ndala. Hiyo itakuwa imetusaidia kabisa, kwa sababu hizo Hospitali zote za Ndala na Nkinga ni hospitali kubwa, ile Nkinga ni Hospitali ya Rufaa ambayo ndiyo wananchi wote

wa Mkoa wa Tabora na mikoa ya jirani wanaitegemea hiyo hospitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ninataka kulizungumzia ni masuala ya barabara hizi zingine za mtaa. Tunaomba hii Barabara ya kutokea Nsimbo – Igoweko mpaka Mabeshi ipandishwe daraja iwe barabara ya *TANROADS* na pale tuna madaraja mawili tu katika Mto Roya. Mbunge mwenzangu, jirani yangu kaelezea, hiyo ni barabara muhimu sana kwa Jimbo la Manonga ili tuweze kufungua uchumi wa wananchi wa Manonga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara zingine za huko na zenyewe pia zina umuhimu, hivi ninavyozungumza hakuna mawasiliano kati ya Mwisi na Mizanza na kuna Barabara nyingine ya kutoka Chibiso kwenda Choma, hizo barabara zipo katika hali mbaya na nyingine ni ya kutokea Nyandekwa kupitia Ntigu mpaka Ulaya, kwa hiyo tumeona kama mahitaji ni mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kwenye suala la maji, hili suala la maji kwenye Jimbo langu la Manonga limekuwa kitendawili. Juzi niliomba kuonana na Waziri wa Maji akanipa *appointment* bahati mbaya nimeenda ofisini kwake sikumkuta. Tuna Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria. Maji ya Ziwa Victoria yamefika mpaka Jimboni kwetu, huo mradi umeenda mpaka Choma, Choma umetumia zaidi ya milioni 400, lakini mpaka sasa hivi ninavyokueleza shida ya maji kule bado iko vilevile, hivyo, tunahitaji maji. Pia huwa kuna Mradi huo wa Maji ya Ziwa Victoria yanatakiwa yatoke Nkinga Hospitali kupitia Mwisi – Chabutwa mpaka Nsimbo. Huo mradi ulikuwa ukamilike mwaka jana lakini mpaka leo huo mradi umesimama sijaelewa na sijui tatizo ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu masuala ya kilimo tunaishukuru Serikali imeweka pesa za kujenga bwawa la umwagiliaji kule maeneo ya Choma. Masuala ya elimu pia tumepata vya kutosha, afya na michezo. Sisi tunayo shule moja ya Sekondari ya Ziba hiyo imeanzisha timu ya watoto wasichana na sasa hivi inaenda kucheza ligi daraja la kwanza. Ninamwomba Waziri Makonda aje naye atie nguvu yake kwenye suala hilo. Hii ni timu ya Kata pekee Tanzania hii ambayo

inacheza ligi ya Taifa tena ya wasichana na hiyo timu ya wasichana imeshatoa wachezaji wanne kwenda timu ya Taifa. Kwa hiyo hilo jambo na lenyewe linatakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuje sasa kwenye suala zima la uchumi wa nchi hii. Ndugu zangu mimi kama nilivyosema ni mtoza kodi, uchumi wa nchi hii unahitaji kwa kweli kutizamwa kwa jicho la tatu, lazima mifumo yetu na sera zetu za kodi ziwe zinatabirika na zenye kukaa muda mrefu. Tumesema ili tufikie maendeleo ya 2050 tunahitaji wawekezaji ambao watakuja kusukuma hapa, bila kuwa na sheria za kodi ambazo zinatabirika itakuwa ni shida sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kwa haraka haraka ni tunatakiwa ili tupate maendeleo ya kweli, lazima tukusanye kodi vizuri kila shilingi inayotakiwa ikusanywe ikusanywe na matumizi yawe mazuri, ndiyo tutapata maendeleo. Sasa kwenye suala la kodi Rais alizungumza kuhusu…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Abubakar, muda wako umekwisha.

MHE. ABUBAKAR A. OMARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa ninamalizia dakika moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kodi inabidi tunapo-*tax* madini yetu sasa hivi hayatupi tija sana, kwa sababu ya muda, nilitaka nieleze hapa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa utakuwa na muda mwingi, tunayo bajeti ya Wizara ya Fedha, tuna Bajeti Kuu, zote ni kodi tupu kwa hiyo utapata muda mwingi tu.

MHE. ABUBAKAR A. OMARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache ninaomba, kwa niaba ya wananchi wa Manonga baada ya kutoa haya, nina imani

kabisa Waziri Mkuu katika majumuisho yake ataangalia haya tuliyosema Wabunge kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja kwa niaba ya wananchi ya Manonga. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Grace Elias Mkoma, Mheshimiwa Tamima Haji Abass na Mheshimiwa Kassimu Amari Mbaraka ajiandae.

MHE. GRACE E. MKOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii katika Bunge lako Tukufu ili nichangie hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa kuanza ninaomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii, kwa kunifikisha siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia nichukue nafasi hii kumpongeza na kumshukuru sana Mwenyekiti wetu wa Chama Cha Mapinduzi, Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa kura nyingi ambazo alizipata na zimepelekea Chama Cha Mapinduzi kuwa na Wabunge wengi katika Bunge hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutuona sisi watu wa Singida; kwa maana ya kutuchagulia au kumteua Waziri Mkuu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba ambaye anatokea Mkoa wa Singida. Tunashukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutuamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuaminiwa na Mama Samia Suluhu Hassan. Sisi wananchi wa Singida tunampongeza sana. Tunamwombea kwa Mungu aendelee kuchapa kazi, Wanasingida tunamwamini, lakini na Taifa la Tanzania linamwamini; aendelee kuchapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue nafasi hii pia kumshukuru mama yetu mlezi wetu wa UWT, Mama Mary Chatanda.

Ametulea vizuri wanawake wa UWT na ametuweka pamoja na wanawake wote tumekuwa na umoja. Ninaomba nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Singida ambao wao sasa walinichagua kwa kura nyingi na wamesababisha mimi kuwepo kwenye Bunge hili Tukufu kwa ajili ya kuwawakilisha. Ninawaahidi kwamba nitawawakilisha vyema na kwa weledi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza sana Serikali kwa kazi nyingi ambazo inazifanya, pia kwa kuleta fedha nyingi katika Mkoa wetu wa Singida na kusababisha miradi mingi kutekelezeka; ninaipongeza sana Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuleta fedha nyingi hizo, bado katika Mkoa wetu wa Singida kuna changamoto nyingi sana. Ninaiomba Serikali, kwa mfano kwenye suala la barabara; ninaona kila Mbunge akisimiama hapa analalamikia habari ya barabara. Vilevile, kila Mbunge akisimama hapa analalamikia maji na kila Mbunge akisimama hapa analalamika kuhusu elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue nafasi hii kutaja changamoto mbalimbali ambazo ziko katika Mkoa wangu wa Singida, hasa nikianza katika barabara. Katika Mkoa wetu wa Singida, hasa katika Wilaya ya Iramba, tuna changamoto kubwa sana ya barabara. Tuna barabara inayoanzia katika Kijiji cha Misigiri. Barabara hiyo inapita Ndago inaenda mpaka Singida Mjini. Barabara hiyo inaunganisha wilaya tatu za Mkoa wetu wa Singida. Barabara hiyo ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hiyo imeanza kujengwa tangu miaka miwili iliyopita, lakini bado inasuasua; mpaka sasa barabara hiyo haijakamilika. Ninaiomba Serikali itusaidie kuikamilisha barabara hiyo ya Mkoa wa Singida ambayo inaunganisha wilaya tatu; iwasaidie wananchi wa Mkoa wa Singida ili sasa na wao waweze kufaidika na barabara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mikoa yetu iliyoko Tanzania Mkoa wa Singida ni moja ya mikoa kongwe na mikoa ya zamani sana, lakini mpaka hivi sasa ninavyozungumza katika Mkoa wa Singida hatuna

chuo kikuu. Ninaiomba Serikali itusaidie kutujengea chuo kikuu katika Mkoa wetu wa Singida; ukizingatia kwamba *population* ya Mkoa wa Singida sasa inakuwa kubwa, ili sasa na sisi wananchi wa Mkoa wa Singida tuendelee kunufaika na chuo kikuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changmoto nyingine kubwa sana ambayo inafanya wanawake wa Mkoa wa Singida kukosa amani na hata familia sasa zinakuwa na manung'uniko. Changamoto hiyo ni maji. Katika Wilaya ya Iramba ambalo ndilo jimbo la Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika Kitongoji cha Kiomboi tuna changamoto kubwa sana ya maji na wanawake wa wilaya hiyo hasa katika Kitongoji cha Bomani wanateseka sana. Ninaiomba Serikali itusaidie sana kututatulia changamoto hiyo ya maji ambayo imekuwa kero sana kwa wanawake wa Wilaya ya Iramba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyojua, maji ndiyo uhai, maji ndiyo kila kitu, lakini katika Wilaya ya Iramba tuna changamoto kubwa sana na hiyo imekuwa kero kubwa sana kwa wanawake wa Wilaya ya Iramba. Ninaomba sana sana Serikali itusaidie kutatua changamoto hiyo ili sasa hawa wanawake waondokane na hiyo changamoto ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, ninashukuru sana, ninaishukuru Serikali yangu. Ninaamini Serikali yangu ni Serikali sikivu, itaenda kusaidia kero hizi na kutatua kero hizi za watu wa Mkoa wa Singida, ili sasa watu wa Mkoa wa Singida waifurahie Serikali yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Grace Mkoma. Ninamwita sasa Mheshimiwa Tamima Haji Abass atafuatiwa na Mheshimiwa Kassimu Amari Mbaraka, Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza ajiandae.

MHE. TAMIMA HAJI ABASS: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi jioni hii ya leo ili kuwa sehemu ya wachangiaji.

Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia na kunijaalia uhai, uzima na afya njema katika kufanikisha majukumu yangu ya kila siku; ninamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana vilevile, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na uongozi wa chama changu wote, pamoja na uongozi wa Jumuiya ya UWT, kwa kuniamini, wakasema na ninaweza kulisukuma gurudumu hili na kuwa Mbunge kupitia kipindi hiki cha Bunge la Kumi na Tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Kaskazini Unguja na wao kwa kuniamini na kunichagua nikaweza kuwakilisha ndani ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anazozifanya kila siku na hatimaye maendeleo kila kona yanaonekana. Vilevile, ametuheshimisha wanawake ndani ya Tanzania na ndani ya dunia kwa jumla. Dunia imetambua kama mwanamke na yeye ni nguzo imara na uongozi anauweza na anaweza kusimamia chochote akiamua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa jitihada zake kubwa za kuing'arisha Zanzibar. Zanzibar imeonekana, kila kona maendeleo yameonekana, tunampongeza sana kwa kazi kubwa anazozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani kwa uongozi mzima wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Waziri Mkuu tunampongeza, kwanza kwa kuteuliwa kwa nafasi hii. Anaitendea haki nafasi hii na Mheshimiwa Rais hakukosea kumteua Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kusimamia Wizara hii au kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi zangu pia na shukrani kwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kipindi

ambacho amekaa tunampongeza sana. Tumeona mabadiliko makubwa ya kimaendeleo yamefanyika ndani ya Bunge hili kama maboresho ya mitambo, tunampongeza sana. Pia, tunampongeza kwa uendeshaji wake wa kutufundisha, wa kutuendeleza mpaka tukaweza kuwa Wabunge wazuri na tunaweza kutoa michango yetu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo, niende kwenye mchango wangu sasa kwenye hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo ameiwasilisha hapa. Nianze kwenye suala la kuwaendeleza vijana. Vijana ndani ya nchi hii tunasema ndiyo nguvukazi na ni nguvukazi kweli. Sasa, katika kuwaendeleza vijana ni lazima tuwe na mipango imara, mipango thabiti ya kuwasimamia vijana hawa ili wawe vijana bora baadaye wawe wazazi bora. Tutafanya hivyo kwa kuanzisha jitihada za kuwasomesha watoto wetu, kwa sababu watoto ndiyo wanaoanza, baadaye wanakuja vijana. Hawa watoto tuwajengee misingi imara wanapoanza shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali kwa kujitahidi kuandikisha wanafunzi wengi sana katika kipindi hiki. Tunaambiwa hadi Februari, 2026, wanafunzi wapya wa shule za awali zaidi ya 70% wameandikishwa na zaidi ya 80% wameandikishwa darasa la kwanza. Hiyo inaonesha wazi kuwa wananchi wamehamasika kuwapeleka watoto shule. Pia wazazi wametimiza wajibu wao wa kuwapeleka watoto wale shule kwa ajili ya kupata elimu bora ili waje wapatikane vijana bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika takwimu ile ya 70% na 86% walioandikishwa tunaona kuwa baada ya muda lile kundi lote lililoandikishwa linafikia mahali wengine wanaishia njiani kutokana na sababu mbalimbali ambazo wao wenyewe wanazijua. Sasa, ni vyema Serikali iwe na mkakati madhubuti wa kuwafuatilia wale watoto wanaoandikishwa kwa kipindi kile. Kama tumeandikisha 70% au 80%, basi tuwafuatilie mpaka ifikie wakati wamemaliza shule na wamehitimu. Kama hatukuwafuatilia tutakuwa tunasema ufaulu umeongezeka, lakini kumbe kuna kundi la watoto wamedondoka njiani, hawajafika hata darasa la saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, niiombe Serikali katika hatua hii tutilie mkazo wale vijana au watoto ambao wanaacha shule mapema kabla ya kumaliza. Kama hatutatilia mkazo, kutokana na wale watoto ambao wataachia njiani tutapata kundi ambalo halisomeki popote. Kama halisomeki popote wakati mwingine unakuta wanajiingiza katika mambo wasiyoyafahamu kwa kufuata mkumbo, kumbe hawakupata misingi bora. Ndipo pale tutakapowatafuta wale vijana bora, hatutaweza kuwapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeambiwa hapa kuwa Serikali ina mpango madhubuti wa kuwaendeleza vijana. Sasa, vijana hawa ni lazima watokane na kule wapate ule msingi bora waweze kuja kujiendeleza huku. Hata ile mikopo tunayowapelekea vijana ya 10% hawataweza kuitumia vizuri kama hawatakuwa na elimu au hawana misingi mizuri ya matumizi ya zile fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazazi wengi au wazazi wote wanategemea kuwa watoto wao watakuwa na msingi mzuri na hawatokuwa tegemezi. Kwa sababu, wakiwa tegemezi ile faida ya kuwasimamisha vijana itakuwa haipatikani. Kwa hiyo, ninaiomba sana Wizara ya TAMISEMI ijitahidi basi kusimamia ili watoto wote wapate elimu bora bila ya kujali umri, bila ya kujali wapi anatoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika lile kundi linaloacha njiani kuna changamoto ambazo zinajitokeza. Pengine wengine wanakatisha tu masomo kutokana na labda kuna upungufu wa vyoo. Basi ni lazima Serikali hili iliangalie. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, muda wako umekwisha, malizia.

MHE. TAMIMA HAJI ABASS: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Kassimu Amari Mbaraka, atafuatiwa na Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza na Mheshimiwa Yumna Mmanga Omar ajiandae. *(Makofi)*

MHE. KASSIMU A. MBARAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani sana kwa kupata fursa hii ya kuchangia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa siku hii ya leo. Jambo kubwa la msingi zaidi, ninamshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujaalia sote kuwepo hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao mizuri waliyoiwasilisha hapa Bungeni kwenye hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, michango yenye kujenga, kuonyesha mwelekezo na kutoa njia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia kuna machache ambayo nimeyaona nikasema nichangie ili hatimaye niweze kuunga mkono hoja juu ya hotuba hii. Jambo la kwanza ni kuhusiana na mikopo ya 10%. Kwanza tuipongeze Serikali kwa kutoa mikopo hii kwa muda mrefu sana ya 10% kwa makundi ya vijana, akina mama na walemavu. Ni jambo kubwa na jambo zuri sana. Tukiangalia kwa muhtasari na muktadha tulionao sasa na kule tunakokwenda, tunahitaji kufikiria upya suala hili la mikopo ya 10%, hususan kwa kundi la vijana *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu sana vijana wamekuwa wakipata asilimia nne kwenye mikopo hii ya 10%. Sasa, tunatakiwa tubadili fikra kwa kule tunakokwenda. Idadi ya vijana sasa hivi ndani ya nchi yetu ni kati ya 60% hadi 70%. Ukiangalia katika taasisi mbalimbali za fedha utabaini kuwa kuna programu nyingi sana za uwezeshaji za mikopo ya akina mama, au tuseme wanawake; lakini kundi hili la vijana limeachwa nyuma kwa namna moja ama nyingine, liko kwenye mikopo hii ya 10% ambao wanaambulia asilimia nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, ninaomba tubadili fikra na mtazamo kwa kushauri kwamba, tuanze kufikiria kuwa na Benki ya Maendeleo ya Vijana ndani ya Taifa hili la Tanzania. Vijana hawa 60% hadi 70%, ambayo ndiyo idadi ya *population* ya Tanzania ni muhimu sana kuwalea, kuwajengea uwezo kwa sababu hawa ndiyo mabilionea na wawekezaji wa kesho ndani ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa harahaharaka ukiangalia utaona kuna takribani milioni moja ya vijana au tunazungumzia *rural-urban migration*. Kila mwaka nguvu kazi inatoka vijijini inakuja mjini, lakini wakati huo huo kuna wanaohitimu shuleni na ambao wamefikia umri wa kuajiriwa takribani nao milioni moja. Yaani wako tayari kuingia kwenye soko la ajira. Hawa wote tunawapeleka wapi? Hatuwezi kuwaajiri wote, lazima tuwe na benki itakayowalea. Isiwe benki kama benki zilivyo za sasa hivi, iwe benki ya ulezi katika kusimamia *startups* za hawa vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano mdogo, kijana ana andiko mradi zuri, ana wazo zuri, anapokwenda kwenye *financial institution* yoyote leo hii atahitajika *collateral*. Amehitimu chuo huyu kijana, hana *collateral* yoyote ataweza kuanzia wapi? Jambo kubwa na la msingi zaidi linalohitajika kufikiriwa upya, benki hiyo ianzishwe, ikishaanzishwa ifanye kazi ya kushirikiana na hawa vijana katika ufanyaji wa biashara. Haya yatasaidia vijana na itaweza kuwajengea uwezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia pia suala zima la matumizi ya vyeti wanapohitimu, viweze kutumika kuweza kuwapatia fedha. Sasa, idadi kubwa hii ya vijana tusipoitengenezea mazingira mazuri leo, kesho yao itakuwa ngumu na inaweza ikawa bomu la Taifa. Kwa hiyo ninaomba sana, katika hoja hizi zilizotolewa, ushauri wangu Serikali ianze kufikiria upya sasa kuleta Benki ya Maendeleo ya Vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuanzisha Wizara ya Vijana. Wizara hii ya Vijana imeanzishwa imetengewa takribani shilingi bilioni 200 ziko pale. Leo tungekuwa na benki ya maendeleo ya vijana fedha hizi zote zingewekwa pale, za kwenye kilimo kama kuna zinazowahusu vijana zingewekwa pale, asilimia nne za halmashauri zingewekwa kwenye Benki ya Maendeleo ya Vijana. Hatimaye vijana wa Taifa hili wakanufaika na wakaweza kujiajiri na kuja kutengeneza ajira nyingi kwa hapo baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nukta nyingine ya msingi ninayotaka kuchangia ni kuhusiana na suala zima la sekta binafsi. Sekta binafsi imekuwa ikifanya vizuri sana ndani ya nchi yetu na imekuwa ikichangia sana maendeleo ya nchi yetu na pato letu la Taifa, lakini yapo mambo ya msingi ambayo tunahitaji kuyaangalia kwa upana na kwa sura ambayo ni nzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa kiwango gani Watanzania wanaofanya kwenye sekta binafsi wananufaika, ambapo kundi kubwa bado ukienda huko ni vijana? Tarehe 13 Oktoba, 2025 Wizara ya Utumishi wa Umma ilitoa tangazo la kuongezeka kwa kima cha mshahara katika sekta binafsi, lakini ukiangalia kwa harakaharaka ukifuatilia mchanganuo uliowekwa kwenye lile Gazeti la Serikali, tangazo lile lililosainiwa na Mheshimiwa Waziri wa Utumishi wa Umma, ukipitia na ukiangalia hali halisi ilivyo huoni utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niishauri Serikali, sekta binafsi wakati inakua na maisha ya watu wanaofanya kazi ndani ya sekta binafsi, basi tuhakikishe nayo yanakua na mishahara ile iliyotangazwa kuongezeka ifuatiliwe iongezeke. Nitatoa mfano katika hili; Bandari ya Tanga kumefanyika uwekezaji mkubwa takribani shilingi bilioni 423, lakini kwa muda wa miaka 10 vibarua walioajiriwa pale kuna kampuni zimechukua *tender* ndani ya *TPA (Tanzania Ports Authority)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zile kampuni baada ya kuchukua *tender* kwa muda wa miaka 10, vijana wale wanalipwa kati ya shilingi 9,500 mpaka 11,000 na wapo vijana takribani 17,000. Tangazo la Serikali limetoka, *TPA* inazilipa zile kampuni vizuri kabisa, wale watu wanachelewesha mishahara kwa wale vijana, lakini mwisho wa siku kilichokuwepo ni kwamba mpaka leo wale vijana bado hawajaongezewa mishahara wala hawajaongezewa ujira wao kwenye vibarua. Hii ni changamoto wakati maelekezo ya Serikali yametoka na yametolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mawaziri wetu wanafanya kazi kubwa nzuri sana. Katika hili ninaomba waamke, wapite kwenye viwanda na kwenye sekta mbalimbali za binafsi waangalie maelekezo yaliyotolewa kutoka kwa Waziri wa Utumishi wa Umma, je,

yanatekelezeka ili hali za maisha ya wananchi wetu yazidi kustawi na kuboreka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nukta nyingine ya msingi ninayotaka kuchangia ni sehemu ya uvuvi. Niipongeze Serikali kwa kutoa boti na kuwasaidia wavuvi hususan watu wa ukanda wa bahari na sehemu ya maziwa; wanafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ninataka niliambie Bunge hili Tukufu, zaidi ya 80% ya uvuvi wa Tanzania ni *traditional*. Boti zilizopelekwa kule ni *modern*: boti zimepelekwa zina rangi nyeupe, wavuvi wanaenda kuvua usiku baharini wana karabai zao, kunatokea *reflection* ya *light* samaki wanatawanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi watu wa Pwani, unapoenda kuvua basi unapaka lile dau lako au mashua yako inaitwa sifa, iwe na rangi nyeusi kama rangi ya lami ili itengeneze kiza samaki wakusanyike karibu kwenye mwanga ili mwisho wa siku upate samaki wa kutosha ili mambo yaweze kwenda vizuri. Matokeo yake boti zile zimepelekwa, watu wanafukuzana na waliopewa boti kwa ajili ya marejesho, kumbe ukiangalia watu wameshindwa ku-c*onsider point* moja kwamba, uvuvi wetu 80% ni *traditional*, tunawapelekea vifaa ni *modern*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri katika hili ikiwezekana Wizara husika ikae na wavuvi kwanza iangalie *modality* kwenye maeneo yao husika ni aina gani ya boti wanazozihitaji kuliko kutumia gharama kubwa ya pesa na kuleta boti ambazo kwa namna moja ama nyingine mwisho wa siku zinakuwa hazina tija kwa wavuvi kulingana na ile sekta ya uvuvi jinsi ilivyo. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. KASSIMU A. MBARAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza haya, ninaunga mkono hoja. Shukrani sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana.

Nilimwita Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, atafuatiwa na Mheshimiwa Yumna Mmanga Omar na Mheshimiwa Martha Festo Mariki ajiandae.

MHE. AGNESTA L. KAIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili kwa uchache kabisa niweze kuchangia katika hoja ambayo ipo mbele yetu, hoja ambayo ni hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, sambamba na hotuba ya Bajeti ya Wizara ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninaomba kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha na kuniwezesha kusimama siku ya leo kwa mara nyingine kwa ajili ya kuleta sauti ya Wanajimbo la Segerea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ninayo pia historia ambayo ningependa kuieleza ndani ya Bunge hili Tukufu. Kwa mara ya kwanza kabisa katika maisha yangu jana nimeweza kushiriki katika mbio za Mwenge ndani ya Jimbo langu la Segerea na nimekesha mpaka asubuhi, niseme nimejifunza mengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa moja kwa moja niungane pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine ambao wameweza kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa yale ambayo anayafanya yeye kama Rais, ambayo yanaonekana kuwa na tija kwa maslahi mapana ya wananchi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niweze pia kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na hotuba yake nzuri, lakini nikiri kama Mbunge kwamba ameanza vizuri. Tumemwona akifanya ziara za hapa na pale, ziara ambazo kwa namna moja ama nyingine zimeleta faraja kubwa sana kutoka kwa wananchi wakiamini kwamba sasa wanaweza kupata faraja na tabasamu lile ambalo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amewaahidi kuwapatia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya hapo kwa harakaharaka nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI,

niwapongeze sana Manaibu wote kwa maana ya Naibu unaye-*deal* na masuala ya elimu na afya na Manaibu wote waliopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, hakika wanafanya kazi nzuri sana ambayo kwa kweli wanapaswa kupongezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mama Samia Suluhu Hassan, anafanya kampeni zake, alisema na aliwaambia Watanzania kwamba pale atakapokuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, zipo changamoto ambazo ndani ya siku 100 atakwenda kusimama kuhakikisha kwamba anatatua ili kuleta faraja na tabasamu kwa Watanzania. Pamoja na mengi aliyoyaahidi alisema moja kwa moja kwamba ndani ya siku 100 atakwenda kuhakikisha anamtua mwanamke ndoo kichwani. Wote tunafahamu dhana ya Mheshimiwa Rais, ya kumtua mwanamke ndoo kichwani haijaanza leo imeanza kipindi akiwa ni Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu hii alisema kwamba ataenda kuweka nguvu sana kuhakikisha kila mwanamke wa kitanzania habebi tena ndoo kichwani bali maji yanamkuta ndani ya nyumba yake. Wakati Waheshimiwa Wabunge wengine wakiwa wanalalamika na kusema kwamba katika majimbo yao wanapata maji kwa mgao, ninaomba nimwambie Waziri, ndani ya Jimbo la Segerea hatulilii mgao kabisa, tunalilia upatikanaji wa maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Wabunge wengine wanasema kwamba wanapata maji mara mbili kwa wiki, ninaomba nikwambie kwamba ndani ya Jimbo la Segerea kuna wananchi ambao mpaka hivi ninavyoongea wana miezi sita hawajaona maji safi na salama, lakini kuna wananchi wengine ni miezi 10 hawajaona tone la maji katika mabomba yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ninayoyaongea mbele ya Bunge lako Tukufu, Mheshimiwa Waziri wa Maji Aweso, atakuwa ni shahidi kwamba hiki ninachokisema ni ukweli mtupu na Mwenyezi Mungu anafahamu kwa sababu yeye mwenyewe ambaye amebeba ndoto za Mheshimiwa Rais, za kumtua mwanamke ndoo kichwani, ameiona hiyo changamoto ndani ya Jimbo la Segerea na alikuja mwenyewe kuweka kambi ndani ya Jimbo la Segerea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alijionea kwa macho, alisikia kwa masiko na akaelekeza kwamba, *DAWASA* iweze kuweka kambi ndani ya Jimbo la Segerea kwa sababu kero ya maji ndani ya Jimbo la Segerea imekuwa ni kubwa ukilinganisha na maeneo mengine. Kwenye hili ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Aweso, ni kwa bahati mbaya sana simwoni, lakini amefanya kazi kubwa sana. Mheshimiwa Aweso, akisikia sehemu yoyote kuna changamoto ya maji hata kama jambo hilo lipo nje ya uwezo wake kwa wakati huo atafika kusikiliza na atatoa mwelekeo. Ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Aweso lakini niwapongeze watendaji wote wa *DAWASA*, *engineer* Bwire na mameneja wote ambao wapo ndani ya kanda hii ya Jimbo la Segerea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeanza kwa kuelezea hiyo tathmini ili kuweka kumbukumbu sawa kwamba ndani ya Jimbo la Segerea wananchi wanalia na wana kiu wanahitaji maji safi na salama, kwa sababu Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliwaahidi kuwatua ndoo kichwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa harakaharaka nina ombi kwa upande huu wa maji. Kutokana na hali ilivyo kwa sasa, uzalishaji wa maji imekuwa ni changamoto kubwa sana na majuzi hapa nimemwona Mheshimiwa Waziri, akiwa kule China akifuatilia *pump* kwa ajili ya kuja kuzifunga ili kuhakikisha uzalishaji wa maji na usukumaji unakuwa na nafuu kubwa sana na hivyo wananchi kuweza kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa nilizonazo, *pump* nne tayari zimewasili ndani ya Nchi yetu ya Tanzania, ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam. Ombi langu pamoja na kazi nzuri hiyo, niwaombe Mheshimiwa Waziri na niseme nipo chini ya miguu yao kwa niaba ya Wanajimbo la Segerea, zile *pump* nne wanazosema kwamba zikifungwa zitakwenda kuleta nafuu kwa wananchi wa Dar es Salaam na hususan Jimbo la Segerea niwaombeni chonde chonde ziende zikafungwe ili akinamama wa Jimbo la Segerea wasiweze kubeba ndoo kichwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hilo nina ombi. Kuna ufumbuzi mwingine wakati mwingine unaweza ukawa wa dharura na mwingine ukawa ni wa muda mrefu. Ndani ya Jimbo la Segerea ukosekanaji wa maji safi na salama kwa sababu ni kilio kikubwa sana, ninaomba kwamba Mheshimiwa Waziri akubali kuja kutuchimbia visima vya kisasa virefu ndani ya kata zote 13. Kwa kuwa kazi hii wameshakwishaanza ndani ya kata mbili; Kata ya Kisukulu na Kata ya Segerea, ambao hawajapata maji zaidi ya miezi sita, niwaombe na nimwombe Mheshimiwa Waziri aje akatuchimbie visima kwenye kila kata wakati tunasubiri miradi mikubwa ambayo hatuna uhakika kwamba ni lini itakwenda kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo ninaomba niende moja kwa moja katika suala zima la *TARURA* kwa maana ya barabara. Wakati Wabunge wenzangu wanasema kwamba wanahitaji barabara za kuunganisha kutoka jimbo moja kwenda jimbo lingine, kutoka kata moja kwenda kata nyingine. Ninaomba nimwambie Waziri, ndani ya Jimbo la Segerea lenye mitaa 61, mitaa yote 61, hakuna mtaa hata mmoja unaopitika ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyoongea maeneo mengi yamefungwa, njia hazipitiki kabisa, ni barabara zote kiasi kwamba ninashindwa hata kukutajia kwamba ni barabara ipi na ipi ambayo ina changamoto kubwa zaidi. Kwa sababu nikianza kutaja barabara moja baada ya nyingine nitakuwa ninajichonganisha mwenyewe na wananchi wa Jimbo la Segerea, kwa sababu wanafahamu mitaa yote 61 haipitiki kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona katika hotuba hii ya TAMISEMI, bajeti imeongezeka ya *TARURA* imekuwa sasa shilingi trilioni 1.2 na wameelezea katika hotuba yao, wamesema kwa sasa hawana madeni kabisa kwa wakandarasi. Ombi langu Mheshimiwa Waziri, ninajua ni msikivu, chonde chonde hii fedha shilingi trilioni 1.2 ielekezwe kwenye majimbo ambayo njia hazipitiki kabisa. Mfano, nimwambie ndani ya jimbo langu tumepoteza watoto watatu kwa sababu mvua iliponyesha mafuriko yamekuwa ni mengi wameondoka na maji Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Kimanga tumezika mtoto mdogo, Kata ya Kinyerezi watoto wawili. Mheshimiwa Waziri, nimwombe chonde chonde hii shilingi trilioni 1.2 ielekezwe kwenye majimbo ambayo changamoto yake ni kubwa, ninamwomba aanze na Jimbo la Segerea. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa....

MHE. AGNESTA L. KAIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Mheshimiwa muda wako umekwisha.

MHE. AGNESTA L. KAIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalizie.

MWENYEKITI: Malizia kwa haraka, *wind up*.

MHE. AGNESTA L. KAIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati namalizia kwenye Kata ya Kipawa katika Mtaa wa Kipunguni; kuna wananchi waliopisha ujenzi wa *airport* mpaka leo ninavyoongea hawajalipwa fidia, wanaishi katika mazingira magumu, hata huduma za kijamii hawazipati kwa sababu mazingira ni mabaya, ni mabaya. Ninaomba kwa haraka niseme kama ifuatavyo...

MWENYEKITI: Aaah! Usianze kutaja majina, Waziri ameshasikia *compensation*, malizia bila ya kwenda kwenye *list*.

MHE. AGNESTA L. KAIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Jambo la mwisho sasa ni kuhusiana na stahiki za Waheshimiwa Madiwani pamoja na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa. Kwa dakika moja ninaomba niseme, Waheshimiwa Wabunge, wote wanafahamu wakati mimi ni Mbunge wa Viti Maalum sikujua kama kuwa Diwani ni kazi kubwa sana na kuwa Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa ni kazi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, aangalie namna ya kuwasaidia hawa Madiwani, Diwani kulipwa shilingi 350,000 halafu unampelekea mradi wa mabilioni na mamilioni ukiamini atausimamia wakati ana njaa kali, haiwezekani kabisa Mheshimiwa Waziri...

MWENYEKITI: Haya, ahsante.

MHE. AGNESTA L. KAIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, wenyeviti wa Serikali za Mitaa wanapewa shilingi 100,000 kwa mwezi Mheshimiwa Waziri, hii siyo sawa...

MWENYEKITI: Ahsante...

MHE. AGNESTA L. KAIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, na haiendani na kauli ya Mheshimiwa Rais, anayosema: "Utu na Kazi, Tunasonga Mbele", utu utangulizwe kwa Wenyeviti wetu pamoja na Waheshimiwa Madiwani...

MWENYEKITI: Haya, shukuru....

MHE. AGNESTA L. KAIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana, tunakwenda na muda. Waheshimiwa nilimwita Mheshimiwa Yumna Mmanga Omar, atafuatiwa na mchangiaji wetu wa mwisho Martha Festo Mariki.

MHE. YUMNA MMANGA OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi hii. Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema ya uhai na uzima, lakini kwa kunipatia kibali cha kuwa miongoni mwa Wabunge wa Bunge hili la Kumi na Tatu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa heshima kubwa nipende kumshukuru kipenzi chetu Mama yetu, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha nimshukuru pia Mama yetu, mlezi wetu Mama Mary Pius Chatanda, kiongozi na Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania kwa uongozi wake ulio thabiti na kutulea sisi mabinti na wanawake ndani ya jumuiya hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo sasa nielekee moja kwa moja kwenye kuchangia hoja iliyopo mezani ambayo ni hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mimi nitagusia vipengele viwili ambavyo ni sekta ya elimu na sekta ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijakwenda moja kwa moja nipende tu kuipongeza Serikali kwa hatua kubwa za maendeleo inayoendelea kuzipiga katika sekta hizi. Pia, kama Taifa tulipo sipo tulipotoka, lazima tukiri hilo ila sipo tunapotaka kufika. Kwa hiyo inatulazimu tuseme ili tuweze kufikia kule tunapotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, inazungumzia kwamba kupitia Wizara ya Elimu, Serikali imetenga shilingi bilioni tisa kwa ajili ya ufadhili wa wanafunzi kwa masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi, sambamba na Hisabati ambapo Serikali imefadhili wanafunzi 1,786. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imetoa pia shilingi bilioni tano kwa *Samia Super Scholarship Fund* kwa wanafunzi 50 bora kwa sekta ya akili unde na Sayansi *data*. Hapa napatwa na maswali, kwenye ufadhili huu wanafunzi wenye ulemavu wamefikiwa kwa kiasi gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunafahamu kwamba, ndugu zetu watoto wetu wenye ulemavu wanakumbana na changamoto mara tatu zaidi kuliko wanafunzi wengine, kuanzia elimu ya msingi hadi elimu ya juu na ndiyo maana hata ukitazama takwimu zimejichora kabisa *pyramid* kwamba huku ngazi ya chini wanakuwa wengi, lakini kutokana na changamoto mbalimbali ikiwemo miundombinu, vifaa saidizi, uelewa, mazingira, vinawarudisha nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kumwangalia mwanafunzi mwenye ulemavu ambaye amepata *division two,* ukam-*recognize*

sawasawa na asiyekuwa na ulemavu ambaye ana *division one*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila shaka huyu ametumia nguvu mara tatu zaidi afikie pale *highest of his/her potential*. Kwa hiyo, ni ombi langu kwa Serikali kuhakikisha kwamba fursa hizi tunaweka mikakati madhubuti *(affirmative measures)* ambazo zitaongeza ushiriki wa wanafunzi wenye ulemavu kwenye fursa hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukizungumzia *science technology engineering and mathematics* ni uchumi wa nchi, tunapoliacha kundi hili nyuma, maana yake tunawaacha nyuma katika ushiriki wao wa uchumi ndani ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuendelea mbele nigusie sekta ya afya; ambapo tumeona Serikali kwa kuimarisha ubora wa sekta ya afya nchini, imesomesha madaktari bingwa na bingwa bobezi kwenye kada mbalimbali. Nipende tu kutoa ushauri wangu kwa Serikali kwamba madaktari hawa waende wakagusie kada ambazo zinatugusa sisi watu wenye ulemavu moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaathiriwa na mionzi ya jua; mionzi hiyo hupenya hadi kupitia kioo, hata kunapokuwa na mawingu ya mvua, bado hupita. Hivyo basi, ninahitaji kuwa na *periodic check up* ambazo zitaniwezesha kuangalia uwezo wa ngozi yangu, kwa kuwa ninafanya kazi siwezi kuepuka jua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama binadamu ninakonda, ninanenepa, ninakua ule mguu bandia ambao umenipatia unaweza ukawa haunitoshi ni lazima niende kwa daktari kila baada ya muda akaangalie, aniongezee, anipunguzie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zetu wenye ulemavu wa uziwi pia wanahitaji kwenda kwa daktari kuangalia zile shime sikio waliozopatiwa zinawasaidia? Wapewe nyingine. Ndiyo maana idadi kubwa ya ndugu zetu wenye ulemavu wa uziwi hawataki kutumia shime sikio kwa sababu madaktari hawa hawapo ni pungufu kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, ni mapendekezo yangu kwa Serikali kuhakikisha kwamba wanaongeza madaktari bingwa kwenye kada hizi ili kupunguza, lasivyo tutakuwa tunaongeza *intensity* ya ulemavu kwa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie kwamba, tunapoandaa bajeti zetu tuhakikishe kwamba hizi bajeti zinakuwa *inclusive budget* ili katika kila eneo tuone ni kwa namna gani tunatenga fedha kuwajumuisha watu wenye ulemavu kwenye sekta ya afya, kwenye sekta ya elimu, kwenye sekta ya michezo katika kila eneo pamoja na zile *key performance indicators* ili tuone kama Taifa tuko wapi na tunahitaji kwenda wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, sisi kama Taifa, sisi kama Wabunge humu ndani kila mmoja ana haki na wajibu wa kuzungumzia watu wake, nami kwa niaba ya watu wenye ulemavu, ninaunga mkono hoja pamoja na mapendekezo hayo. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Nimwite mchangiaji wetu wa mwisho, Mheshimiwa Martha Festo Mariki.

MHE. MARTHA F. MARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia katika hotuba ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge hili Tukufu katika Bunge hili la Kumi na Tatu, nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetujalia uzima na afya njema na Mwenyezi Mungu aliyeniweza kurudi katika Bunge hili la Kumi na Tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze pia kwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya katika Taifa letu la Tanzania. Sisi Wananchi wa Mkoa wa Katavi tunampongeza sana na tunamshukuru sana kwa namna ambavyo ametupa kipaumbele katika miradi mbalimbali ya

maendeleo ikiwepo afya, elimu, kilimo na mambo mengine mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee sana nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo ametupigania sisi wananchi wa Mkoa wa Katavi katika kipindi chake cha uongozi wake ameweza kuacha alama kubwa sana ambayo wananchi wa Mkoa wa Katavi tutamkumbuka kwa jinsi ambavyo ametusaidia kutuunganisha katika gridi ya umeme ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hilo limetuwezesha wananchi wa Mkoa wa Katavi kuweza kuvutia wawekezaji kuja ndani ya Mkoa wetu wa Katavi na ukizingatia Mkoa wetu wa Katavi sisi ni wakulima wazuri na tuna biashara nyingi na hivyo kutokana na umeme kuwa wa uhakika sasa viwanda vingi vinakwenda kujengwa ndani ya Mkoa wetu wa Katavi. Hivyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mkoa wetu wa Katavi wanaendelea kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo ameboresha sekta ya afya, sekta ya afya tunajua inawagusa sana wananchi wote, lakini akinamama na watoto imewagusa kwa kiasi kikubwa. Kwa kuzingatia kwamba katika kipindi cha uongozi wake vifo vya mama na mtoto vimepungua kwa kiasi kikubwa ndani ya Mkoa wa Katavi hivyo tunampongeza sana na tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze katika hotuba ya Waziri Mkuu, nianze kwa kumpongeza Waziri wetu Mkuu kwa jinsi anavyofanya kazi alikuja ndani ya Mkoa wetu wa Katavi kufanya ziara na tuliona kazi kubwa anayoifanya hivyo tunampongeza sana, lakini tunampongeza kwa hotuba nzuri aliyoitoa katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunatambua Serikali na jitihada zake katika kuwezesha wanawake kiuchumi pamoja na vijana na watu wenye ulemavu. Katika suala la 10%, wananchi wa Mkoa wa Katavi hususani akina mama, vijana na watu wenye mahitaji maalum wanatoa shukrani za dhati kwa Serikali kwa jinsi ambavyo imesimamia

halmashauri zetu kuwawezesha akina mama hao, vijana na watu wenye mahitaji maalum kuweza kupata mikopo ya 10%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Mkoa wangu wa Katavi tulipoenda kuinadi Ilani ya Chama Cha Mapinduzi; tulipokwenda kuomba kura, takribani zaidi ya shilingi 9,000,000,000 zilikuwa zimeshatolewa katika vikundi hivi vya akina mama, vijana na watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi kuiomba sana Serikali, bado kuna changamoto, tunahitaji katika mikopo ya 10% tuweze kufanya maboresho katika maeneo machache. Wako akina mama wenye watoto walemavu; akina mama hawa wanapokwenda katika vikundi vya kawaida vya akina mama wengine wamekuwa hawapati fursa na kutengwa kwa sababu wana watoto wenye ulemavu *critical* unaosababisha wao kutoshiriki vizuri katika shughuli za uzalishaji; hivyo, akina mama wale wengine huona kwamba wakiwaunga katika vikundi vyao hawataenda sambamba na wao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, ombi langu lilikuwa ni nini? Ombi langu lilikuwa ni kwamba tuangalie akina mama hawa ambao wanawalea watoto wenye ulemavu hususani ulemavu ule *critical* kwamba ikiwezekana waweze kuingizwa katika ile asilimia mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lililopita nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya *LAAC,* tulikuwa tukishuhudia kwamba baadhi ya fedha za watu wenye mahitaji maalum zilikuwa fedha zile haziishi. Kwa nini, sasa Serikali isije na mpango wa kuunganisha akina mama hawa katika ile asilimia mbili kwa kuwa wanapoteza sifa ya kuunganishwa na akina mama wenzao? Kwa kuwa wanatumia muda mwingi wa kuangalia watoto wao katika majumba yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalotaka nishauri; ni kutokana na Sheria ya Mwaka 2018, katika kifungu cha 37A sheria hii inasema kwamba mikopo hii itolewe ndani ya siku 90, siku hizi ni nyingi sana, tuombe Serikali iweze kuangalia. Kuna baadhi ya maeneo kama Mkoa wangu wa Katavi akina mama wanavyojaza mikopo hii

unakuta mama ame-*target* kwamba afanye biashara ya mpunga, lakini unakuta mpaka muda wa msimu wa biashara umepita, ndio mikopo hii inatoka ndani ya siku 90 ikiwezekana mikopo hii iweze kufupishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tulikuwa tunaomba hawa Maafisa Maendeleo waweze kuwafuata akina mama hawa katika kata zao au katika tarafa kwenda kuwapa mafunzo badala ya kuwakusanya katika halmashauri ili waweze kuwapunguzia adha za kutoa nauli na gharama kubwa kwani wengine wamekuwa wakitokea katika maeneo ya mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine wananchi wa Mkoa wa Katavi, wamenituma kwamba wanaomba sana Serikali iendelee kuwaangalia katika kuunganisha barabara za mikoa na mikoa. Tunaishukuru Serikali tumeunganishwa wananchi wa Mkoa wa Katavi kutoka Mpanda mpaka Tabora, tunaishukuru sana kwa kiwango wa cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya Wanakatavi tuunganishwe na Barabara ya lami kutokea Mpanda kwenda Kigoma kupitia Vikonge - Luafe mpaka Mishamo na Uvinza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii tukiunganishwa kwa kiwango cha lami itakwenda kutufungua sisi wananchi wa Mkoa wa Katavi tuweze kufanya biashara zetu vizuri. Ukizingatia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshatujengea bandari ya kisasa, Bandari ya Karema ambayo imekwenda kutuunganisha sisi na wananchi wa Kongo ambapo tunakwenda kuwa ma-*giant* katika kufanya biashara, wananchi wa Mkoa wa Katavi. Hivyo, ombi letu ni kuunganishwa na barabara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo barabara yetu ya kutoka Kibaoni – Sitalike; katika Jimbo la Kavuu tunalima sana mpunga, sote ni mashahidi. Wananchi wa Mkoa wa Katavi wanaotazama nikiwa ninaongea hapa, wanaelewa kwamba katika Jimbo la Kavuu ukienda utakuta watu wa nchi jirani wamekuja kufuata mchele wa Mkoa wa Katavi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ile bado ni kizungumkuti; hata Mheshimiwa Waziri Mkuu, alivyokuja ametuahidi kwamba fedha zipo na Serikali imeshatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ile kilometa 51. Tuombe Serikali itusaidie kupitia Wizara ya Ujenzi, barabara hii iweze kukamilika kwani mkandarasi amekuwa akisuasua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya akina mama wa Mkoa wa Katavi, tunaendelea kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan; na nimalizie kwa kuwashukuru sana akina mama wa Mkoa wa Katavi kwa imani kubwa waliyonipa na kunirudisha katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ninaahidi kwamba sitawaangusha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kumshukuru pia Mkuu wa Mkoa wangu Mheshimiwa mama Mwanamvua Hoza Mrindoko, kwa kazi kubwa anayoifanya; lakini Mwenyekiti wangu wa UWT Taifa kwa kazi kubwa aliyoifanya, kuhakikisha kwamba tunapata ushindi. Ninashukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana, kwa mchango wako Mheshimiwa Mariki.

Waheshimiwa Wabunge, tumefikia mwisho wa shughuli yetu ya leo na hatuna matangazo. Hata hivyo, kuna jambo moja ningependa kulisemea kwa kuwa limejitokeza.

Waheshimiwa Wabunge, kama Mheshimiwa Spika alivyowahi kutoa mwongozo hapa siku moja, Bunge hili lina uhuru wa mawazo kwenye majadiliano yake, ambao unalindwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 100.

Waheshimiwa Wabunge, tukumbuke kwamba kanuni zetu zinaweka wajibu wa Mbunge, anapochangia kuhakikisha anasema jambo analoliamini kuwa ni kweli. Aidha, kazi ya Kiti ni kusimamia kanuni hizi ili Bunge letu liendelee kutamalaki, kuwa na heshima na hadhi yake. *(Makofi)*

Sasa kuna kauli moja imesemwa hapa ningependa niiseme kidogo, Mbunge anapochangia na kusema kwamba jimbo langu au mkoa wangu au kijiji changu ndiyo kinaongoza duniani kwa kuwa na barabara za vumbi, busara inakutaka uoneshe utafiti kuwa umetafiti mwenyewe au ukarejea utafiti, ili kulipa hadhi jambo unaloliongea. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ni vizuri kutokutumia mifano ya kujilinganisha, sisi na dunia nzima kama hatuna utafiti; ni kwa sababu tunataka Bunge letu liwe ni Bunge ambalo linaongea vitu kwa uhakika. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, ninaahirisha Shughuli za Bunge mpaka siku ya kesho, Jumatano tarehe 15 Aprili, 2026, saa 3.00 asubuhi.

(Saa 1.51 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 15 Aprili, 2026 Saa Tatu Asubuhi)